ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaybah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.

35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
47.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.

49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.

69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 06 Julai, 2010

(Mkutano ulianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti, (Thuwaibah Edington Kissasi) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 99

Uzito Mkubwa wa Magari

Mhe. Said Khelef Ali Kny (Mhe. Haji Mkema Haji) - Aliuliza:

Tunaipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika jitihada zake za ujenzi wa barabara nzuri na kubwa Unguja na Pemba. Madhumuni makubwa ya kujengwa barabara hizi ni kukuza maendeleo ya kiuchumi na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za kijamii. Lakini hivi sasa barabara hizi hupitishwa magari ya uzito mkubwa unaopindukia tani 200.

Mhe. Waziri, Je, barabara hizi zimejengwa kuhimili uzito wa magari ya uzito huo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yoe kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria Kikao cha Baraza na kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 99 kama ifuatavyo:-

Napenda kumjulisha Mhe. Mwakilishi kuwa barabara zetu nyingi zinajengwa kuhimili uzito wa magari ya tani kumi (10 *tons*). Huu ni uzito wa *AXLE LOAD.*

AXLE LOAD" ni taminologi ya kitaalamu ambapo uzito hupimwa kwenye matairi ya kwenye axle. Si hoja gari kuwa kubwa bali kinachoathiri barabara ni huo uzito wa mipira kwenye *axle.* Hii ndio maana utaona kuwa magari makubwa ukayaona yana "axles" zaidi ya tatu au nne. Sababu ni kuwa uzito wote huwa unagawanywa kwenye utaratibu maalum ili kila "axle" isizidi tani hizo zilizokusudiwa kimuundo. Aidha upande wa mizigo au abiria kwenye

magari makubwa pia husaidia kuondosha tatizo la kuzidi uzito kwenye *axle*. Hivyo nadhani kuwa Mhe. Mwakilishi atakubaliana nami kuwa hapa Zanzibar hakuna magari yanayopitishwa barabarani yenye uzito mkubwa unaopindukia tani 200.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, mimi bado naipongeza Wizara kupitia Idara ya Ujenzi na Utendaji Barabara kwa kuhakikisha kwamba serikali inajitahidi katika kazi zake juu ya kuwaondolea adha wananchi katika huduma ya usafiri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa wenzetu kuiga mema mara nyingi miye huwa napenda. Kwa wenzetu Tanzania Bara na Kwengineko wana mpango maalum wa viwango vya uzito kwa kupimia usito wa magari na bidhaa iliyokuwemo ili kunusuru usalama wa barabara zile. Pamoja na kwamba swali hili kuulizwa kwamba kuna mtiririko wa magari mazito sasa hivi kupindukia kiwango, je, Wizara ina mpango gani wa makusudi labda kuanzisha mpango huo ambao baadaye utaleta haja na utakidhi kuzilinda barabara zetu zisife kwa muda mfupi.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimpongeze Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihada) kwanza nataka nimpongeze kwa kutupongeza Wizara yetu. Lakini pia katika kujibu swali lake ushauri wake tutauchukua na tutaufanyia kazi.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri kwamba Wizara ya Mawasiliano yenyewe ina kifaa kinachoitwa *low loader* ambacho hupakia zana nzito zenye uzito mkubwa.

(a) Je, ana hakika kwamba *low loader* hauchukui uzito zaidi ya ule ambao unakiwango cha barabara zinavyojengwa.

(b) Je, yale maburdoza na vifaa vyengine vinavyopakiwa vinauzito gani.

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Waheshimiwa Wajumbe wamemsikia Naibu Waziri akijibu utaratibuu wa hizi gari zenye uzito mkubwa na mambo mengineyo.

Mheshimiwa *low loader* na magari makubwa yote ambayo yanayochukua mizigo kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri yana *axel* katika kila *axel* utaona kuna uzito wa tani, hata ile *low loader* yetu utaona ina maringi pengine zaidi ya sita au manane kwa hivyo kila sehemu inauzito wake. Kwa hivyo hakuna uzito ambao mpaka sasa hivi unaathiri barabara zetu.

Kuhusu kuwa na *way brag* nafikiri katika *master plan* yetu jambo hilo lipo na sasa hivi tunaye mtu mmoja anaitwa Baharesa anayo hiyo *way brag* kwa hiyo kama kuna shaka fulani tunaweza kwenda kupeleka gari kwenda kuipima. Lakini kwa hakika hadi sasa hivi hatujaona tatizo hilo.

Nam. 89

Daladala za Fuoni Jitimai

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu – Aliuliza:

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa mimi naishi ndani ya Jimbo la Fuoni kwa muda wa miaka 11 saa. Na kwa kuwa suala la daladala jana lilizungumzwa sana na waheshimiwa wajumbe wako lakini halijapata jibu.

Daladala zenye ruti iendayo Fuoni Jitimai hazifiki kwenye kituo cha mwisho kilichopangwa kuishia daladala hizo na siku zote huishia Fuoni Kiembeni kwenye njia ya kuendea Jitimai. Pamoja na ukweli kwamba barabara hiyo ni mbovu, ni lazima kwa kuzingatia shida za wananchi, usalama wa waendao kwa miguu nyakati za usiku na umbali uliopo kutoka Fuoni Kiembeni hadi Fuoni Jitimai.

(a) Je, Serikali kwa nini isisimamie wenye dala dala ili wafike ruti yao inakomalizia.

(b) Ili kuondo kabisa tatizo hilo kwa wakaazi wa eneo hilo kwa nini Serikali isifanye mpango wa dharura wa kuitengeneza barabara hiyo hasa ikizingatiwa kuwa hivi karibuni kutafanyika IJITIMAI kubwa ya Kimataifa.

(c) Kwa kuwa hivi sasa daladala hazifiki kwenye kituo cha mwisho kilichopangwa, Je, Wizara yako inatoa wito gani kwa wenye daladala.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 89 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kuwa Wizara yangu kupitia Idara ya Usafiri na Leseni haina taarifa ya kuwa Daladala zenye ruti iendayo Fuoni – Jitimai hazifiki kwenye kituo cha mwisho kilichopangiwa kuishia daladala hizo. Hata hivyo kwa kuwa taarifa hizo zimeshaletwa katika Wizara yangu,

Wizara yangu kupitia taasisi husika italifuatilia na kuhakikisha gari hizo zinafika katika ruti yake iliyopangiwa. Vile vile kwa gari yoyote ambayo itabainika kutotekeleza agizo hilo Wizara yangu itaichukulia hatua ya kuizuia kufanya biashara hiyo kwa muda wa mwezi mmoja. Aidha Serikali inatarajia kuifanyia matengenezo ya dharura barabara iendayo Fuoni – Jitimai ili iweze kupitika kwa kipindi chote.

Nam. 101

Ardhi Ichimbwayo Kifusi kwa Ujenzi wa Barabara

Mhe. Said Khelef Ali Kny (Mhe. Haji Mkema Haji) - Aliuliza:

Katika ujenzi wa barabara kubwa, Serikali hutoa ardhi ya kuchimba kifusi bila ya kuwatoza fedha zozote wakandarasi wa ujenzi. Aidha tumezoea kuona ya kwamba wakandarasi hao wakiondoka kifusi, kokoto na eneo lililochimbwa kifusi au kokoto hizo hurudishwa Serikalini. Aidha hata majengo yaliyotumika wakati wa ujenzi yaliyotumiwa na wakandarasi hukabidhiwa Serikali.

(a) Kwa nini wakati wa ujenzi wa barabara ya Kitope hadi Kidimni mkandarasi aliachiwa kusombwa majengo aliyotumia.

(b) Kwa nini “Quary” ya ubago iliyotumika kuchimba kifusi imeuzwa kwa mtu binafsi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 101 lenye kifungu (a), na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Napenda kulifahamisha Baraza lako tukufu kuwa suala la Mkandarasi kupewa eneo la kuchimba kifusi linakuwemo ndani ya Mkataba baina ya Serikali na makubaliano baada ya kumalizika kwa mradi husika. Aidha majengo anayojenga Mkandarasi kwa ajili ya usimamizi hukabidhiwa Serikali mara baada ya kazi husika kukamilika. Kutokana na maelezo hayo ni napenda kumthibitishia Mhe. Mwakilishi kuwa Majengo aliyojenga Mkandarasi wakati wa ujenzi wa barabara ya Kidimni – Kitope bado yapo Kiyanga na yanatumiwa na Wizara yangu. Aidha suala la kuuza maeneo haliko katika Wizara yangu hivyo sitokuwa na jibu sahihi la suala hilo.

Mhe. Moh’d Ali Salum: Ahsante Mhe. Mwenyekiti naoma nimuulize Mhe. Naibu Waziri. Kwa kuwa wakandarasi huchimba kifusi katika maeneo mbali mbali wanayopewa wachimbe kifusi wanapojenga barabara. Kwa kuwa

maeneo yale huwa yanaharibika na wananchi huathirika ama kiuchumi au kwa njia nyengine yoyote ile kutokana na athari yakuchimbwa kifusi au mawe katika maeneo yale. Je, wananchi wale wanapata fidia gani ya kuondoa athari wanayoipata katika uchimbaji wa kifusi kile au mawe.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, wakati wowote wa mradi wa ujenzi wa barabara unapofanyika suala la kwanza mabalo tunakuwa tunalifanya Wizara ya Mawasiliano ni kuangalia maeneo ya upatikanaji wa kifusi. Baada ya maeneo hayo kupatikana taratibu za kawaida za kuwatafuta wamiliki wa eneo hili na fidia huwa zinatolewa. Tunapitia watu wa Wizara ya Kilimo wanatutathminia na baadaye sisi watu wa Mawasiliano tunawalipa. Kwa hivyo hakuna tatizo la malipo kwa wanaohusika.

Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim: Nashukuru Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja la nyongeza. Nataka kuuliza wizara je, mnakuwa na utaratibu gani wakati mnapoandika mikataba kwa hawa wanaochimba vifusi. Mfano Kwambani limechimbwa shimo pale mpaka pamechimbuka maji lakini na Michamvi vile vile kuna shimo kubwa sana. Katika mikataba yao hawaandiki kwamba huyu mjenzi akimaliza kazi ayafukie mashimo yale.

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, miradi yote ya ujenzi wa barabara inahusisha watu wa Mazingira, lazima tupate ripoti ya mazingira ndio tufanye mradi. Kwa kawaida kuna kiwango maalum cha kwenda chini kuchimba kifusi.

Kuna baadhi ya maeneo wakandarasi wahakikishe wameyarejesha kama kawaida mengine hawakuyarejesha. Kwa sababu pia kuna tatizo la wananchi wenyewe pengine na serikali za Mikoa kwamba sisi tukichimba na wao wanataka kwenda kuchimba hapo hapo. Kunasehemu nyengine tumewalipa fidia sisi lakini bado Serikali za Mikoa wakauza maeneo hayo. kwa hivyo wakati mwengine inakuwa shida inatukabili sote kwa upande mmoja.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na Mungu akupe heri. Mhe. Mwenyekiti, majibu ya Mhe. Waziri amesema kwamba maeneo ambayo yanatolewa vifusi wananchi walioathirika huwa wanapewa fidia.

(a) Nikitaka kujua tangu mwaka 1999 ambapo Mwambe ilitoa mchango mkubwa wa kuchimba mawe, vifusi na kokoto kwa ajili ya kujenga gati ya Mkoani hadi hii leo inaendelea kutoa mchango huo na mashimo tayari yanafikia mita saba na zaidi kwenda chini. Ni wananchi wangapi wamepata fidia kutokana na uchimbaji huo wa kifusi.

(b) Kwa kuwa sasa baada ya kumaliza kifusi sasa tumeanza kupata neema ya maji kutoka chini mtaendelea kuchimba mita ngapi ili tuweze kupata bahari katika maeneo yale.

(c) Hivi mkitoa miradi ya barabara na miundombinu mengine Makampuni hayapewi masharti ya kuzingatia umuhimu wa mazingira na kama wanapewa masharti nini hatua ya serikali juu ya makampuni hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza lazima nikiri kwamba suala la Muwambe ni suala maalum ni suala la kipekee na pengine Mhe. Hija analitambua. Kwa muda wa hiyo miaka tisa aliyosema kuna mtu kazunguka kwa Waheshimiwa Wawakilishi mpaka Mahakamani kudai kwamba ni eneo lake lakini kote kaambiwa sio lake. Sasa inawezekana Mhe. Hija bado hajaridhika na maamuzi yale ya Kimahakama, lakini sisi taratibu tulizonazo kaje kwetu, kenda Wizara ya Maji, kenda Mahakamani lakini bado anaambiwa hili sio eneo lake. Kwa hivyo kwa suala hilo hatujaweza kumlipa kwa saabu hizi ni fedha za serikali hatuwezi tukatoa tu kwa sababu mtu anadai. Kwenye mibuyu yote ile ya Mwambe anasema mibuyu yake, pengine ilikuwa yake wakati anafanya shughuli zake lakini sio kwa ardhi ile.

Kuhusu uchimbaji nimeshasema kwamba kwa kawaida sisi hatuna ataalamu wa mazingira sisi tunaongozwa na watu wa mazingira, wanaturuhusu wao chimbeni kiwango gani. Pemba pengine ukanda wote ambao nimetembea sehemu ya Mashariki ya Pemba una matatizo ya mazingira na sio kuchimba kifusi tu lakini ukataji wa mawe ndio mbaya zaidi katika ukande ule kuanzia Mwambe, Vitongoji, mpaka Kangagani, Ole huko kote huko kumeumizwa sana kwa ukataji wa mawe. Sasa hili nalo tujiulize je linalofaida kwa nchi yetu.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2010/2011
Wizara ya Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kupata nafasi hii ya mwanzo nichangie Bajeti hii ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi nikiwa kama ni mwanakamati wa Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina budi kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na uongozi wake wote kwa jumla kwa kufikia ufanisi wa kazi zake. Shukurani za

pekee zimfikie ndugu Ali Twahir Fatawi kwa mchango wake mkubwa sana waliotusaidia sisi twenye majimbo kwa kutujengea barabara, japo wengine tumepata kwa njia yakifusi lakini tunashukuru ametung'arisha katika majimbo yetu. Hongera Mheshimiwa.

Nitaanzia na sekta ya usafiri wa nchi kavu. Ukurasa wa 12 kwa kweli tumetembelea barabara nyingi za Unguja na Pemba ambazo zimefanyiwa kazi kwa kipindi hichi kifupi. Lakini mvuto wangu zaidi ulilenga kwenye barabara za Pemba zile ambazo zimejengwa kwa bei nafuu kwa kushirikiana na *contractor* iliyoshiliriki kwenye mradi, barabara zile zimejengwa kwa lami na maji. Nahisi kwa mfumo ule barabara hazitumii pesa nyingi kwa hiyo hasara serikali haingii inakuwa ni hasara ndogo tu. Napendekeza ule mfumo wakimaliza kule tuje na huku kwenye hizi barabara ndogo ndogo na barabara nyengine ambazo zilizobakia. Kwa vile serikali haili hasara kubwa ukilinganisha na kutengeneza barabara kwa lami.

Ukurasa wa 24 nashukuru nimeona haya mafunzo ya konda. Kwa kweli konda na madereva wanaona yale matusi ndio ukonda na ndio udereva. Watu wengi wanakuwa wana hasira kwa zile lugha zao au kauli zao wanazozitumia wakati wakiwemo kazini. Kwa hivyo namshukuru Mhe. Waziri hili zoezi alifanye kwa muda mfupi tu ili hawa watu warekebishike na hii tabia. Namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kulipendekeza hili pamoja na uongozi wake.

Ukurasa wa 33, Mamlaka ya Usalama na Usafiri wa Anga. Tulivyotembelea hii mamlaka inafanya kazi vizuri sana, kuziongoza ndege kwenye mwendo wake, kutua na kuruka. Hata nimefarijika sana na nimefurahi sana kuona hichi chombo cha mtambo wa kuongozea ndege ambacho kitanunuliwa hivi karibuni. Kwa vile uwanja wetu tayari utakuwa umepanuka na umekuwa mkubwa ndege nyingi zitaingia za Kitaifa na za Kimataifa. Hicho chombo kitatusaidia sana ambacho kinatumia mtambo huo ili kuboresha uwanja wetu na huduma zatu za anga.

Usumbufu wa wafanyabiashara, namuomba Mhe. Mwinyi Haji na Mhe. Waziri wa mawasiliano wakae pamoja ili kuondoa suala la usumbufu kwa wafanyabiashara. Bado nasema wafanyabiashara wanasumbuka, wale wanaotoka nje kurudi kwao Zanzibar. Kwa kawaida tukirudi tunakuwa na. mizigo *hand luggage* zile wangine wana 100, wengine wana 80, wengine wana 70.

Na Mashirika ya Ndege yamekubali kufanya *conection* baina ya Shirika moja kwenda jengine mfano kama Emeret na Qutar zile zinatuwa Dar-es-Salaam hazifiki huku. Kwa hivyo pale madhali wamekubali. wanaungana na *Precision* ile mizigo yote isiishie pale kwa sababu pale sio mwisho wa safari, safari yetu

sisi mwisho Zanzibar. Ile mizigo madhali ina *tag* waichukue waiingize Zanzibar sio kuipitisha kwenye *Precision*, *Precision* ni kilo 27 tu sasa zile zilizobaki inakuwa unazinunua tena kilo Sh. 3500/= Je, kama una kilo 100 faida iko wapi hapo. Tumeingiza nini. Kwa hiyo usumbufu bado tunao.

Nawaomba mawaziri hawa wawili wakae pamoja na Mashirika ya Ndege Emeret na *Precision* inayofanya *conection* walizungumze hilo. Pale unaweza kulipa Mhe. Mwenyekiti, hata kama laki tatu unaweza kuzitoa kwa mkupuo au unaamua bora usamehe mzigo. Lile ni tatizo, tena ni tatizo kubwa sana.

Afisi ya Mrajisi wa Meli, kwa kweli nampongeza mrajisi wa meli kwa kazi zake nzuri ambazo anazifanya kutafuta soko, kupanua hii biashara na kuingiza mapato serikalini. Kwa kweli wanastahili sifa na aendelee kusajili hizi meli za kimataifa na kuongeza zaidi kutafuta soko zaidi. Na kwa vile *conection* itakuwepo na uwanja wa ndege utakuwa tayari nahisi tutaendelea zaidi kuingiza zaidi kwenye nchi yetu.

Ukurasa wa 38 Bandari nampongeza sana Mkurugenzi wa Shirika la Bandari kwa kazi yake nzuri. Kwa niaba ya wafanyabiashara wanakupongeza sana. Mizigo yao siku hizi ya Makontena yanafika kwa wakati muwafaka na yanaondoka kwa wakati muwafaka na mizigo wanaipata kwa wakati mzuri na haichelewi mizigo pale wanaipata mara moja kuuza au kusafirisha na kuagizishia nyengine. Kwa hivyo hili hongera kwa kupata *truck deal* zinazofanya kazi kinyume na kawaida.

Usafiri Baharini tunashukuru kwa kuwapa maelekezo hao wenye vyombo vya baharini. Nakusudia maboti. Ilikuwa wanahisi kazi kubwa sana lakini sio kazi kubwa ni kazi nyepesi ilimradi tunafata *instruction* ili kupata kukaa kwenye mpango mzuri wa usafiri. Wasione tabu bado waendelee na mawazo yetu kama vile wasijaze abiria kupita kiasi. Hili ni tatizo kama ikitokea ajali inakuwa watu waokufa ni *over crowd* ni kinyume na usajili wa meli yao idadi ya watu wanaoambiwa wachukue. Kuzichunguza meli zenye matatizo na hata abiria wenyewe naona wamefahamu. Kwa sababu kama meli imejaa kupita kiasi abiria wenyewe wanalalamika, waliwahi kufanya hata zoezi la kupiga simu polisi *captain* akakamatwa. Kwa hivyo hili naona limefanikiwa vizuri na tutaenda nalo vizuri. Tutazoea tu mwanzo unakuwa mgumu.

Mawasiliano ya simu pia tunashukuru kwa kuleta hili la kusajiliwa hizi simu za mkononi. Kwa kweli simu za mkononi zilikuwa hazina amani wala *dressing*. Wakati wote unakuwa una hofu ya simu yako kwa utashi tu anaweza akachukua laini akakutukana akisha akaitupa. Lakini siku hizi limekuwa hili zoezi limepungua kwa asilimia kikubwa. Tunakwenda vizuri na amani na simu zetu za mikononi. Kwa hiyo pia napongeza kwa hili.

Uwanja wa Ndege kwa kweli tumeshapata zile *running way* za uwanja wa ndege. Ninatamaa kubwa sana tunayokaribu tu kumaliza kwa jengo letu la abiria lakini nakushauri Mhe. Waziri. Kwanza tupate wadhamini wazuri wa d*uty free International Air Port* zote zinakuwa na wadhamini wa *duty free* wazuri wanaendesha d*uty free* vizuri. Kwa hiyo wateja wanakuwa wanafurahi na d*uty free* ya pale kutokana na huduma zake. Halafu kutoa huduma nzuri za *parking* za ndege ziboreshwe zijekuwa nzuri ili tupate ndege nyingi zinazolenga kufanya *parking* tutaingiza mapato kwa kiasi kikubwa.

Kuongeza huduma ya utiaji wa mafuta. Kwa vile zitakuwepo ndege nyingi pale ile huduma ya mafuta naona kama itakuwa kidogo, inabidi kutoongeze tenki zile ili huduma zetu ziwe zinaupana zaidi.

Jengine ni lazima tuwe na hoteli *transit* yenye hadhi ya kisasa. Kuna siku nyengine *emergence* hatuombezei lakini kuna mashirika mengine mara yanagoma abiria tutakuwa hatuna pa kuwaweka. Lakini kama shirika lina hoteli yake ni *transit* wanachukuliwa wanawekwa mpaka baada ya muda wanaendelea na safari yao bila ya kupata usumbufu.

Mwisho kwa niaba ya wananchi wa Magogoni naiyunga mkono hotuba hii mia kwa mia. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii asubuhi hii ya leo. Pia napenda nimshukuru Allah (SW) aliyeweza kunisimamisha katika kikao kikubwa kama hichi kwa wakati huu kwa kweli namshukuru.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda nianze kwa kutoa pongezi zangu nyingi sana kwa Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi, Katibu Mkuu wake pamoja na watendaji wengine wote wa Wizara ya Mawasiliano, lakini kwa sababu niko Pemba pia napenda nitoe pongezi za pekee za Afisa Mdhamini wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa kweli anafanya kazi nzuri, anafuatilia wakati mwengi Mhe. Waziri anakuwa hayupo lakini yeye hatulii wakati wote anakuwa yuko barabarani.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya kazi kubwa ya kuimarisha sekta hii ya barabara na wagonjwa wanaona, wafanyabiashara wanaona, wakulima wanaona kutokana na shughuli zao na namna walivyopata ufumbuzi wa kushughulika katika kupita kwenye sehemu za barabara wanazotoka, kama ni kukimbilia hospitali, kama ni kwenda kufanyabiashara, kama ni mkulima anapeleka mazao yake shambani. Mhe. Mwenyekiti, serikali

imejitahidi sana mwenye macho haambiwi tazama, sote tunaona hali ilivyokuwa na sasa ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba Mhe. Rais sijui ana macho ya kiasi gani ya kumuona huyu Mhe. Waziri akajua kwamba Mhe. Waziri aliyekuwepo hali yake sio nzuri akamteua yeye Mhe. Machano kwa kweli anaifanya kazi hii vizuri sana. Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwamba tumshukuru Mhe. Rais tena tumshukuru sana kwa kazi kubwa aliyompa Mhe. Waziri na anawaambiwa hawa waliomchagua Mhe. Waziri wamchague tena, tena kwa kura nyingi ili aendeleze hizi kazi za barabara kwani bado hatujamaliza. Mhe. Mwenyekiti, Pemba tulikuwa na kilio kikubwa lakini sasa hivi tunamshukuru Mwenyezi Mungu tumefikia pazuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikianza na mchango wangu nasema kwamba barabara zimejengwa, nzuri, zimeimarishwa vizuri lakini nina ushauri kwamba tunapojenga barabara lazima tuweke *reserve* kwenye barabara kwa sababu dunia inakuwa, sisi tunaondoka, mambo yanabadilika, Mhe. Mwenyekiti, wakati wowote ikitokezea barabara inataka kuongezwa basi isiwe kuna tatizo na hasara kwa serikali kwa kuwaondoa wananchi isipokuwa ile reserve ndio itakayosaidia kuongezea barabara. Hilo naomba tulishughulikie sana.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuhusu barabara nitakuwa si mwingi wa fadhila kama sikuishukuru serikali kwa barabara ya Mkoani-Makombeni. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli barabara ile naifananiza na barabara sijui ya Morogoro-Dodoma kwa namna ilivyonyooka, ilivyopendeza na kwa namna inavyovutia. Lakini jambo kubwa jengine ninalotaka kulisema ni kwamba kuna haja ya kuona tunapotengeneza barabara milima yetu tuikate kwa utaratibu kwa sababu tunajua tuko kisiwani na milima ndio inayotusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, siku moja nilikuwa nimefuatana na jamaa kutoka Tanzania Bara wakasema mbona nyinyi huku mkitengeneza barabara mnakata kata hii milima, musiikate sana hii kwa sababu ndio inayokusaidieni. Kwa hivyo, na mimi nikahisi kwamba kwa kweli tulivyokuwa tunatengeneza barabara ya Mkoani-Chake Chake sijui kuna kampuni ilizunguka mabondeni lakini hata walipoifungua barabara milima yetu imenusurika na sasa barabara ipo inafanya kazi yake vizuri. Kwa hivyo, ushauri huo natoa kuhusu barabara kwamba tusipendelee kuikata sana milima. .

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ninalotaka kulisema ni kuhusu Pemba sasa hivi imeimarika vizuri. Mhe. Mwenyekiti, hapa mimi nina choyo kidogo lakini sio kibaya, lakini naona hapa katika barabara za Unguja kuna hizi *round about* ambazo zinajengwa vizuri sana na zinavutia. Mhe. Mwenyekiti, kwa nini sisi kule Pemba na sisi angalau tusipate *round about* japo mbili. Mhe. Mwenyekiti,

moja iwe Machomane kwa sababu mji mkubwa wa Pemba *center* yake hasa ni Chake Chake, Machomane kuna barabara zinazotoka Vitongoji, inayotoka Wete na inayotoka Chake Chake pale zinaunganishwa pamoja. Mhe. Mwenyekiti, nahisi kwamba sehemu hiyo ingevutia zaidi na haiba ingepatikana zaidi ya mji wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikija kati kati ya mji hapa Benki kuna barabara inayotokea Wesha, Mkoani, Machomane zote zimekusanyika pale barabara nne. Mhe. Mwenyekiti, nahisi katika mawazo yangu kwamba tukipata *round about* moja pale ya kisasa na nzuri basi mji wetu utazidi kuimarika na utapendeza. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kupitia kwako namuomba Mhe. Waziri jambo hili alitilie maanani alishughulikie. Mhe. Mwenyekiti, siku hizi Chake Chake kuna majumba ya ghorofa yamejengwa yatazidi kuvutia na yatazidi kupendeza.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nataka niende kwenye usafiri wa baharini. Mimi napenda sana kusafiri kupitia njia ya bahari, wengine wananiambia anaogopa ndege, sikuogopa ndege jamani. Mhe. Mwenyekiti, ikilazimika kupanda ndege huwa napanda ndege, nilipanda ndege nikenda Harare, nilipanda ndege nikenda Ghana, nilipanda ndege nikenda China. Mhe. Mwenyekiti, lakini nikiwa natoka Pemba kuja Unguja pale huwa nafuatana na ndugu zangu na jamaa zangu ambao wengi siku nyingi hatujaonana kwa hivyo napata nafasi ya kuamkiana nao, kuzungumza nao tukiwa kwenye chombo na mambo mengine mengi. Kwa hivyo, napendelea sana kusafiri kupitia baharini kutoka Pemba kuja Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu mimi nahisi kwamba wakati mwengine wenye vyombo wanakuwa wana tamaa kubwa na inabidi wapakie watu kiasi ya kile chombo. Mhe. Mwenyekiti, jambo hilo ni hatari kubwa ikitokezea tatizo lolote inakuwa ni hatari kubwa kuhusu uokoaji wa watu. Mhe. Mwenyekiti, ni afadhali kuwe na chombo maalum kiangalie chombo fulani kitachukua abiria wangapi na kweli kiwe kinachukua kama inavyotakiwa. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu siku moja kilikuja chombo kule Mkoani na mimi nilikuwepo, foleni ilikuwa refu sana nikasema jamani mbona watu wengi.

Mhe. Mwenyekiti, yule mwenyewe hasa anayeendesha meli akasema juzi nilipata tatizo Dar es Salaam sasa na leo mnataka kuniletea matatizo mbona abiria wamekuwa wengi mno. Mhe. Mwenyekiti, abiria wanakuwa wengi kama wanauziwa tiketi nyingi kuliko kiasi. Kwa hivyo, naomba jambo hili tulishughulikie sana kabisa. Mimi pamoja na kuwa napenda kusafiri baharini lakini nikiiacha Pemba nikiingia Nungwi basi nakuwa nakata tamaa nasema hee kuogelea najua, mbona mkondo mkubwa huu. Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo tukiwa wengi ikitokezea tatizo lolote itakuwa ni hatari.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ninalotaka kulizungumza jana hapa Mhe. Omar Ali Jadi alisema gati yetu ya Mkoani tuitobowe ili maji yapate yaingie baharini. Mimi nikasema bwana sisi hatujui kuogelea, mwenzetu anajua kuogelea watu wa Kojani ni mafundi sana wa kuogelea lakini sisi hatuna uwezo wa kuogelea leo maji yanaingia, yanatoka lakini yakiingia yanaingia kwa kasi ikiwa tumeshaitoboa ina maana maji tunayapa nguvu yaje juu, hiyo itakuwa ni hatari kwetu. Mhe. Mwenyekiti, pale Mkoani zamani kulikuwa na mabenchi ya kukalia pale jioni mimi binafsi nilipokuwa kijana wakati huo nilikuwa nashuka nakwenda kwenye mabenchi nikikaa kitako nazungumza na wenzangu. Mhe. Mwenyekiti, mabenchi yale yote sasa hivi yameshachukuliwa na bahari havipo tena nina hakika Mhe. Waziri havijui kabisa.

Kwa hivyo, naomba tufanye utaratibu wa kuimarisha gati ile pia na kuangalia vipi tutakuwa salama ili bahari isiingie kwenye mabanda ya karafuu kwani sasa hivi inasogea kwa nguvu. Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi nilikuwa namsikia Mhe. Waziri akisema kama watashughulikia gati ya Mkoani, lakini ni kwamba bado siku haijafika. Mhe. Mwenyekiti, naomba kupitia kwako Mhe. Waziri awe makini katika jambo hili alishughulikie, wenzetu wa visiwa vyengine wamezama kwa kudharau mambo madogo madogo kama haya. Kwa hivyo, naomba na sisi tulishughulikie hili ili tujihami na mapema.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi nije kwenye usafiri wa anga. Mhe. Mwenyekiti, Uwanja wetu wa Karume hauna taa miaka sio kidogo, kuna wakati ndege zinatoka huko na pengine kuna mvua kubwa basi huwa hawaoni uwanjani na kwa sababu hakuna taa inakuwa dhiki hata kushuka. Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka Mhe. Shawana Bukheti Hassan mara moja alikuja na ndege pale nusu saa nzima haijatua kwa sababu hawaoni ni kiza. Kwa hivyo, suala hili la taa sio mimi tu niliyelizungumza na wenzangu wamelizungumza.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, suala la taa naomba litiliwe maanani sana pia na ule uwanja wenyewe kukaa na msitu kama vile nao haioneshi sura nzuri. Kwa hivyo, kama hatuna wakataji wa majani basi tuhangaike tuwapate lakini ilimradi kiwanja kionekani kina sura nzuri. Mhe. Mwenyekiti, jambo nililoliona ambalo wizara wanalishughulikia sasa hivi ni kuweka uzio tayari kazi hiyo imeshaanza kufanya. Kwa hivyo, na hili nalo naomba tulishughulikie.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja hii kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba ambao nategemea sana kuwa watanirudisha tena katika kikao hiki. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa hali na mali na namtakia kila la kheri Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi naye achaguliwe kwa kura nyingi ili tuendeleze kazi zetu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii na kwa kuwa nina tabia ya kuchangia kwa muda mfupi nadhani leo utanivumilia kidogo niongeze muda kwa sababu wizara hii ni muhimu na Mhe. Waziri ni mwenzangu sana.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwenye Idara ya Barabara na nitoe pongezi kwa jumla kwamba Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi katika suala la miundombinu Zanzibar lazima tuwape pongezi wamejitahidi. Pamoja na pongezi hizo lazima tuelekeze kwa yale mambo ambayo tunahisi yanaenda kidogo kinyume. Mhe. Mwenyekiti, nianze na barabara ya Mtambile-Kengeja-Mwambe barabara ambayo ina urefu wa kilomita 9.4 na ni miongoni mwa barabara sita za Kusini Pemba. Mhe. Mwenyekiti, kwa jumla hatua ya ujenzi wa barabara ile sio mbaya, lakini kumekuwa na changamoto ambazo ningependa nizizungumze Mhe. Waziri aziangalie.
Mhe. Mwenyekiti, changamoto ya mwanzo ambayo barabara hii ni ucheleweshwaji wa kazi. Mimi binafsi nilivyoichunguza barabara hii imechelewa na kuchukua muda mrefu kwa sababu zifuatazo. Sababu ya kwanza ni uchache wa vifaa, sababu ya pili ni usimamizi mbovu na sababu ya tatu ni tatizo la lami ambalo tumeliona.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la ucheleweshwaji wa vifaa hili ni tatizo la wizara ambalo bila shaka Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba linakuwepo, jambo la kusikitisha ni tatizo zima la usimamizi mbovu. Mhe. Mwenyekiti, nilifanya ziara kule Mwambe nikauliza kwa nini hamjaanza kazi ya kuweka lami, wakaniambia sisi kama wasimamizi wa serikali tunasubiri kokoto. Tumekuwa hatuna kokoto kwa sababu Meneja wa mradi ule amekuwa hatoi mafuta kwa sababu ya kuchukua kokote Vitongoji. Mhe. Mwenyekiti, kama hii sababu ni ya ukweli kwamba tatizo ni mafuta ambayo hayapatikani basi huu ni usimamizi mbovu na ndio uliochangia kucheleweshe barabara ile na kuchangia kucheleweshe barabara nyengine zilizofuatia.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo jengine ambalo pale nimeliona ni tatizo la lami. Mhe. Mwenyekiti, pale ililetwa lami ya mwanzo, lami ile ilisemekana sio lami iliyoagizishiwa. Kwa hivyo, katika hili ningemuomba Mhe. Waziri aniambie lami ile nani aliyepewa jukumu la kwenda kutafuta lami na kwa nini lami ile ya mwanzo ilikuwa sio lami iliyokubalika na serikali kwa ajili ya mradi ule.

Mhe. Mwenyekiti, suala la tatu ambalo ni changamoto kwa mradi ule ni kiwango cha barabara wenyewe. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kilomita 1.3 ile ya mwanzo basi utaona kwamba kile kiwango cha barabara ile ni madhubutu lakini kila ukisogea mbele kumekuwa na uripuaji wa dhahiri kwa ajili ya kufuata muda na bila shaka kunakuwa na mkono mkono unaofanywa na watendaji ambao sio waaminifu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba kilomita moja ile ya mwanzo ya barabara basi barabara ile ni nzuri na kwa kweli ilichukua muda mrefu bila ya kuharibika. Lakini leo nenda pale Kengeja ambapo tumejenga pale Kengeja Majenzi ni kwamba nondo zote ziko nje, zege imekatika nondo ziko nje hadi naondoka Pemba. Hii ni dhahiri kwamba kiwango cha barabara sehemu ya mwanzo ni madhubuti lakini kila tukenda mbele kwa sababu watu wanafuatia muda waende Kangani basi kumekuwa na uripuaji mkubwa. Kwa hivyo, hizi ni changamoto ambazo lazima tungezizungumza ili miradi mengine inayoendelea mbele ya Kangani na Wambaa basi tukaona kwamba ni dosari ambazo zimetokezea kule eneo la Mwambe.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo jengine ambalo ningelizungumza ni tatizo la athari kwa wananchi vipando na nyumba. Hivi vipando najua Mhe. Waziri ataniambia kwamba ni Wizara ya Kilimo nataka niliwache, lakini tatizo la nyumba nne za Mwambe ambazo zimeingia maji kwa sababu ya kukata mlima ni tatizo la Idara ya Ujenzi wa Barabara. Hapa Mhe. Mwenyekiti, nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba wakati nyumba hizi nne zimeathirika Mwambe mimi kama mwakilishi ningelichukua hatua ya mpigia simu Afisa Mdhamini kwamba aje Mwambe aangalie nyumba nne zilizoingia maji na zimeanguka. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ni nyumba za watu wanyonge, mlima ule umekatwa umekusanywa kwenye sehemu ya maji kwa hiyo maji yametuama nyumba zinaathirika, Afisa Mdhamini akaniambia mimi nina safari ya Kenya. Mhe. Mwenyekiti, afisi hiyo ina watu wengi nikamuomba basi kama wewe una safari ya Kenya basi nilitee wafanyakazi wako waje waone kwamba nyumba zimeanguka. Mhe. Mwenyekiti, nilitaka waje waone mbele yangu ili kila mmoja tukubaliane kwamba nyumba zimeathirika, lakini hadi naondoka sikupata jibu lolote.

Mhe. Mwenyekiti, nilipoona juhudi zile za Pemba zimenishinda nilikumuandikia barua Mhe. Waziri nikakuletea hapa uje Pemba uone kwamba nyumba zilivyoathirika. Najua Mhe. Mwenyekiti, wakati ule ilikuwa mchakato wa kura bado muda alikuwa kidogo anao wa kuruka Mwambe lakini kwa bahati mbaya umeshindwa kuja kuziona nyumba hizo. Mhe. Mwenyekiti, mimi mtaji wangu ni wananchi najiuliza hivi kwa nini niunge mkono hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, suala la nyumba nne Mwambe zilizoanguka kwa sababu ya maji yaliyotuama chanzo ni ujenzi wa barabara hatukuwafanyia haki watu wa Mwambe niliwaomba mje mzione angalau mtafute lugha ya kisiasa tuwape wale watu, mimi mwenzetu huo ndio mtaji wangu. Kwa hivyo, wameniambia na niwaombe kambi ya upinzani peke yangu ndio nikatae bajeti hii, ili nitoe sauti kwamba nimetetea na waandishi watakwenda kusema kwamba Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani peke yake ndiye aliyekataa. Kwa nini? Kwa

sababu nyumba nne zimeathirika kwa maji afisi ya Pemba imekataa na Mhe. Waziri amedharurika, hilo ni tatizo.

Kwa hivyo, mimi ningemuomba Mhe. Abubakar Khamis Bakari na kambi nzima leo waniachie peke yangu nikatae ili waandishi wa habari waseme kwamba mwakilishi amekataa kwa hoja hii. Mimi nampenda sana Mhe. Waziri wizara hii inajitahidi ni wizara inayoongoza hapa Zanzibar lakini hii waliofanya wao ni dharau.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye barabara ya Kiwani. Mhe. Mwenyekiti, barabara ya Kiwani tangu niingie katika Baraza hili la Wawakilishi bajeti ya mwanzo niliyoshuhudia ilitengwa milioni mia tatu, bajeti ya pili barabara ile ikapata bahati ya kutengenezwa kwa milioni 27 kwa teknolojia ya Romex kwangu mimi nina ahadi hii leo naiweka *super glue*. Mhe. Mwenyekiti, na bajeti ya mwaka jana barabara ile imetengewa milioni mia sita, hadi mwezi Machi zimetolewa milioni mia nne na hamsini na tatu sawa sawa na asilimia 76.

Mhe. Mwenyekiti, kazi iliyofanywa barabara ya Kiwani kwa jumla milioni mia sita na ishirini na saba kwa miaka mitano haionekani, mimi sio mtaalamu hata kidogo wa barabara lakini kwa kiwango cha kifusi barabara ile ingemalizika kwa miaka mitano. Nimekuwa nikisema mara nyingi kwamba ningeshauri watu wa Kiwani waombe ile barabara kama lami bado basi iwekwe kifusi. Kwa hivyo, bajeti tatu tumetumia karibu milioni mia tisa lakini hali ya barabara ile ni mbaya na la kusikitisha kabisa kule kwenye barabara magari yamekwama niliomba Pemba njooni mtuletee magari, wakaniambia kusanya watu kesho tutakuletea kifusi waje wachawanye wenyewe, hadi hii leo sikuwaona. Mhe. Mwenyekiti, hiyo ni dharau kwa nini niunge mkono bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anipe matumizi ya milioni mia sita ambapo hadi leo tumetumia asilimia 76 kwa kukata ile milima, ikiwa kwa kuikamata milima ndio pesa hizi basi sijui milioni ngapi ile barabara itamalizika. Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeomba na hizi milioni mia tatu safari hii mmetenga Mhe. Waziri musiitie kwa sababu hizi mtazitia mtakata mlima mmoja itakuwa milioni mia moja ni kazi ya kukata mlima tu, hivyo mlima huo ni wa kiasi gani. Kwa hivyo, mimi Mhe. Waziri nakuomba kabisa hizi pesa usizitie kwa sababu zitapotea kwa kukata mlima.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nataka nilisema ni suala zima la uharibifu wa mazingira na nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba tutofautishe baina ya kesi ya Ali Hamad aliyedai ardhi yake na kesi ya kimazingira. Mimi nafahamu Mahakama imeamua Ali Hamad hana haki wala

sizungumzi, Ali Hamad mlikwenda Mahakamani mkashinda yamekwisha, nazungumza kesi ya mazingira Mwembe tunaathirika.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 58 zipo barabara hapa ambazo zimejengwa Kusini Pemba hasa Wilaya ya Mkoani, nambie fusi limetoka wapi? Fusi lile lote limetoka Mwambe mwaka 1999 tulijengewa gati Mkoani *COGEFAR* walikuwa wanatumia baruti Mwambe ina visima vitatu vya maji kwa ajili ya *COGEFAR*, hivi leo imefika zaidi ya mita saba kwenda chini maji yanatoka ya bahari. Mhe. Mwenyekiti, bado wananiambia suala la Ali Hamadi na ardhi, sio suala hilo ni suala la mazingira. Mhe. Mwenyekiti, mimi najiuliza kwa nini niunge mkono bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, naendelea kuiomba kambi yangu ya upinzani kwamba leo mniachie nikatae peke yangu wala sio aibu lengo ni kwa sababu natoa sauti kwamba watu wa Mwambe wanaathirika bahari ikipanda juu je, nyinyi mnakaa mjini watu hawa watakufa mwanzo. Kwa hivyo, ni bora tuzame lakini sauti yangu isikike kwamba nimekataa, haiwezekani Mhe. Mwenyekiti, namuandikia barua Mhe. Waziri njoo ulione tatizo la Mwambe.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo la Mwambe ni mazingira na Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi wametembea Unguja na Pemba wamekiri kwamba Mwambe tatizo ni baya mtu anakwambia sababu ni bwana Ali Hamad, Ali Hamad ana kesi ya ardhi wala haimuhusu mimi nazungumza kesi ya mazingira Mwambe inavyoathirika. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakuomba kwamba ujitayarishe watu wa Mwambe wanaendelea kuzama tena kwa makusudi. Mhe. Mwenyekiti, mashimo waliyoyachimba *COGEFAR* mpaka leo hayajafukiwa, barabara hizi sita ambazo zinajengwa na *NORAD* zote zinategemea kifusi cha Mwambe, je, ingelikuwa maeneo yenu nyinyi mngekubali?

Mhe. Mwenyekiti, ingelikuwa eneo lako hili ungekubali kufika hatua kama hiyo. Mimi nasema kwamba kama kweli ni kufanyiana haki basi watu wa Mwambe wako tayari wanadhirika na serikali kwa kutumia rasilimali ile kwa ajili ya ujenzi wa barabara lakini basi mashimo yawe yanafukiwa. Kama kuna fidia ni fidia gani kampuni hizo zilizotoa. Kwa hivyo, leo mbuyu unaning'inia mita saba kutoka mzizi wa mbuyu mpaka chini. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba watu wa Mwambe wanasema mnawaonea kwa mazingira mabaya na hili halikubaliki. Nyinyi kaeni ofisini muandae miradi lakini msubiri siku moja watu wa Mwambe wazame.

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba sekta ya mawasiliano ya simu mnara wa Mtambile nimesema sana kwamba ule mnara wa Tigo mawasiliano pale hayapatikani lakini tatizo jengine ambalo limezunguka ni mmongonyoko wa

ardhi wa ule mlima kwa hiyo nao mkiuachia basi msubiri ajali nyengine pale Mtambile itokezee.

Mhe. Mwenyekiti, nasema kuwa, bila ya kupata majibu ya kuridhisha tena ya kwenda uso kwa uso na uongozi wa wizara kuona, basi siungi mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii ya asubuhi kutoa mchango mdogo kuhusiana na bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru *Allah* kwa kutujaalia uzima na kutupa afaya tukaweza kuzungumza.

Mhe. Mwenyekiti, kiukweli kumetokezea mabadiliko katika Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Sisi au mimi binafsi napongeza mabadiliko hayo yaliyotokea. Tulipokuja hapa mwaka 2006 ambao ndio uliokuwa mwaka hasa wa mijadala, picha ilikuwa ni tofauti na ilivyo sasa. Mimi nazungumzia ile *point* ambayo niliitoa katika bajeti kuu ya serikali, kwamba moja katika jambo muhimu sana katika bajeti za serikali ikiwa ni kuu au ya kiwizara, ni kuwa uiyano wa kimaendeleo kati ya Unguja na Pemba na kati ya Mkoa au wilaya na wilaya . Hili ni jambo sana kabisa.

Kwa sababu wataalamu wetu pamoja na waheshimiwa wanasiasa wanaweza kuwa na *interest* zao katika maeneo yao na pengine wakaingiza katika utekelezaji wa shughuli za kiserikali. Lakini kutakapokuja ule uiyano wa kimaendeleo kwanza kutazuia wimbi la uhamaji kutoka sehemu moja kwenda nyengine. Pili kutakuwa na ridhaa ya wale wananchi na kuwa na ushirikiano wa kutosha na ile serikali ambayo ipo madarakani. Kwa hivyo, kwa sababu vilio vya wengi vilisikikana, hatuna budi kuipongeza wizara kwa kuona kwamba kumepatikana mabadiliko ya mwelekeo wa uiyano kati ya sehemu na sehemu, hususan katika ujenzi wa barabara.

Lakini mimi nina mchango mdogo katika hii Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara. Kwa sababu kuna kazi mbili ambazo hata hiyo idara yenyewe ilivyoitaja imeainisha kazi hizo. Haiwezekani kazi mbili kufanywa na *management* moja au *super management* moja, lazima kuwe na *section* mbili, bila ya hivyo barabara zitajengwa lakini hazitengenezwi wala hazitunzwi. Hii nimeona kwamba, kwa sababu *management* ni moja hakuna *special section* ambayo hii hata kukawa na kitu gani wao kazi yao kwenda kutizama *patch* iko wapi basi.

Kwa mfano, njia za Pemba sasa hivi tunashukuru kwamba tumepata ufadhili, lakini njia tatu zile zinajengwa kwa ushirikiano baina ya *NORAD* na sisi wenyewe. Sasa utaona kwa sababu kuna *foreign component* kule na kwa sababu kuna *time factor* inayonipelekea ile, mkazo umewekwa kule zaidi kuliko sehemu nyengine. Hii ni kwa sababu hakuna *section* nyengine *section* ndio ile ile, kwenye *main road* inayokwenda Wete.

Mhe. Waziri Nchi (AR) Kazi Maalum alitaja hapa ni Machomane ambapo lipendekeza pawe na *round about*, kama mita 20 mpaka 30 kutoka hapo anapopendekeza kuwe na *round about* kuna *dispensary.* Sasa hapa panakuwa sio pahali tena pa kuja kufanya matibabu ni pahali pa watu kuja kutafuta ajali zao. Kwa sababu tu njia imekatika katika, pana sehemu maji yanakaa. Kwa hivyo, magari yanapembua ikipembua inakula kwenye *dispensary*.

Hivi karibuni alichukuliwa msaidizi mmoja akakatwa miguu na pikipiki kwa sababu alikuwa akikimbia yale maji yaliyotuama. Sasa tukitizama sisi na yale mashimo yanayokuwemo njiani utaona tatizo kubwa ni kwamba Mhe. Waziri hajatenga *section* ya kuangalia utunzaji wa zile barabara ambazo zishajengwa.
Kwa hivyo, mimi napendekeza kama *section* hiyo haipo, kwa sababu sijenda *detail* siko katika Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, kama haiko *section* hiyo basi mimi naomba kungekuwa na *section* maalum na wao wasipewe kazi yoyote. Nakuhakikishia Mhe. Mwenyekiti, wakipewa gari moja tu ya lami kwa kila wiki, basi njia zote zitapitika bila ya matatizo, zile zilizokwishatiwa lami. Lakini ikiwa kazi watapangiwa yoyote tu, haya matengenezi yatakuwa ni magumu. Hilo moja.

Mhe. Mwenyekiti, la pili *feeder roads*. Mara hii kidogo nimeona kuna mapungufu katika bajeti hii. Kwa sababu tumetajiwa zile barabara ambazo ni zile ambazo zishapata ufadhili au zinashughulikiwa, lakini kuna *feeder roads* nyengine zinataka fusi tu na tunalo. Kwa hiyo, tungelizitaja.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano katika jimbo langu nimepiga kelele sana. kuna barabara moja nishaanza kupata kidogo, lakini kuna ile barabara yenye kilomita zaidi ya kumi ambapo hivi karibuni ulipokewa *wire* wa umeme kutoka Tanga, hiyo iko hali mbaya sana. barabara ya Wesha – Ndagoni au wengine wanaita Mkumbuu, iko hali mbaya sana. kwa sababu ni eneo lenye milima sehemu nyengine na mabonde lakini pia utengenezaji wa shughuli za umeme kwa sababu walipeleka matrekta makubwa na zana nyingi, ikabidi yatokee mashimo kwa kuchimbuka.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aipe *special consideration* kwa sababu ni Wizara ile ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi ndio iliyotibua zaidi ile barabara.

Lakini kuna na kitu muhimu sana cha kitaifa, likitokea tatizo kunatakiwa lazima wende na *four wheel.*

Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa tu, siku moja nilikuweko mimi zikaja gari mbili hizo za umeme, basi moja ilipiga msererekо ikarudi kule kule ilikotoka kwa ile njia ilivyo mbaya, lakini wao wanapita hivyo hivyo tu hakuna anayetia fusi wala nini, hata wewe Mhe. Waziri njia yako? Tunaendelea mbele.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakuja kwenye Mamlaka ya Uwanja wa Ndege, kama hii mamlaka ni moja baina ya Unguja na Pemba basi nafikiri si haki kwamba kaka unamnunulia suruali ndugu hata shuka usimpe. Mwaka jana nafikiri Mhe. Waziri alifikiria nafanya masihara kuwa mimi nitanunua ndege. Mimi nilisema vile kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, haifikii wakati, Allahu Yaalam, haifikii wakati kwamba mimi nitanunua ndege, ndio maana nikasema hiyo siku itakayotiwa taa uwanja ule ndio mwaka huo nitakaonunua ndege mimi. Kwa sababu haifikii na bajeti hii inasema hivyo hiyvo, tutatia taa lakini hazitiwi, lakini ile gharama kwa viongozi ni kubwa zaidi na kwa wananchi.

Karibuni hivi alikufa kijana mmoja akaja akamalizikia hapa Uwanja wa Ndege wa Unguja. Kwa tabu na mashaka wakakodi tenza ndege siku ya pili ndio akaletwa kwa sababu ya mvua tu. Kwa hivyo, ikinyesha mvua na Alhamdullilah Pemba mara hii kama wengi mnavyoijua imepata mvua nyingi sana kuliko kawaida. Kwa hivyo, kungelikuwa na taa ndege nyingi zingetua, sijui kama hampati malalamiko kutokana na hayo mashirika ya ndege, kwa sababu na wao ni wadau.

Lakini katika hilo la uwanja wa ndege mimi ningelifikiria kwamba mambo ya wale Zimamoto ile mamlaka ikawa inahodhi nao wawaondoe katika kikosi kile. Juzi hapa tulipokuwa tukizungumza bajeti niliuliza Kikosi cha Zimamoto na majukumu yake yanapewa bajeti chini ya Kikosi cha Valantia. Basi kwa usalama wa ndege za kimataifa mamlaka ya uwanja wa ndege kikosi chake za Zimamoto kiwe nacho wenyewe kisiingize kule, kwa sababu kule hawako *serious.* Watu hawajui chochote wale, mimi nakuhakikishia hasa hawajui chochote.

Angalia mtoto yule, nilisema hapa sitaki kurudia tena, waliku na dude la kuzimia moto, ee basi mtoto kazama anakuja na dude la kuzimia moto! Kawaulizeni kama mimi nasema uongo na mimi nilikuweko. Tafuteni watu muwaweke Mamlaka ya Uwanja wa Ndege wanaojua kazi, tunataka kupokea ndege za kimataifa inasemwa hapa hapa sasa hivi, tusije tukafanya makosa tena mara ya pili ndege zikija zikiondoka tena hazirudi hizo. Ziko ndege ziliondoka mkafichaficha hapa lakini wanasema ziliondoka kwa sababu ya matatizo hayo.

Sasa tuwakampeni lakini tujijenge kikweli wakirudi wajue kwamba tuko *serious*, lakini tukija tukiwachezeachezea kidege kinawaka moto wanakwenda pale mtu anapangusa pangusa hajui wala anafanya nini. Mimi naomba Mamlaka ya Uwanja wa Ndege wawa-*train* watu wao wenyewe wa zimamoto, kikosi kiwe na mamlaka yao wasikipeleke kule.

Tuje kwenye bandari sasa hivi kidogo. Bila shaka mimi nitazungumzia kwa yale ninayoyajua. Kwanza naomba kupongeza ile juhudi ya kujenga *jetty* pale tukatenganisha baina ya bandari kuu na shughuli za kiabiria. Imesaida sana na ni sehemu ambayo lazima itizamwe, ili isije ikafeli siku moja kutakuja kuwa na matatizo sana.

Angalia mrundiko wa makontena uliopo kule na ingekuwa abiria wote sasa wanamezwa kule ingekuwa hatari zaidi. Kwa hivyo sehemu ile na kama kuna *improvement* yoyote, kama kuna *study* zozote za kuona kuna nini, basi lazima ile iendelezwe. Kwa sababu inaonesha hasa kwamba kitu kinachohitajika kubagua baina ya bandari inayotupiwa mizigo na bandari ndogo inayochukua abiria wa kawaida. Kwa hivyo, hata hizo Serengeti vyombo vilivyoko sasa hivi vinavyopakia kule kama MV. Maendeleo na vyenginevyo, bado kuna haja ya kutafutiwa mahali ambako ni nje ya ile bandari inayopakia mizigo.

Halafu mimi namuuliza Mhe. Waziri tokea siku zilizotokezea ajali zile za kuzama na nyenginezo, kumetokea mabadiliko gani katika wizara ya Kikosi cha Uokozi. Kuna hatua zozote zilizochukuliwa kutayarisha hiki kikosi cha uokozi, *dives* wangapi wamefundishwa, *equipment* kiasi gani zimeagizwa baada ya somo lile, mambo gani yaliyobadilika katika bandari kuona kwamba sasa likitokea jambo kama lile linashughulikiwa kwa muda mfupi zaidi kuliko lilivyoshughulikiwa.

Namalizia Mhe. Mwenyekiti, kusema kwamba si vibaya kurudia kwa sababu linatuhusu sote, Gati ya Mkoani. Siku moja mwaka 2006 au 2007 nilisema kama tunaingoja i-*settle* basi tuweke ki-*pump* pale cha kutoa yale maji. Sasa imezidi zaidi miaka mingapi iliyopita.

Juzi mimi nilikwenda kule Mkoani, sasa tatizo lililopo ni moja kwamba kuna watu wanaweza sasa wakazama. Kwa sababu mvua nasema ni nyingi na inaponyesha mvua ile sehemu ya kati kati yote inakuwa na maji sasa inayobaki ni ncha ya huku na huku, na gari zinapoingia zina-*park* huku kulikokuwa hakuna maji, kule kwenye maji wanakuacha. Sasa mtu anapopita anaona bora apite huku atambaetambae, sasa akija mchukuzi akimpiga push na yuko ncha ncha. Kwa hivyo, tunaomba sana kabla ya uchaguzi huu wa mwaka 2010 bandari iwe ishatengenezwa au tutabandika mabango pale kwamba CCM imeshindwa. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohammed Ali Salim: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, sitazungumza sana *Inshaallah*. Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mola wetu sote kwa kutuwezesha kufanya kazi hii saa hizi. Na pia kumsalia Bwana Mtume (*S.A.W*) na yeye kwa muongozo alioletewa na Mwenyezi Mungu tukaweza kuishi katika maisha haya yaliyo na ustaarabu mwingi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naomba sasa niingie katika suala zima la bajeti hii ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Kwa kuanzia Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze na suala zima la barabara ambalo lipo katika ukurasa wa 14 na 15.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani serikali wakati mwengine huona humu ndani ya Baraza watu waliomo ni wa kudanganywa tu basi, wadanganywe watu waendelee na yao. Nasema hili Mhe. Mwenyekiti, nikiwa na sababu nzito.

Katika mradi wa barabara za vijijini Kusini Pemba, mwaka jana kipindi kama hiki ndani ya Baraza hili tuliuzungumza. Tuliuzungumza kwa kina na tukahoji mambo ya msingi na tukapewa majibu kwa wakati ule yalionekana yalikuwa majibu mazuri. Tulisema hizi barabara sita ni nyingi zote kupewa Idara ya Ujenzi wa Barabara kuzijenga. Kwa sababu kama itapewa idara hii barabara hizi zitacheleweshwa, kwa sababu idara hii haijengi barabara hizi za mradi tu, ina barabara za mradi, barabara za Mfuko wa Barabara, ina utiaji wa viraka, ina barabara za kifusi, ni idara hii hii moja inayofanya kazi zote hizo. Tukasema kupewa hawa mradi huu barabara hizi zitacheleweshwa.

Pia tukasema mbona Unguja wanaletwa makandarasi kutoka sehemu mbali mbali wakaja wakajenga barabara sisi wapewe zote hizi hawa mawasiliano wazijenge wao. Lakini kumbe lile lile tulilolisema ndio lile lile linalofanywa.

Tuliposema hivyo jibu tulilopewa Mhe. Mwenyekiti, tuliambiwa barabara kwanza zitaanza tatu kwa umoja tukatajiwa na majina, itaanza ya Mtambile – Mwambe, Mtambile – Kangani na Mzingani – Wambaa. Hizo zitaanza kwa umoja. Nataasaf kusema kuwa Mhe. Waziri alitudanganya, alilidanganya Baraza hili. Kwa sababu mpaka hivi sasa muda wote uliokwishapita hivi sasa hazijaanza kwa pamoja barabara tatu, ilianzwa moja ya Mwambe mpaka leo haijesha, ikaanzwa nyengine ya Mtambile mpaka leo ndio tunaambiwa hapa kuwa, kwa upande wa barabara ya Mtambile – Kangani kazi za usafishaji zimekamilika, ina maana barabara ile kumekamilishwa usafishaji tu, hakuna jengine.

Sasa je, hivi hatukudanganywa? Hivi Baraza hili halikuambiwa vilivyokuwa si kweli kwa sababu kusema uongo si vizuri kutoka ndani ya mdogo wa mtu

mzima neno uongo. Lakini haionekani kama haikuwa kweli tulivyoambiwa? Lakini hilo lilikuwa moja tu Mhe. Mwenyekiti.

Jengine tulilodanganywa ndani ya Baraza hili katika kipindi kilichopita, tuliambiwa mradi huu serikali inalengo la kupata vifaa vipya, vitaagizwa vifaa mradi ulete vifaa ili utakapomalizika mradi vifaa vile viwe mali ya serikali. Ni wazo zuri sana lakini leo katika kitabu hiki Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 14 kifungu cha 28 tunaambiwa naomba ninukuu.

Kifungu cha 28 kinasema:

> "Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia mfumo wa nguvu kazi……"

Yaani hakuna vile vifaa sasa tunatumia nguvu kazi. Barabara zijengwe kwa nguvukazi. Hivi ni barabara zipi zinazojengwa kwa nguvukazi zaidi ya hizi, kuna nyengine? Hizo wanazojenga huku hivi zinajengwa kwa nguvukazi au zinajengwa kwa mashine?

Mhe. Mwenyekiti, huu umekuwa ni utoto, kuja Barazani hapa kila siku tukidanganywa leo unaambiwa hili, kesho unaambiwa lile, wakati wa utekelezaji inafanywa kinyume na vile tulivyoambiwa ndani ya Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, hali hii haitufikishi pahali ndani ya nchi hii, lazika tunaliambiwa ndani ya Baraza hili liwe ndio lile litakalofanywa. Saa hizi mimi nilikuwa natarajia barabara ya Mzingani – Wambaa tayari nayo inajengwa kwa sababu tuliambiwa zitajengwa tatu kwa pamoja. Nilimwambi Mhe. Waziri ende akaangalie barabara ilivyo. Nashukuru angalau kwa hilo kuwa alikwenda na akaiona barabara. Leo watu wa Wambaa kufika Mkoani au Chake Chake siku mbili kwa wiki, siku ya Jumatatu na Alhamisi, kwa sababu ndio siku pekee linalokwenda Tata na Tata ndio pekee linaloweza kufika Wambaa hivi sasa.

Kuna *Hiace* tatu Wambaa haziwezi kutoka kwa sababu barabara ni mbovu haipitiki. Wagonjwa, wazazi na watu wengine sasa hivi limekuwa ni tatizo kubwa, hizi *Ambulance* za Mbunge na Mwakilishi ndio gari pekee zinazokwenda kila siku mara tatu au nne kwa siku kwenda kuchukua wajawazito waliokuwa wanataka kujifungua, wagonjwa wanaoumwa sana na wale waliopata ajali. Hivi tunatarajia kwenda na mwendo huu mpaka lini Mhe. Mwenyekiti? Najua na leo nitaambiwa mengine, lakini nasikitika sana kuwa sitarajii kurudi ndani ya Baraza hili kwa sababu sikugombea tena, lakini *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atamleta mtu hapa pengine awe mara mbili kuliko mimi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa basi naomba, kwa sababu Mtambile – Kangani tumeambiwa usafishaji umemalizika, kazi ya usafishhaji sasa ianze Wambaa mara moja. Kule usafishaji ushamalizika ati, sasa hivyo vyombo vya kusafishia vinasubiri nini huko? Sasa hivi waanze kusafisha Mzingani – Wambaa. Kwa sababu tayari kule hakuna tena kazi za usafishaji zimeshakamilika.

Mhe. Mwenyekiti, labda nimuulize Mhe. Waziri kwa sababu barabara kenda kaiona, kwa sababu sasa hivi watu wa Wambaa wana shida kubwa hawawezi kufika nje ya Wambaa kutokana na barabara ilivyo, atawafanyia nini hivi sasa kabla hata hajaanza kuijenga hiyo barabara?

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe shukurani za dhati kabisa nilizotumwa na watu wa Makombeni kwa kujengewa barabara ya Bandarini – Makombeni. Wananchi wamefurahi, wananchi wanashukuru. Sasa hivi wana gari inayokwenda kila wakati ya abiria. Kwa hivyo, kwenda Makombeni na kurudi sasa hivi imekuwa ni jambo la kawaida halina tatizo tena. Sasa kama Makombeni imewezekana ambapo ni karibu zaidi na pale mjini je, huku Wambaa kulikokuwa mbali zaidi na mjini, na kulikokuwa kuna matatizo makubwa hivi sasa?

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri hili alitie katika mawazo yake na akilala asipate usingizi mpaka pale itakapoanza kujengwa barabara ya Wambaa. Lakini zaidi nataka nimjuilishe Mhe. Waziri kuwa katika Jimbo la Mkoani kuna barabara iliyotengenezwa na *TASAF* kidogo, inaitwa barabara ya Mbuguwani – Tironi.

Tironi kuna skuli, Tironi wakati wa uandikishaji kuna kituo cha uandikishaji na wakati wa uchaguzi kuna kituo cha uchaguzi. Katika uandikishaji mara hii iliyopita siku ya kwanza Tume ya Uchaguzi waliweza kufika Tironi kwenye skuli wakaweza kuandikisha, siku ya pili hawakuweza kufika kutokana na mvua. Barabara ilikuwa mbovu mno hawawezi kufika pamoja na gari zao zote nzuri, lakini hawakufika ikabidi wakae chini ya mlima. Wananchi waliojitolea wakaja wakachukua masanduku kwa kichwa wakayapeleka. Lakini siku ya tatu hata hapo chini ya mlima hawakufika tena ilibidi kituo kihamishwe kiwekwe Manyaga ambapo ni karibu sana na Mbuguwani.

Mhe. Mwenyekiti, leo sikukusudia kuzungumza sana, leo nilikusudia nizungumze barabara hii ya Mizingani/Wambaa lakini tu pia niseme ile Bandari ya Mkoani kwa kumalizia imeshafika huo wakati tunavyoambiwa Julai hii itaanza marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kujua tu ni kampuni gani iliyopata tenda ya kuirekebisha bandari ile ambayo itaanza Julai hii. Pili na mimi nijue nakwenda

Pemba Mkoani kuwa tayari kuna kampuni imeshapewa tenda ya kutengeneza bandari hii na Julai hii tukijaaliwa itaanza kutengenezwa.
Mhe. Mwenyekiti, ahsante naheshimu wakati wako.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi kunipa fursa hii kuchangia machache sana katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Kwa sababu ya muda mfupi sana mchango wangu utakuwa katika mfumo wa maswali.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niulize je, wale wananchi ambao walipakia mali zao katika meli ya MV Fatih iliyozama bandarini, nani hasa mwenye dhima ya kuwasaidia kuona kwamba wanalipwa haki zao. Kwa sababu mna vijana mle wafanyabiashara wadogo wadogo mali zao zilizama na mpaka sasa wanahangaika mtaji wao umepotea wala hawajapata msaada wowote. Ni Shirika la Bandari au Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa ujumla au ni nani wanaohusika na malipo yao.

Mhe. Mwenyekiti, la pili nimeshangaa hapa kuona taarifa kwamba katika ukurasa wa 37 kifungu cha 97 kwamba uingiaji wa meli katika bandari ya Zanzibar umepungua. Mimi nilikuwa natarajia kutokana na bandari kwamba imemalizika sasa hivi ni nzuri meli zitaongezeka. Kwa nini utafiti wenu unaonesha meli zitapungua kuingia katika bandari yetu ya Zanzibar.

Halafu jengine Mhe. Mwenyekiti, ni kuhusu uimarishaji wa Bandari ya Mkoani. Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka wakati wa Mhe. Adam Mwakanjuki Mwenyezi Mungu hajamjaalia kupata bahati mbaya ya ajali sikumbuki bajeti ya mwaka gani, lakini kama miaka mitano nyuma hivi. Katika hotuba ya bajeti tulielezwa hapa kwamba Bandari ya Mkoani itakuwa Bandari ya Kimataifa na itatangazwa rasmi na serikali kwamba ni Bandari ya Kimataifa na tukielezwa mipango mingi ya ku-*improve* ile bandari iwe ya kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, bahati nzuri siku moja nikaona wataalam wanaohusika na bandari Mkoani pale nikasikia wamo katika kuangalia kufanya *plan* ile bandari iboreshwe. Je, azma ya kuifanya ile bandari kuwa ya kimataifa imefikia wapi au serikali imeghairi imeona basi hakuna haja tena.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni kuhusu uwanachama wa *IMO*. Mhe. Mwenyekiti, wakati tulipokuwa tunajadili mswada unaohusu na mambo ya bahari tulielezwa kwamba Zanzibar itaombewa kuwa mwanachama mshiriki wa *IMO*. Je, juhudi za kuomba Zanzibar kuwa mwanachama mshiriki wa *IMO* zimefikia wapi. Kwa sababu mpaka leo asubuhi nilikuwa naangalia wanachama wa *IMO* Zanzibar haimo, pia nikaangalia katika wanachama washiriki *(associate members)* nikaona kuna Hong Kong - China, Maccao - China, Fero

Ireland – Denmark, wanachama washiriki watatu. Sasa Zanzibar juhudi zetu za kutaka tuwe wanachama washiriki wa *IMO* zimefikia wapi.

Halafu ikiwa hatujakuwa mwanachama mshiriki ndio tunabebwa na kaka zetu huko Jamhuri ya Muungano. Je, Zanzibar wanapokwenda inashirikishwa kiasi gani katika vikao vya *IMO*. Hilo nataka kujua kwa sababu nimeona kwamba tarehe 7 mpaka 11 mwezi huu kuna Kikao cha Baraza Kuu la *IMO*. Sasa kwa Zanzibar nani anayeshirikishwa kwa kupitia huu mwamvuli wa Jamhuri ya Muungano katika vikao hivyo.

Lakini tarehe 26 mpaka 30 mwezi huu huu kuna kikao cha kamati ndogo inayohusika na mambo ya usalama wa uongozi wa vyombo vya bahari. Je, kwa kupitia hawa ndugu zetu wa Jamhuri ya Muungano nani sisi Zanzibar hapa anashiriki katika kikao hicho. Tarehe 5 mpaka 9 mwezi huu vile vile kuna kikao kinachohusika na mambo ya bendera. Sasa ikiwa sisi sio mwanachama mshiriki. Je, nani kashirikishwa kwa kupitia huu mwamvuli wa wenzetu Jamhuri ya Muungano kushiriki katika vikao hivi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kusikia kilio chetu cha muda mrefu cha kutaka uwanja wa ndege uwe ni mamlaka inayojitegemea. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katika kitabu chake cha bajeti kaeleza azma hiyo kwamba viwanja vya ndege sasa vitakuwa ni mamlaka inayojitegemea, ni wazo zuri.

Lakini ushauri wangu Mhe. Mwenyekiti, kwamba hata baada ya kufanywa mamlaka basi usimamizi utahitajika. Kwa sababu kuifanya mamlaka bila ya usimamizi mzuri ufanisi haupatikani na tuna mfano. Mhe. Mwenyekiti, tunayo mashirika yanayojitegemea katika wizara hii lakini mchango wake katika serikali ni mdogo sana nitaeleza huko baadae. Kuna mashirika mengine ni mzigo kabisa kabisa hayafai hata kuwepo. Sasa hiyo natoa angalizo na mapema kwamba hapa katika kufanya mamlaka usimamizi ni mzuri sana.

Kwa sababu sasa hivi si mamlaka inaitwa ni Idara ya Anga, lakini ndio inayochangia mchango mkubwa kuliko shirika lolote la wizara hii. Sasa hofu yangu kwamba sifa hii isije ikatutoka.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Shirika la Meli. Mhe. Mwenyekiti, hapa sina swali lakini nina ushauri kwamba huduma za uwakala wa meli ziondolewe katika Shirika la Meli. Hizi pesa zinazopatikana kutokana na uwakala zinapotea bure, zinaangamizwa bure. Mimi nadhani Shirika la Meli wangeachiwa meli tu kwa sababu hawa wanakuwa wajanja, wanategemea hizi pesa za uwakala zije pale ziliwe basi.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani hizi pesa kuzinusuru zingewekwa pahala zikapatikana zikatumika na serikali. Lakini leo zinakwenda pale na Shirika la Meli wakizipata bilioni 2 na matumizi yao bilioni 2 ukiangalia katika vitabu vyote vya bajeti. Mhe. Mwenyekiti, nadhani kuna haja uwakala utolewe wabakie na Shirika la Meli ikisha wataangalia watakula nini hawa sasa.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni meli ya MV Mapinduzi tumeona humu katika hotuba kwamba imeuzwa. Je, imeuzwa kiasi gani, aliyenunua nani na kuna mpango gani wa kununua meli nyengine mpya.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nimeona katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 61 lakini zaidi nimeangalia katika kitabu kikubwa hichi ukurasa wa 38 juu ya mchango. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo Afisi Kuu Pemba inachangia milioni 82, Idara ya Mipango na Sera inachangia milioni 80, ambapo hapa ndio michango mingi inatokana na vitengo vya bandari.

Halafu kuna Idara ya Anga inachangia bilioni 1,130,000,000. Kuna Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara bilioni 6, Idara ya Usafiri na Leseni inachangia milioni 310. Kwa hivyo, hapa mchangiaji mkubwa kama nilivyosema ni Idara ya Anga. Sasa inasikitisha Mhe. Mwenyekiti, kuona shirika kubwa kama la bandari kwa kupitia vitengo vyake mbali mbali milioni 80, Idara ya Anga bilioni 1.13. Sasa kwa kweli haiingii akilini kwa sisi tusiofahamu mambo ya undani ya vyombo kama hivi. Kwa hivyo, nasema ipo haja sasa mashirika yetu yote yafanye kazi kwa tija, serikali ifaidike na isiwe kama Shirika la Meli ikichuma bilioni 2 inatumia bilioni 2.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, suala jengine katika hili Shirika la Meli ningependa kujua. Zamani katika hotuba za bajeti ilikuwa tunaelezwa madeni ya shirika hili. Sasa hivi mimi sijaona deni la Shirika la Meli. Je, ndio kusema kwamba Shirika la Meli sasa hivi halidaiwi.

Halafu jengine nataka kujua Shirika la Meli zamani ilikuwa kuna kilio cha wafanyakazi wengi wasiohitajika. Je, Mhe. Waziri sijui juhudi gani alizochukua kuwapunguza wafanyakazi ambao hawana kazi yoyote wanakaa wanaweka zogo tu. Ikiwa kachukua juhudi za kupunguza je, wafanyakazi waliobakia Shirika la Meli ni wangapi. Mbona kuna hasara jamani wakichuma bilioni 2 wanatumia bilioni 2, hii kwa kweli inakuwa haileti tija na tukiangalia mapato serikalini hayapatikani. Mhe. Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo mimi nahitaji majibu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni ushauri kuhusu barabara. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Said Ali Mbarouk namuonea huruma sana Mwenyezi Mungu inshaallah amnusuru na kupata *pressure* kutokana na suala la barabara yake ya Gando.

Lakini zaidi ya miaka 7 barabara ya Gando inatajwa. Halafu barabara nyingi tu za Pemba zinachukua muda mrefu kutajwa utekelezaji haupo.

Ushauri wangu Mhe. Mwenyekiti, serikali sasa isitangaze ujenzi wa barabara kama haina uhakika. Bora ibakie kimya mpaka lile jambo lina uhakika hapo ndio iwatangazie wananchi, lakini wananchi wanaona kama wanafanyiwa dhihaka. Miaka saba utasikia mnatangaza azma tu, watu wanatangaza azma leo, siku ya pili wanachukua fomu, siku ya tatu mchakato. Lakini miaka saba mnatangaza azma ya kujenga barabara, urais uliokuwa mkubwa tunatangaza azma siku moja, siku ya pili mtu anachukua fomu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani bora serikali ingebakia kimya, ikafanya mambo yake kimya kimya mpaka itakapokuwa tayari wananchi wanaona zana zinapelekwa inajengwa hapo itakuwa ni bora, lakini mtawatia waheshimiwa *pressure*.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nashukuru *Alhamdulillah* jimbo langu zuri kuna kipande kidogo tu kutoka Shidi kwenda Mwambani pale nategemea Mhe. Waziri atanimalizia. Lakini kwa kweli wenzangu wengine wataingia *pressure* kwa hii dhihaka mnayowafanyia.

Mhe. Moh'd Ali Salim mwalimu wangu kwa kweli namuonea huruma sana. Maana mara nyengine tukenda katika kamati naweza nikakaa pale Mizingani namsubiri kwa muda wa saa moja kutoka Wambaa kufika pale Mizingani. Anaondoka kwa kweli barabara hii kila siku inatajwa hadithi. Lakini kama alivyosema yeye atakayemrithi kijana atakuja kuendeleza ghasia zake.

Mhe. Mwenyekiti, jengine barabara ya Kangani/Mkanyageni nayo hii imekuwa hadithi vile vile, huu unafika mwaka wa tano inatajwa. Mwaka jana imeombewa milioni 100, mwaka huu milioni 50, nafikiri mwakani itaombewa milioni 10, halafu itaombewa milioni 5. Sasa nasema ile inakuwa kama ni *joke*.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nataka niipongeze Kampuni ya *Zantel* kwa kuchangia bilioni 1.68 katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nadhani kwa makampuni ya binafsi hii ndio inayoongoza. Lakini pia nataka nayo niilaumu kwa kutudanganya. Muda mrefu hapa unasikia watu wa Wete na Mkoani wanadai huduma ya *internet* hawapati. Tunaambiwa aaa sijui tusubiri baada ya minara hii tukiongeza huduma hii itapatikana. Lakini wenzetu Chake Chake ndio wanaofaidi *internet* kwa kutumia *Zantel.*

Sasa sisi wengine kama Mkoani labda utumie Kampuni ya *Vodacom* ndio unaweza ukapata, lakini Wete nafikiri inakuwa tabu, ukenda *Zanlik* sisi watu masikini hatuwawezi. Sisi ni watu wa kutumia *modem* ya shilingi 180,000 ndio

tunazoziweza, sasa mambo ya kwenda *Zanlink* sisi wengine uwezo hatuna. Mhe. Mwenyekiti, tunaomba kwamba watu wa Wete, Mkoani na Micheweni minara ipo, kitu gani kinachowashinda *Zantel* na sisi kutupatia huduma hii ya *internet*.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana ahsante.

Mhe. Ali Denge Makame: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakuja katika mchango ukurasa wa 12 (iii) Sekta ya Usafiri wa Nchi Kavu. Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa juhudi waliyochukua. Kwa kweli sasa usafiri kama unatoka mitaa inayotembea gari zetu za daladala na kufikia mjini umerahisishwa umekuwa afadhali sana, si muda mrefu unakaa unapata usafiri na unafika katika shughuli zako mbali mbali za kikazi. Isipokuwa tu katika magari yanayotumia usafiri huu ningewaomba wakayachunguza sana, kuna baadhi ya magari mengine yanatishia hasa hata maisha ya binadamu. Kwa hivyo, kama inawezekana linapoagizwa lile gari bora alete picha kabisa iangaliwe ile gari iko katika mfumo gani.

Mhe. Mwenyekiti, kuna magari mengine yanatisha bora zile zilizokuwa kama dungu zinaridhisha, lakini kuna nyengine sasa hivi huijui kama *ambulance*, yaani huwa kama cheche utashangaa gari zinavyotembea barabarani, hazina *shape* hasa ya kuchukua abiria wa daladala. Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sekta hii ikaangaliwa sana. Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano ukileta gari katika nchi yetu zenye sifa au sura nzuri zinaleta haiba katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, unajua kuwekwa matuta kwenye maeneo ya skuli au soko kunapunguza ajali na mwendo wa kasi. Kwa mfano, tumeona skuli ya Bububu kwa kipindi kirefu baada ya kuwekwa matuta ajali zimepungua. Hata ukija hapa skuli ya Chumbuni pamewekwa matuta ambayo huwa yanapunguza ajali. Lakini sijui kwa nini Mhe. Waziri anashindwa kuweka matuta kutoka Uwanja wa Demokrasi hadi Amani Kwa Wazee ambapo zinatokea ajali nyingi na tumeshalalamikia sana. Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri akatazama yale maeneo mengi yanayotokea ajali kwa mfano Soko la Mwanakwerekwe au katika maeneo ya skuli.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja ukurasa wa 21 kifungu cha 51 Usafiri na Leseni. Katika usimamizi na ukaguzi wa vyombo yaani magari mimi nimeshangaa sana kuambiwa kuna baadhi ya gari zimezuiliwa zisifanye kazi ya kusafirisha abiria kama daladala na wakati gari hizo ukizitazama sura yake inapendeza kama zile wanazoita dungu. Mhe. Mwenyekiti, ukitazama kituo kikubwa cha madaladala

ni Darajani ambacho ni eneo dogo, daladala mbili tu zinabanana. Je, tukitafuta hizo gari kubwa za maringi sita mfano *costa*, kwa kweli nafasi atakuwa nayo kubwa ya kuenea magari kama hayo makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri akaangalia gari hizi ambazo zimekuwa tegemeo kwa baadhi ya wananchi wetu wengi waliostaafu ndio ajira yao inayowasaidia kutafuta maisha. Kwa hivyo, kosa sio gari, mimi ningeomba akaangalia sana gari ikiendeshwa na dereva yuko vipi, mmiliki wa gari analishughulikia vipi kulitengeneza, pia wakiangalia kama madereva wana leseni za uhakika nafikiri ajali nyingi hazitotokea. Uzembe huu unasababishwa na madereva na wamiliki wa magari, sio hukumu itolewe kwa gari. Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri suala hili la kuziondoa daladala za aina ya dungu alitupilie mbali na zifanye kazi kama kawaida ili kuwapatia ajira ndugu zetu.

Mhe. Mwenyekiti, upasishaji wa madereva hii ningeomba waangalie sana kwa sababu baadhi ya madereva wengi huwa wanapasishwa tu umri si wao kwa kuendesha magari. Kwa hivyo, suala hili ndio linachangia zaidi kusababisha ajali na uzembe barabarani. Namuomba Mhe. Waziri skuli ya udereva iangalie sana ili kuepusha masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Shirika la Bandari. Mhe. Mwenyekiti, nalipongeza sana shirika hili kwa juhudi yake kubwa inayochukua katika kupanga vitengo vyake na shughuli zake mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, Mkurugenzi wa Shirika la Bandari anajitahidi kwa kushughulikia kazi zake za usimamizi. Isipokuwa tatizo kubwa lililokuwepo hii bandari yetu imekuwa ndogo sasa hivi. Kwa hivyo, lile suala la kuwekezwa eneo jengine la bandari Mpigaduri nafikiri tukilipata hili tutampa nafasi nzuri zaidi ya kupanga vitu vyake na mitandao yake katika bandari. Ningeomba suala la utanuzi wa Bandari ya Maruhubi likaangaliwa.

Mhe. Mwenyekiti, suala la minara limekuwa na matatizo sana hususan mnara wa Nungwi. Huu umekuwa kero sana kwa waongozaji meli huwa mara nyingi unababaisha kutokana na mnara na jeti iliyokuwepo pale katika hoteli ya Nungwi. Kwa hivyo, hili ningeomba liangaliwe sana kama alivyosema mwenyekiti wangu linaweza kuja kusababisha ajali halafu baadae jibu likawa halipatikani.

Mhe. Mwenyekiti, nije ukurasa wa 20 kifungu cha 45 barabara ya Mhe. Benjamin William Mkapa, Amani/Mtoni. Mhe. Mwenyekiti, tumeshailalamikia sana barabara hii na kwa muda mrefu, tokea mnamo mwaka 2006/2007 lakini utekelezaji wake bado hatujauona. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hii inaleta

bughudha sana ajali kila siku zinatokea katika barabara hii, mpaka watoto wanakanyagwa vichwa.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba Mhe. Waziri akaliangalia sana suala hili. Kwa kuwa alikuwa anafahamu kuwa ilikuwa ni ahadi ya Jamhuri ya Muungano na alikuwa anajua kuwa fedha italetwa na fedha hii ilikuwa imeshaletwa, kwa hivyo sijui nini kilichomkwamisha kufanya matayarisho ya ujenzi wa barabara ile mpaka kufikia hii leo tumemaliza kipindi hichi cha miaka mitano. Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri akija hapa awaeleze zaidi wananchi ili wafahamu. Mimi sitozuia shilingi, lakini shilingi hiyo itasababisha kuzuiliwa na yeye jinsi ya maelezo atakayoyatoa kwa wananchi na jinsi watakavyomkubali. Hawatozuia shilingi hapa Barazani, sijui huko jimboni watazuia nini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ingawa barabara hii ina majimbo matano, lakini jimbo langu mimi ndio limekwama zaidi, wananchi kila siku wakivuka barabara kwenda skuli wanakanyagwa sana vichwa vyao. Kwa hivyo, ningeomba hili suala aliangalie.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara kama walivyosema wenzangu juhudi wanachukua barabara nyingi wametia lami na nyenginezo wametia vifusi. Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa hilo, lakini tatizo sijui kigezo gani anachotumia cha kufanya aliyefika mwanzo hapewi mradi wa kutengenezewa barabara, yule aliyefika mwisho anapewa mradi wa kutengenezewa barabara.

Mhe. Mwenyekiti, nimsifu tu Mhe. Waziri kwa juhudi aliyochukua barabara ya Fuoni/Kwarara, barabara ya Kissasi/Mwanyanya, hata barabara ya Magogoni/Kinuni kajitahidi sasa hivi ziko vizuri. Kwa hivyo, Waswahili wanasema ukimwona mwenzako ananyolewa na wewe tia maji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ishara hii nadhani Mhe. Waziri kabla hajamaliza kipindi chake hichi labda atanifikiria na kwangu mimi anitilie japo *grader* katika eneo langu la Amani Freshi/Ziwatuwe, barabara ya Kipanga/Kwaboko na hata ile barabara iliyoahidiwa na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume kutoka Kinu cha Soda mpaka Welezo. Lakini kipindi kirefu barabara hii haijafikiriwa na wala haijashughulikiwa kutengenezwa. Ningemuomba Mhe. Waziri akaiangalia sana barabara hii iliyopakana mipaka ya Kwamtipura na Amani ambayo watu wengi wanaitumia.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi imepangiwa *route* lakini wanashindwa kwenda mashimo yamekuwa mengi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri angeangalia ukosefu wa kuitengeneza katika kipindi hichi basi angalau kutia *grader* tu.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi waliotuleta hapa wanalalamika wanasema kwa nini wao wameachwa kwa muda mrefu, wengine wametajwa juzi tu wanafanikisha kutengenezewa. Mhe. Mwenyekiti, kwa ninavyomjua Mhe. Waziri atakuwa ameshayasikia haya na atafanya juhudi angalau na mimi kunitilia *grader* tu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia nizungumzie Idara ya Anga. Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza sana idara hii kwa juhudi kubwa waliyochukua. Mara nyingi ilikuwa mimi nikisimama hapa nalalamika kuwa uwanja wetu wa kimataifa leo utashangaa paka, mbwa wanapenya tu mle kumbabaisha rubani.

Lakini baada ya kelele za muda mrefu namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Anga kajitahidi kujenga ukuta wa kileo, hata uende na doza hauvunjiki. Mwenyezi Mungu aepushie mbali lisitokee tetemeko, lakini ukuta uliojengwa ni mzuri wa uhakika, ndio maana nikasema sehemu ya anga sina maneno mengi leo. Isipokuwa sehemu iliyobakia ile ya uzio wafanye maarifa kama itawezekana japo ukuta wa tofali wa futi mbili ili kuepusha mbwa na paka wasichimbe kuja kuweka uwazi wa kuingia kwenye uwanja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mwisho niwapongeze watendaji wa wizara hii akiwemo Katibu Mkuu, tokea kuwepo Katibu Mkuu mambo yake yanakwenda vizuri tunaona juhudi anayoichukua. Magari mapya wamepata UUB, barabara sasa hivi zinatengenezwa, ingawa na hiyo yangu mimi ipo njiani.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mkurugenzi wa Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara kwa kweli ni kijana hodari sana, namshukuru sana akipatiwa nyenzo tu anafanya kazi. Mhe. Mwenyekiti, juzi tu kaniokoa katika ziara kubwa ya Mwenge wa Kitaifa kumuomba tu kaniwekea njia sawa. Kwa hivyo, nampongeza na yeye kwa juhudi zake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Pemba nampongeza Afisa Mdhamini kwa kweli anajitahidi vya kutosha. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba ujitahidi sana kuwapatia nyenzo hawa ili wakamilishe kazi zote wanazotumwa na serikali.

Kwa hivyo, kwa hayo tu nakupongeza sana na naunga mkono hotuba yake kwa asilimia mia kwa mia, pindipo na hizo barabara zangu zitapigwa japo *grader* tu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa na mimi fursa kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nichukuwe fursa hii kuwashukuru wote watendaji wa Wizara hii ya Mawasiliano na Uchukuzi, kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Afisa Mdhamini pamoja na watendaji wake wote.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kwanza mimi naomba nimpongeze Mkurugenzi wa Bandari, pamoja na mabaya yake anayofanya, lakini yamo na mema mazuri ambayo ameyafanya. Mhe. Mwenyekiti, Mkurugenzi wa Bandari kwa kweli ahadi zake anazoweka nyingi anazitekeleza. Kuna mengi ambayo tumeyaona ambayo ameyatekeleza kwa vitendo kabisa, anaweka ahadi na anaitekeleza.

Kwa mfano, bandarini kwetu pale kulikuwa kuna sehemu ambazo zilikuwa zimechafuka, kwenye sehemu za makontena basi aliahidi na ametekeleza. Tulipokwenda kwenye kamati tumeona na tumeridhika kuwa amefanya kweli.

Suala jengine kuna ukuta ambao ulikuwa una mmomonyoko baina ya bandari ya Wete. Kwa kweli amefanya jitihada kubwa ya kujenga ukuta mkubwa wa kuridhisha, ambapo ule mporomoko uliokwenda ukaathiri watu kule Wete basi tunatamaa ya kuwa hauwezi kutokea tena. Kwa kweli wamefanyakazi ya ziada tena ya kupongezwa.

Mhe. Mwenyekiti, Mkurugenzi wa Bandari kwenye sehemu ya mnara ambao uko Kigomasha, aliouzungumza Mhe Said Ali Mbarouk, tumekwenda wamejitahidi kuuhushi ule mnara. Kuna majengo ya wafanyakazi wamejengewa vizuri sana na wanaendelea kujenga. Kama kuna matatizo ya mnara kutowaka hilo ni tatizo jengine ambalo namuomba Mkurugenzi afanye jitihada, kwa sababu ule mnara ni muhimu na ni mnara wa kimataifa ili utengenezwe na huo uwe unafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, Waheshimiwa Wajumbe wanakuuliza hawajalifahamu hili neno ‘kuhushi’.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ni kutengeneza, yaani ni kuutengeneza ule mnara. Hiyo ni kamusi ya Kimicheweni, kuutengeneza ameuhushii saafi. *(Vicheko/Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ninalomuomba Mkurugenzi wa Bandari, ni suala la Bandari ya Mkoani imekuwa ni tatizo sugu na kila anayesimama hapa ana lalamika na suala hilo. Kwa hivyo, namuomba Mkurugenzi asimamie kwa jitihada zote, ili tatizo la Bandari ya Mkoani liondoke, ajitahidi kadiri ya uwezo wake ili na lile tatizo lisimtie doa liondoke, alikamilishe hili ili liwe zuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende kwenye utunzaji wa barabara, kwa sababu waswahili wanasema sadaka huanza nyumbani, kwa hivyo na mimi ikiwa nikisahau ya nyumbani, nitakuwa sikutoa sadaka.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu barabara namuomba Mkurugenzi pamoja na waziri wakishirikiana, waone kwamba barabara ile iliyoko Chuo cha Kiislamu ina umuhimu na hiyo kujengwa, kwa sababu kile kipande ni muhimu. Kule kuna Chuo cha Kiislamu, kuna wanafunzi wanaotoka sehemu mbali mbali ya Zanzibar, pengine tunaweza tukapata wanafunzi wanaotoka nje ya Zanzibar na wageni wengi wanaokwenda kule na ukizingatia kule pia kuna hayo maeneo huru. Lakini Mhe. Mwenyekiti, katika bajeti hii na kwenye matengenezo ya barabara ya maeneo huru yameingizwa kwamba kutatengenezwa Fumba, na kule Micheweni maeneo huru yapo lakini haimo na wakati tunataka hawa wawekezaji wakienda maeneo huru basi barabara watakayopita ni ile. Sasa kama haikutengenezwa itakuwa hizo miundombinu za kuwapeleka hao wafadhili hazipatikani.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwamba ile barabara ilianza kuwekwa kifusi lakini kikakwama njiani. Sasa waswahili wanasema, kufanyakazi usiifikishe mwisho ni sawa sawa na kuwa hukuifanya. Kama mimi nitapeleka suruali yangu ikashonwe charahanini, lakini nikashonewa mguu mmoja tu, nikenda kutaka nguo yangu imeshonwa mguu mmoja. Haya hivyo nitaambiwa nimeshonewa. Kwa hivyo, kile kifusi kimetiwa sehemu mawili tu. Nawaomba kwa kuwa ile kazi wameianza vizuri, basi waende wakaimalize. Ni sawa sawa na kushonwa nguo mguu mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri zile barabara azione kwamba zina umuhimu sana, kuna maeneo huru, kuna Chuo cha Kiislamu na kuna milleniam. Kwa hivyo, hicho kijiji ambacho tunataka kujengewa kama hakuna barabara kitakuwa vipi. Namuomba Mhe. Waziri ile barabara aimalize.

Halafu suala la pili. Kabla ya kuambiwa kwamba inakuja kujengwa barabara ya Konde Gando Wete, baada ya kuwa kifusi kinachimbwa kule Micheweni, tulikubaliana na Afisa Mdhamini pamoja na waziri kama kule kwenye barabara yetu inayochukuliwa kifusi ile ya watu wa Mjini Wingwi ambayo kila kifusi kinatoka pale, basi na wao wafadhilike na kile kifusi ili wapate faida. Kwenye ile barabara ya kwao watiliwe na wao kifusi ili na wao waone kwamba wamepata faida. Lakini leo wanatufanyia yale maneno ya Kiswahili ya kuwa ‘mfinyanzi ale kwenye kigae’. Kwa sababu kifusi kinatoka Micheweni sisi watu wa kule Micheweni hatufaidiki, mnatufanyia vile vile kwamba ‘mfinyanzi anakula kwenye kigae’.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri, tulikubaliana na tulikwenda. Kwa bahati nzuri siku hiyo niliwakuta wote, waziri, mkurugenzi wa mfuko wa barabara, pamoja na watendaji wake nikawaomba kama jamani hii barabara imechafuka kupita kiasi. Hali ya kuwa hata mtu akitaka kupeleka mgonjwa hospitali hasa kwa kipindi hiki cha mvua hawezi kumpeleka kwa sababu wengine wanakwenda na mabaskeli, wengine ndani ya gari, kila mmoja anakwenda kwa uwezo wake. Nawaomba angalau mtutilie kifusi. Lakini cha kusikitisha pamoja na kuwasifu kwangu kote, mimi kwa vile ninawasifu basi hata kile kifusi kunitilia.

Kwa hivyo, nawaomba waheshimiwa tena nasema kwa masikitiko, naomba na mimi ile barabara mnitilie kifusi, kwa sababu barabara zile zinatumika kwa magari yetu sisi viongozi ambao ni wawakilishi na wabunge, tunaisadia serikali kwa hayo magari yetu, gari zetu sisi ni *ambulance*, saa zote tunachukua wagonjwa tukiwapeleka hospitali. Kwa hivyo, zile barabara mukitusaidia basi yale magari yetu yatakuwa kidogo mnatupa nafuu.

Mhe. Spika, kama barabara ya Mhe. Said Ali Mbarouk, sote tunasikitika. Mimi nilikuwa naona gari yangu itaharibika njiani kwa ubovu wa barabara na ile gari ya mheshimiwa niliona kama gari yake ilikuwa ndio, sijui imekatika kitu gani. kwa hivyo, jamani tunaposikitika tuonewe imani. Mhe. Ali Denge Makame yule pale, yeye anasema mimi nashukuru nimetengenezewa barabara yangu. Kwa hivyo, na sisi tukisema tusikilizeni, tukilalamika ni wajibu wetu, kwa sababu watu wanatuangalia machoni, kuwa wana viongozi. Sasa na sisi viongozi tukisema tusikilizeni.

Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri ile barabara yangu mnitilie kifusi. Leo hii nimepigiwa simu kwamba *bulldozer* lenu liko linachimba mawe kule Micheweni, hasa eneo langu la Mjini Wingwi. Kunachimbwa mawe kwa ajili serikali inataka mawe kutengenezea barabara. Lakini sasa sisi kule kunakotoka vipuri ndio hatufaidiki. Kwa hivyo, tunawaomba jamani mutusaidie.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende kwenye Shirika la Meli. Waheshimiwa Meli ya Mapinduzi imeuzwa, kama imeuzwa Zanzibar ni visiwa. Jamani kila siku tunasema kama serikali kutakuwa na meli yake ya uhakika ni matatizo. Kama meli imeuzwa ya mapinduzi, basi tunaomba serikali ifanye jitihada lakini isipange siku tu kwamba tutanunua meli, kila siku tuta tuta mpaka lini tuta. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri asimamie kwa nguvu zake zote, kama tunaona Zanzibar ni kisiwa na kama serikali haina meli zake kwa kutegemea tu meli za wafadhili, kuna siku wafadhili tutazitaka meli tuzikose. Ingawaje ukiwa na fedha hukosi lakini utakosa. Lakini ukiwa na yako je, ukiwa na yako unafanyakazi kwa ajili ya chako, mtu chake hakikosi.

Kwa hivyo, nawaomba mufanye jitihada ili muone kuwa kuna umuhimu wa serikali kuwa na meli yake, kwa sababu meli ya maendeleo imeshachoka. Mhe. Spika, meli ya maendeleo sasa hivi ni spana mkononi, hasa hiki kipindi kinachoingia cha upepo mkali. Tunakwenda hatujui Mwenyezi Mungu atunusuru, lakini upepo mkali kama huu meli ikija ikizima mashine ndani ya safari tena mkondoni ni hatari, kwa hivyo ni spana mkononi. Kuna umuhimu wa kununua meli za serikali ili muona kuwa ni muhimu na hili mulisimamie kwa kidete kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwa Mrajis wa Meli. Mhe. Mwenyekiti, huyu kijana ni hodari kweli kweli na anasimamia kazi zake kikamilifu. Lakini awezeshwe, kwa sababu kama nilivyozungumza kama Zanzibar ni visiwa, basi tuhakikishe kuwa safari zetu nyingi ni za baharini. Sasa kuwezeshwa kwake ni kwamba apewe vyombo ambavyo vitakuwa vina uhakika wa kuwa inapotokea ajali ili yeye kama Mrajis aweze kuwasaidia, aweze kufuatilia na kujua kwamba hapa ilitokea ajali ni chombo gani kitafuatilia ili kuweza kuokoa watu na maisha yake.

Lakini huyo Mrajis hata akipigiwa simu kuna matatizo kadha kadha hana la kufanya atafanya nini. Kwa hivyo, Zanzibar inastahiki kuwa na vyombo maalum vya uokozi, ikiwa ni maboti, ikiwa ni *helicopter* na vyenginevyo basi serikali itajua vya kupanga. Lakini naiomba serikali hili suala ilione kuwa lina umuhimu na ilizingatie, kuwa na vyombo vya uokozi vya uhakika, kwa sababu Zanzibar ni visiwa, kama ni visiwa watu wetu wanasafiri kwa meli, kwa majahazi na vyombo vyengine. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hili suala nakuomba ulizingatie na ulione kama lina umuhimu mkuhwa.

Mhe. Mwenyekiti, vyombo vya uokozi vinakuwa ni vya aina nyingi. Kwa mfano kama siku ilipopata ajali meli ya Serengeti, iliporipuka watu wakawa wanashangilia kule juu tu, meli inawaka kule hakuna chombo cha kuweza kuchukua maji na kuzima, watu wanashangilia meli inawaka. Kwa hivyo, vyombo vya uokozi vinakuwa ni vya aina nyingi juu baharini. Mhe. Waziri na hili ulizingatie na ulione lina umuhimu.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda haraka ili nisikumalizie muda wako. Mhe. Mwenyekiti, nakwenda kwenye Idara ya Anga, nasikia itakuwa Mamlaka hivi karibu ndio maana nawaombea dua kabisa. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli na hawa nawashukuru sana na ninawapongeza serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa kweli uwanja wa ndege ulipo hapa Unguja ni uwanja sasa hivi wa kujivunia na sisi tunaweza kujivunia kama tuna uwanja wa ndege uliokuwa ni safi kabisa. Zaidi tutajivuna ikiwa lile jengo la abiria nalo litakuwa limeshakamilika na *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu litakamilika.

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Idara ya Anga Zanzibar sisi tumebahatika tuna viwanja viwili tu, kila siku mimi nasema nikichangia, uwanja wetu ni uliopo Unguja na uliopo Pemba. Sasa siku zote mtu anapovaa koti basi ndani anavaa na shati. Lakini sisi tunavaa koti ndani haina shati tutaonekana vipi. Kwa hivyo, uwanja wa Unguja ni mzuri, lakini Pemba haujulikani. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri zile taa ambazo haziwaki kwa muda mkubwa, pamoja na kwamba sasa hizi tunatengeneza uzio, maana tulikwenda kukagua tukaona kama hivi karibuni *Inshaallah* uzio utakuwa mzuri.

Lakini uzio tu hautoshi. Vile vile kama ndege ikipata dharura ya kuja Unguja usiku, ikaenda zake mpaka Pemba wakati iko kwenye dharura na taa haziwaki uwanjani je, itajihami vipi, haina vya kujihami. Kwa hivyo, waheshimiwa kutumia ule uwanja kuwa tutumie mchana tu sio busara, tutumie na usiku. Viwanja vyetu viwili tu kwa hivyo tuone kwamba kuna umuhimu serikali ifanye kila jitihada inavyoweza, kama hatujataka kutengeneza ule uwanja, basi hata zile taa angalau ziwe zinawaka, kwa sababu ule uwanja uwe unaonekana. Leo kukiwa na mvua basi uwanja hautumiki, usiku ukiingia Magharibi uwanja hautumiki.

Mhe. Mwenyekiti, siku moja tulikwenda Tanga kamati ya mawasiliano, kwa bahati nzuri au mbaya wajumbe wetu wawili ikabidi ndege ikajaa wakakosa nafasi, ikabidi kije kindege kidogo kuwachukuwa ili kuweza kutufuata sisi kule. Basi usiku ulikuwa umeshaingia kile kindege kilikuwa kinaruka hakijui kuruka wala kutua, kwa sababu kinakimbilia usiku usije kuingia kiwahi kurudi kuna na kutua. Jamani tusifanye hivi, safari za ndege ni tofauti na safari za punda. Punda unamrukia tu unakwenda zako utakako, lakini ndege mpaka mkamilishe masharti. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakuomba na hili ulione kwamba lina umuhimu, ule uwanja wa ndege wa Pemba nao ni uwanja.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nisikumalizie muda wako. Mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia juu ya mia, ninamuomba Mhe. Waziri barabara zangu zikatengenezwe. Ahsante Mhe. Mwenyekiti,

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi.

Kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri na wizara yake pamoja na wafanyakazi wote wa wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya. Kwa kweli wanafanyakazi kubwa na ni kazi ambayo kwamba itasaidia sana maendeleo ya kiuchumi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, biashara, viwanda na uwekezaji kama ni sekta viongozi za kuleta maendeleo ya uchumi katika nchi hii. Nategemea sana kuona kwamba miundombinu inarekebishwa na kuwa katika hali nzuri. Kwa hivyo, naomba kumshukuru sana na kumpongeza Mhe. Waziri kwa juhudi za kuongezwa kwa barabara ya uwanja wa ndege wa Unguja pamoja na kujenga uzio, pamoja na kwamba kuna mpango wa kujenga *terminal* nyengine ambayo itaweza kusaidia kuweka uwanja wa ndege katika hali ya juu kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, utalii wetu unategemea sana namna gani uwanja wa ndege pamoja na bandari utaweza kurekebishwa na kuwa katika viwango vya kimataifa. Nampongeza sana Mhe. Waziri. Lakini ningeomba nimuulize maswali mawili.

Swali la kwanza namuuliza kuwa Mhe. Waziri katika kitabu chake ameandika kwamba mkandarasi ameshapewa kazi ya kujenga hiyo *terminal* mpya ya uwanja wa ndege na mikataba imeshatiwa saini na kazi inaanza mwezi unaokuja. Tungeomba tupate taarifa zaidi kwamba gharama zake ni kiasi gani na uwanja huu utamalizika kujengwa lini na pesa hizi zitapatikana kwa mkopo au kwa msaada.

Mhe. Spika, suala hili ni muhimu sana na sisi tunapenda kuliona kuwa linafanikiwa. Vile vile tungeomba tujuwe kwamba je kutakuwa na *domestic* mbali na *International* mbali au mchanganyiko kama tulivyo sasa. Maana mpaka sasa hivi hali ni mbaya, anayekwenda Pemba anaingia hapo hapo, anayekwenda Italy anaingia hapo hapo na anayekwenda Dubai anaingia hapo hapo. Kwa kweli hali kama ile inaleta mtafaruku katika uwanja wa ndege. Kwa hivyo, tungeomba atutafutie ufafanuzi huo.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika suala la bandari. Kuna haja kubwa ya kutenganisha baina ya sehemu ya mizigo na abiria. Kazi imefanywa vizuri, lakini bado haikidhi haja. Kwa kweli ipo haja ya kuboresha zaidi sehemu ya abiria, watalii wanapokuja ili waone hali ni nzuri waweze kuridhika, kwa sababu hali bado haijawa nzuri hasa katika ile sehemu ya *waiting shade* na hadi sehemu ya *migration* na sehemu nyengine. Kwa kweli hasa inaponyesha mvua hali inakuwa sio nzuri. Kwa hivyo, tungeomba ni utaratibu gani tunataka tufanye kazi ya kuweza kushajihisha suala la utalii katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nakwenda moja kwa moja kwenye suala la Shirika la Meli. Shirika hili katika ukurasa wa 46 na 47 wa kitabu chetu hiki, imeelezwa kwamba Shirika la Meli kwa kweli hali yake sio nzuri, hivyo shirika ifanye maamuzi ya kubadili meli tulizonazo ambazo zimepitwa na wakati kwa kuziuza na kununa meli nyengine zitakazoweza kuhimili ushindani ndani ya soko.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni ngonjera ya kila mwaka inasomwa hapa, lakini utekelezaji hakuna. Kwa kweli mimi naona kwamba kama hili shirika limetushinda bora tulifunge. Kwa sababu ukisema kwamba kila mwaka unasema maneno hayo kwa hayo, biashara haiendi hivyo. Tumeshauri sisi kwamba hili suala la shirika, lingekuwa kama shirika ambalo linajitegemea kisheria likawa na bodi yake na likaanza kufanya kazi zake vizuri, lakini bado shirika hili halina mamlaka yake na linafanyakazi katika njia ya hasara.

Katika ukurasa wa 47 utaona shirika hili limepangiwa kupata bilioni 2,709,009,500 lakini limepata bilioni 1,651,840,466 ambayo ni sawa sawa na asilimia 60.9 au asilimia 61 kwa ufupi. Katika kitabu hiki ili kuficha ficha limeandikwa kwamba limepata asilimia 63, wakati sio kweli ni asilimia 60 tu hizi. Vile vile likaambiwa kwamba limetumia bilioni 1.820,294,973 sawa na asilimia 85, sio kweli ni asilimia 67.1. lakini ukiangalia hapo ikiwa kweli ndio kweli na uongo ni uongo. Ikiwa shirika hili limekadiria kupata 2.7 halikuweza kufikisha kiwango hicho, limepata 1.6. Lakini limetumia 1.8 tayari kuna nakisi ya milioni 168,454,507 je, hizi milioni 168 wamezipata wapi, wamezikopa au serikali imewapa ruzuku au vipi, maana yake hatujui pesa hizi zimetoka wapi hata wakazitumia wao, lazima zimetoka mahala, aidha wamekopa au wamepata ruzuku. Kwa hivyo tunahitaji ufafanuzi pesa hizi zimetoka wapi.

Mhe. Spika, kwa kweli hali kama hii inatia shaka sana kwamba shirika sasa hivi linashindwa kufanya kazi zake. Kwa hivyo, njia ni mbili, aidha kurekebisha kabisa hili shirika au kulifunga kabisa vyenginevyo huko tunakokwenda hali itazidi kuwa mbaya zaidi na kwa kweli badala ya kupata mapato kutoka katika shirika hili tutapata hasara. Kwa sababu mapato yote kama alivyochangia Mhe Haji Faki Shaali pale kwamba mapato yote yanayopatikana kwenye meli yanaliwa na shirika hili. Kwa hivyo, shirika hili ni shirika nyonyaji haliingizi kitu. Kama ni la mfanyabiashara basi zamani ameshalifunga shirika kama hili. Mhe. Mwenyekiti, nashauri kwamba lazima hatua madhubuti zichukuliwe juu ya shirika hili vyenginevyo itakuwa tunadanganyana kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja katika masuala ya barabara. Mhe. Mwenyekiti, katika masuala ya barabara tukiangalia barabara za Unguja *Alhamdulillah* zimejengwa nyingi kwa viwango vya lami. Lakini kwa Pemba ingawaje bajeti hii imejikita katika kuangalia kwenye barabara za Pemba, lakini kwa kweli barabara za Pemba haziko katika hali nzuri na kwa hali hiyo Pemba kazi hazifanyiki.

Mhe. Spika, mimi kule sasa hivi namjengea nyumba zake Mhe. Mugheir nyumba zake za madaktari hospitali. Kwa muda wa miezi mitatu nimeshindwa kwenda kabisa. Kuna sehemu ya Mtangani, Mgelema, Gando na Mtambwe

hakuendiki kabisa, kuna mvua kali sana njia haziendeki na njia hizo wakati wa jua gari zinakufa na wakati wa mvua hakuendi chochote na wananchi wanaokaa maeneo hayo wamo katika dhiki ya hali ya juu kabisa. Kwa hivyo, nasema kwamba kwa kweli mipango ya Pemba sio mizuri.

Mhe. Mwenyekiti, watu wanakaa na kujiuliza, kwa sababu sisi tunafanya mambo yetu hatufanyi mahesabu. Inakuwa kwa nini barabara za Pemba na kwa nini barabara ya Bumbwini, wanaona hapa kuna kuwa na *political questionable*, kabisa. *Why* Bumbwini, *why* Pemba, *why?* Maswali kama haya ndio yanaleta *contradiction* katika siasa za nchi yetu. Ningemuomba Mhe. Waziri alizingatie hilo na aone umuhimu wake na kuona kwamba barabara hizi zinatengenezwa kwa haraka ili kuondosha masuala ambayo yanaweza kuleta matatizo katika siasa za sasa hivi za maridhiano zinazoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, katika tunapotengeneza barabara au tunapojenga majumba tunachimba mashimo sana ya mchanga, mawe na vifusi, katika masuala ya mazingira yanazungumzwa sana masuala haya hata katika Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira na wizara mbali mbali yamezungumzwa na lawama nyingi hutupiwa Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwamba haya machimbo. Kwa mfano ukienda zako Mombasa, kule kuna eneo kubwa sana limechimbwa na kuna Kiwanda cha Saruji. Lakini utakuta maeneo yale yakishachimbwa tu yanafungwa na wanapewa wafanyabiashara ambao wanafanya masuala ya utalii. Ukifika Mombasa kwenye kiwanda cha saruji Bamburi pale, kuna *zoo* zuri kabisa limejengwa ndani ya shimo lililochimbwa kifusi kwa muda mrefu, pale utakuta pana wanyama mbali mbali wanafugwa pale na kuna bustani nzuri. Kwa hivyo, maeneo kama haya hayawachwi vile vile baada ya kuchimbwa wanapewa wafanyabiashara wanaya-*invest*, wanaya-*develop* na yanakuwa ni vivutio kwa watalii. Sio desuster ya nchi katika masuala ya mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano pale Mwanakwerekwe. Zamani pale tukichimba mchanga kiasi miaka 25 iliyopita. Sasa hivi pamekuwa ni bwawa kubwa sana la maji ambalo linaweza kuleta hatari baadae au hata sasa hivi, miripuko ya maradhi. Lakini pale panaweza pakatengenezwa na pakawa ni *fishing pool* pazuri kabisa, watalii wakaenda wakaona ni pahala panavutia na pana tija na nch ikapata mapato yake. Kwa hivyo, nafikiri maeneo kama yale yasiachwe tu yakawa yanakwenda ovyo ovyo ni lazima yawekwe katika mpango wa uwekezaji, na yawe yanaleta tija katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nitazungumzia habari ya huo huo ujenzi wa barabara. Barabara zinajengwa Mhe. Mwenyekiti, lakini wasi wasi wangu mimi

ni je, hizi *road design and road safety regulation* zinafuatwa. Maana kama *road design* zinafuatwa basi tutaepukana na ajali sana.

Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, tuangalie ukitoka Mkapa *Road* njia ya Amani kuelekea Mwera ukitoka Mjini huku basi pale kuna *round about* ile, sifikiri kama palifanywa *design* pale. *Round about* ile ni *very dangerous* na inaweza kuleta *disaster* siku moja. Sifikiri kama pale *design*, pale nafikiri pamejengwa tu, mtu katoa mawazo katika kichwa chake ikajengwa ile *round about* ambayo ni nyembamba sana na mzunguko mdogo sana, ile ni hatari sana. Sifikiri kama hapa kwetu Zanzibar tunayo hii *road safety* na *road design*, nina wasi wasi sana. Kujenga barabara bila kuzifanyia *design* zitaleta ajali mara kwa mara.

Mhe. Mwenyekiti, nyinyi mtashika mnawalaumu dereva na utingo, hapana. Madereva wana makosa yao, lakini *road design* inachukua asilimia 60 ya matatizo ya ajali katika nchi yetu hii. Kwa hivyo, mimi nataka kuona je, Mhe. Waziri hizi njia zinazojengwa zinakuwa *design* au zinajengwa tu, *road safety* zinachukuliwa, nani anafanya, angalau atutowe wasi wasi kwamba hili suala halina matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nataka kulizungumza ni suala la hizi *seaport* na *airport*. *Seaport* na *airport* hizi, tusigeuke kama Mhe. Ali Juma Shamuhuna, tulipomwambia kwamba bora kodisha huu uwanja wa amani. Akasema hali nzuri kama hii tukodishe. Mimi kama nyumba yangu siikodishi wakati ni mbovu, kwa sababu sipati kodi. Mfanyabiashara wewe utachukua jumba lako bovu ukakodishe nani ataitaka, utapata bei ndogo. Lakini nyumba yangu niliyoifanyia matengenezo ya kutosha ndio ninaikodisha kwa sababu nitapata bei nzuri na nitaweza kumuongoza yule mtu.

Kwa hivyo, nasema kwamba tunajenga Uwanja wa Ndege *Alhamdulillah*, utakuwa na litafanywa ni shirika sawa, lakini *management* ni *very important.* Management ya Zanzibar sasa hivi sio nzuri tusidanganyane, katika viwango haimo. Kwa hivyo, tuangalie ni namna gani tunaweza kuona kwamba hivi viwanja vya ndege vipya kunakuwa na *management* ya aina gani.

Mhe. Mwenyekiti, tusione haya wala tusione vibaya, Singapore ni nchi iliyoendelea kweli kweli na uwanja wa ndege wake ni mkubwa sana. Lakini *management* ya uwanja wa ndege wa Singapore unashughulikiwa na ZENATA. ZENATA ni Shirika la Uwanja wa Ndege wa Dubai. Wale wana *tender airport* chungu nzima za Far East huko sasa hivi. Lakini ZENATA ni Shirika la Uwanja wa Ndege wa Dubai ndio unaendesha uwanja wa ndege wa Singapore, tusione haya wala tusione vibaya. *That is how we can make money, that is how we can make use of that infrastructure. Otherwise* itakuwa ni *useless*.

Kwa mfano ukiangalia Zanzibar Airport inaweza ikaipiku Nairobi Airport ikawa ni *transit Airport* nzuri sana, na madege kutoka South Africa yakatua hapa kwanza. Kwa hivyo, inaweza ikaleta fedha zaidi. Lakini panataka watu wenye ujuzi, watu wenye *vision* katika mambo ya kibiashara ya namna hii. Kwa hivyo, naomba tusije tukaona haya na tukang'ang'ania tu shirika lisimamie. Sawa shirika lisimamie lakini ile *management* tuangalie ni namna gani ya kuweza kufanya ili *management* iweze kuwa nzuri na iweze kupata fedha nzuri ili tuone tija katika nchi hii. Kwa kweli tukifanya hivyo tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, ningeomba hii wizara yetu kiasi miaka 15 iliyopita, wizara hii ilikuwa na *system* nzuri sana ikifanya hapa, tulikuwa tuna *contractors* wa Zanzibar ambao wote walikusanywa na tulikuwa Hoteli ya Bwawani kwa muda wa mwezi mzima na kupewa mafunzo jinsi gani ya kufanya matengenezo barabara, namna ya kutia viraka, namna ya kutia kifusi ku-*maintain culverts*, kwa kweli tulipewa elimu kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, mambo hayo ilikuwa baina ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ya SMZ pamoja na Shirika la Ujerumani, tulipelekwa mpaka Moshi kwa ajili ya kwenda kuangalia namna ya kutengeneza barabara. Kwa kweli tuliambiwa baada ya kumaliza mafunzo yale, basi wakandarasi wale watapewa kazi ndogo ndogo za kuweza kusaidia. Kwa hivyo, nimeona kwamba humu wamo *contractors* ambao wanapewa kazi ndogo ndogo, lakini hiyo sio madhumuni ya mafunzo yale yaliyotolewa. Mhe. Mwenyekiti, fedha nyingi hivi sasa ziko kwenye Mfuko wa Barabara, lakini zote zimekuwa *focus* kwa ajili ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Lakini Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi iache kazi ya kuziba viraka, kuzibua mitaro, njia ndogo ndogo za kutia vifusi. Mhe. Mwenyekiti, nadhani ni vyema itafute njia nyengine ya kuweza kuajiri *subcontractors* ambao watafanyakazi za kuziba viraka na kusafisha *culverts*, kufyeka majani pamoja na kutengeneza misingi. Kwa mfano, Tanzania Bara hivi sasa masuala ya barabara mengi sana yanashughulikiwa na Kampuni Binafsi na zimeendelea sana *TANROAD*. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wachukue mfano wa *TANROAD* na waulete Zanzibar, ili *Private Sectors* washirikiane nao katika masuala mazima ya kujenga barabara zetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba niheshimu wakati wako nimalizia hapa. Ahsante sana na nampongeza sana Mhe. Waziri pamoja wa watendaji wake na kwa niaba ya Jimbo langu la Ikulu naunga mkono hotuba ya bajeti ya wizara hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Wasallam Allaykum Warahmatullahy Wabarakatu.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nami baada ya kusubiri muda mrefu hatimaye nimepata nafasi ya kuweza kuongea machache katika Hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kama wenzangu na mimi sina budi na ninayo kila sababu ya kuipongeza wizara pamoja na watendaji wake kwa juhudi pamoja na kazi ambazo wamezifanya, ambapo wengi wetu ni mashahidi na vitu ambavyo tunaweza kuviona na wala sio vile vitu vinavyozungumzwa kila siku, pamoja na kwamba bado kuna mapungufu ya hapa na pale.

Kwa hivyo, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa hatua ambayo tumefikia, kwa upande wa ujenzi wa barabara mbali mbali, uimarishwaji wa gati au bandari. Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, ninayo kila namna ya kusifikia suala hili, kwa sababu naanza hizi kazi hali ya bandari ilikuwa vyengine na sasa iko vyengine. Kutokana na hali hiyo, sina budi kutoa pongezi kwa wizara pamoja na watendaji wake.

Nianze mchango wangu katika suala la mazingira na Mhe. Subeit Khamis Faki alisema sana hapa pamoja na Mhe. Hija Hassan Hija na mimi ni shahidi, kwa sababu nilikwenda na kushuhudia hali halisi ambayo iko kule Mkoani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyomalizia Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, nilikuwa nikiliangalia suala zima la mazingira kwamba si tu uharibifu, lakini tunaweza kuyatumia hayo maeneo. Kwa kweli nilikuwa sijui kama pale Mwanakwerekwe mwanzo wake palichimbwa ndio pakafikia vile.

Tatizo letu naona ni kuyaendeleza maeneo ambayo tumeyatumia na labda wenzangu pamoja na wananchi kwa jumla tujue kwamba maendeleo yanafaida na hasara zake. Miongoni mwa hasara ni haya maharibiko au tunapozungumza uharibifu wa mazingira. Kwa hivyo, hatuna budi kwamba haya yatakuwepo, yapo na yataendelea kupewo, kwa sababu bado tutafanya mambo mengine makubwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kwa kushirikiana na wizara zinazohusika kuona jinsi gani yale maeneo yanaendelezwa, kwa sababu wakati tulipotembelea maeneo ya Msuka kama sikosei sehemu aliyoizungumza Mhe. Hija Hassan Hija. Kutokana na hali halisi ya mazingira ya eneo lile, basi niliwahi kufanya *jock* kwamba hili eneo kwa mujibu lilivyo tunaweza kufanya utaratibu na kuingia maji na mandhari yake ikabadilika, yaani ule mbuyu ukawa umewekwa katikati umezungukwa na maji kama vile sehemu ya Mwanakwerekwe.

Vile vile ni eneo karibu na bahari pakajengwa hoteli wakaja wawekezaji na kukawa na mazingira ambayo yatavutia na ile hasara tuliyopata ikafidiwa, kwa jinsi ya fedha itakayoingia kutokana na uwekezaji na kuliendeleza eneo lile. Sasa nadhani tuwe tunalenga kuona kwamba tutakuwa tunayaendeleza maeneo kama haya pamoja na uharibifu wa kimazingira uliotokea, lakini ufidiwe kwa kutengeneza kitu chengine ambacho kinaleta tija.

Mhe. Mwenyekiti, nikiacha hapo kwa sababu ya muda mdogo nataka niwahi kuzungumza mambo mawili matatu, sasa niende kwenye utengenezaji wa barabara. Kwa kweli na hapa sina budi kama wenzangu kutoa pongezi nyingi barabara nyingi zimetengenezwa tunaziona na zinaendelea na mimi mwenyewe pamoja na wenzangu tumeshuhudia haya.

Lakini tatizo kubwa kuhusiana na masuala haya ya barabara ni vifaa. Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hili hawa wenzetu wanaotengeneza njia ya kurukia na kutulia ndege wanavyo vifaa vingi. Kutokana na hali hiyo, nilijaribu kumuomba Mhe. Waziri aone kwamba kuna haja ya serikali kukaa na kufanya mazungumzo, ili vile vifaa kwa sababu si vyetu na wao wamekuja kwa ajili ya kutengeneza na wanategemea kuondoka navyo wakati watakapomaliza shughuli zao.

Kwa hivyo, hivi sasa tunao muda wa kuviazima na tunaona barabara mbali mbali zinakatwa na kutengenezwa. Sasa baadaye watakapoondoka navyo, nadhani tutarudi kule ambako Waheshimiwa wengi walikuwa wakipiga kelele kila siku kiasa miaka saba inazungumzwa na wala hakuna kinachofanyika. Mhe. Mwenyekiti, ukweli vifaa hivi ni ghali na serikali uwezo wake mdogo na pengine na ufadhili pia nao unakuwa na mashaka yake. Sasa kwa sababu vimeshafika nadhani serikali ikae na ione jinsi ya kufanya mazungumzo na vile vifaa ikiwa kwa mkopo au kwa namna yoyote iwe ambayo wataiona, basi watakapoondoka vibakie kwa ajili ya kuweza kutusaidia na kuendeleza shughuli nyengine.

Suala jengine kuhusiana na barabara Mhe. Mwenyekiti, naiomba wizara kwa makusudi kabisa wawe na mashirikiano na Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atueleze kuhusu suala hili, kwamba kuna masuala haya ya kuweka miundombinu mbali mbali kama vile masuala ya umeme, maji na hivi ni vitu ambavyo vinahusiana na wizara hii.

Kwa hivyo, jinsi gani wanaweza kufanya mazungumzo ya pamoja na kazi ikaweza kufanyika kwa ufanisi, kwa sababu kuna malalamiko ya wananchi kwamba barabara zinatengenezwa. Lakini wakati huo huo kuna matengenezo ya kulaza mabomba ya maji, yaani kunafukuliwa, kunabomolewa na halafu

kifusi kinaangushwa kwenye nyumba za watu au mashambani na kupelekea kupata hasara.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri ni vyema wakae kwa pamoja na baadaye watueleze jinsi gani wanafanya mashirikiano na wizara husika, ili kuona matatizo haya hayaendelei, kwa sababu yatakapokuwa yakiendelea yatatupa shida kidogo. *(Makofi)*

Hata hivyo, kwenye suala la ukataji wa viwanja kwa ajili ya maakazi pamoja na matumizi mengine mbali mbali, masuala kama haya yafikiriwe na hususan maeneo ya kupitishwa barabara. Mhe. Mwenyekiti, hivi asubuhi Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum alizungumza kwamba lazima tufikirie huko tunakokwenda maendeleo yatakuja na tutahitaji kupanua yakiwemo masuala ya barabara.

Sasa katika kupima maeneo ya barabara ni vyema kuzingatia kwa muda wa miaka 50 ijayo ingawa hivi sasa serikali haina uwezo wa kujenga barabara, lakini waone umuhimu wa kuweka *reserved areas* kwa ajili ya barabara kwa wakati ujao.

Kwa kweli kwanza tutaiepusha serikali kubeba mzigo wa kulipa fidia kwa wananchi na wakati mwengine kutokana *experience* nimekwanda nimeona Tanga katika utandikaji wa nyaya za umeme pamoja na maeneo mengine. Kwa mfano, kuna maeneo mtu anajua kwamba hapa italipwa fidia basi anakuja mbio almuradi aambiwe kuwa naye amejenga aweze kupata kitu ambacho pengine chini ya kile yeye alichotumia.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuhusu suala la kukaa muda mrefu eneo linajulikana tutajenga barabara na ikawa limeachwa bila ya kuliwekea alama. Suala hili nilikuwa nikilipigia kelele siku zote kwamba ziwekwe alama na kuwe na matangazo maeneo haya kutoka sehemu fulani mpaka fulani hakuna ruhusa kujenga na kama mtu atajenga, basi serikali itakapopata uwezo wa kujenga barabara haitolipa fidia ya aina yoyote.

Kwa hiyo, hili halichukuliwi hatua ndio maana kunakuwa na *conflict* baina ya wananchi na serikali kuhusiana na masuala ya fidia. Kwa maana hiyo, masuala ya kuweka *reserved areas* kwa ajili ya barabara ni jambo muhimu. Mhe. Mwenyekiti namuomba sana Mhe. Waziri alitilie maanani suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika suala hili la barabara napenda niseme kidogo kuhusiana na kwenye jimbo lake Mhe. Waziri, kuna ahadi ya Mhe. Rais na hii niatakuwa nikimkumbusha kila siku na ninatamani kama angekuwa

ameshaifanya nikamsifu sana, lakini nimetembea mwenyewe na bado hajafanya kitu.

Kwa kweli kuna barabara ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar Mhe. Rais wa Zanzibar alitoa ahadi siku ya tarehe 22 Januari, 2009 na mwenyewe alikuwepo na aliulizwa kama kuna tatizo lolote, alisema hakuna na Mhe. Rais alisema lami na fedha zipo, basi barabara ya chuo itengenezwe. Mhe. Mwenyekiti, nasikitika sana kwamba muda wote mpaka hivi sasa na tukizingatia kuwa chuo kinazalisha na kusaidia uchumi wetu kwa kupitia Sekta ya Utalii bado tumeiacha. *(Makofi)*

Vile vile nadhani tungebeba hiyo dhima kwamba agizo la Rais lipewe uzito wake na wala tusifikirie kuwa amemaliza muda kwa hiyo afanye aondoke apishe wengine. Kwa kweli ningependa kwa barabara ile angekwenda kuifungua.

Mhe. Mwenyekiti, namsisitiza sana kabla hajaondoka kwa sababu ile haifiki nata nusu kilomita, yaani kabla hajaingia kwenye mchakato wa kura, pengine hivi sasa ameshakuwa kwenye nafasi nzuri, basi aitengeze zaidi hiyo nafasi iwe nzuri zaidi, kwa kweli hili ni eneo miongoni mwa jimbo lake na atakuwa amejifyagilia mwenyewe pia. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu napenda nizungumzie kuhusu Idara ya Anga. Kwa kweli hapa nipongeze sana suala zima la njia kama walivyosema wenzangu, kwa sababu muda umeshakuwa mkubwa na wengi wameshazungumza. Aidha suala zima la jengo jipya na tunaona kuna *process* ambazo zinaendelea pamoja na mambo mengine ambapo kama kamati tunajua kuliko wenzetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba kutoa ushauri kwa wizara na serikali kwa jumla iweke malengo zaidi, kwa sababu hivi sasa tumo katika kuimarisha Uwanja wa Ndege na tunaweka jengo jipya, lakini mbele tunalenga kitu gani.

Kwa hivyo, hapa ninalo ombi kwamba sasa tuangalie tusitengeneze uwanja wa ndege pamoja na majengo mazuri yakawepo ndani ya Zanzibar na *Inshaallah* litakuwa ni zuri kuliko yote katika *East Africa* na halafu tukategemea zitue ndege za watu. Kwa kweli ni vyema na sisi tuwe na Shirika letu la Ndege na inawezekana na hilo ni suala la kujipanga mapema, kwa sababu ukitaka kujenga unaanza kufikiria *plan* pamoja na mambo mengine.

Kutokana na hali hiyo, sisi kuanzia hivi sasa tuanza kufikiria suala hili pamoja na utaratibu wa kuwa na ndege zetu pia na za wenzetu zitatua. Lakini na sisi

wenyewe wakati wenzetu wanatua na ndege zao, basi waone kuna ndege zetu ambazo zenye kuonesha hawa ndio wenyeji wa maeneo haya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu Idara ya Leseni kwenye ukurasa wa 21 kipengele cha 51 naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

> Ukurasa wa 21 kipengele cha 51 kinachosema hivi:-
>
> > "Idara hii ina majukumu ya kusimamia usalama kwa watumiaji wote wa barabara kwa kuendesha shughuli za ukaguzi wa vyombo vya moto, usimamizi wa mafunzo ya udereva, upasishaji madereva na Walimu wa Skuli za Udereva.

Kwa kweli hapa nataka kusisitiza tu kwamba idara ichukue juhudi zaidi, kwa sababu inaonekana madereva wengi wanaoendesha vyombo vya moto hawaelewi hata hizo sheria za barabarani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri mimi nakaa Michenzani na wakati ninapokaa juu basi huiona *roundabout* yote, pale pahala pa kusimama kwa ajili ya kumpisha yule mtu ambaye tayari ameshaingia kwenye *roundabout* hawasimami. Kwa hivyo, wanajipima tu kwamba hapa nikiongeza *speed* kiasi fulani basi anakwenda zake moja kwa moja na ajali zinatokea wakati mwengine asubuhi watu wanakwenda makazini, inabidi kwanza wapelekane hospitali na mambo kama hayo.

Kwa hivyo, ninapenda idara pamoja na wizara ione kwamba yale maeneo ambapo mtu anatakiwa asimame kama hapa kwetu nje Barazani imeandika simama, basi tuchukue jitihada za kuona tunaandika. Lakini kwa upande wa askari wenye kusimama kwenye vituo vya dalala, basi wasimame kwenye maeneo haya na kwa wale wasiosimama ndio iwe wao na wala wasisibiriane kwenye matobo ya Michenzani, kwa sababu pale kuna umuhimu wa kulinda maisha ya watu zaidi, ingawa na maeneo mengine yapo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni kuhusu *Zebra Cross*. Kwa kweli hapa pia ninapenda askari wasimame pale, kwa sababu watu wanataka kupita lakini mtu anakwenda tu na wakati mwengine mtu anakaribia kugongwa, ambapo mtu tayari ameshaingia kwa ajili ya kukata barabara na watu wanakwenda na vyombo vyao.

Kwa hivyo, hali hii haileti picha nzuri na kuna haja ya watu kukumbushwa, lakini kwenye makumbusho pamoja na zile alama ziwepo na bado hazijafutika

na zile sehemu ambazo hazijawekwa basi ziwekwe kwa ajili ya kuokoa maisha ya watu.

Vile vile nizungumzie kidogo kuhusu Afisi ya Mrajis. Mhe. Mwenyekiti, afisi hii kwa kweli imejitahidi, lakini bado nataka nizungumzie kuhusu suala zima la utaratibu wa vyombo. Kwa mfano, kuna chombo ambacho vinajitahidi kama vile wenzetu wenye Boti ya Kilimanjaro, nafikiri ni *Sea Bus* pamoja na kwamba wameshawahi kupata mtikisiko, lakini bado wengi hawachukui hadhari katika kuchukua abiria.

Hata hivyo, ni bahati mbaya sana MV. Maendeleo imerudi juzi na imeanza kazi ambapo meli yetu ni nzuri na kila kitu. Lakini bado kuna kasoro nyingi na kasoro kubwa *life jackets* zimo kwenye vyombo tu sasa chochote kikitokea ni matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, tukiacha hilo pia kuna suala zima la kubaba wale abiria, yaani abiria wanaochukuliwa ni wengi sana, kwa sababu chombo kinachukua kuliko uwezo wake, ambapo hivi sasa tunasikia wachukuliwe abiria 400, lakini kuna askari wangu amefanyakazi ya kuhesabu na amepata abiria 670 badala ya 400.

Kwa hivyo, nadhani Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atatueleza kwamba hasa abiri wangapi ambao wanaotakiwa kuchukuliwa, lakini indhari ni bora kuliko kusubiri mpaka hatari ikatokezea. Mhe. Mwenyekiti, tunaomba sana usimamizi uwe wa hali ya juu katika upakiaji wa abiria kwenye vyombo, ili usalama uweze kupatikana basi tuhakikishe vifaa navyo vinapatikana na wala sio *life jackets* ziwekwe vyumbani, isipokuwa ziwekwa kwa mujibu wa idadi wa abiria watakaoingia kwenye vyombo vile.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kuzungumzia suala la minara miwili ya Kigomasha na Nungwi. Kwa kweli ule wa Kigomasha hauwaki na ule wa Nungwi unazibwa na *jetty* ambayo imejengwa kwenye Hoteli ya Nungwi kutokana na ule mnara wenyewe *original* ni mfupi. Sasa tatizo linakuja wakati meli inapokuja inakuwa haioni ile taa kwa Nungwi na Kigomasha taa mara inawaka na wakati mwengine haiwaki.

Kwa hivyo, masuala haya ya minara iko kwenye mambo ya kimataifa, basi wasi wasi wangu ni kwamba isijeikatokezea la kutokezea na nchi ikaingia kwenye matatizo na serikali ikaingia katika lawama. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri hili alichukue kwa hadhari ya juu kabisa, ili tusifikie katika kupata matatizo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru wewe kunipa nafasi hii kwa ajili ya kuchangia Hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi.

Vile vile nisifu juhudi zao ambazo imebadilisha sana Zanzibar kutoka zamani na kuwa Zanzibar ya leo. Kwa kweli Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi imepiga hatua kubwa sana kabisa za kupigiwa mfano. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunayo sababu ya kusifu kwa sababu tunatoka mbali tunajuana. Kwa mfano, huko ninakotoka mimi zamani gari ya kawaida ya maringi manne haifiki Matemwe kabla ya Mapinduzi, kwa hivyo kuna haja ya kusifu.

Sasa katika hali ya mabadiliko huko niliko Matemwe ndiko kunakosifa ya aina zote kwa mambo ya usafiri wa barabara, lakini maendeleo yakiwa mengi basi na hasara inatokea. Kwa mfano, hivi karibuni tu kulikuwa na Mashindano ya Msererekо wa Magari kwa bahati mbaya wakati wanaporudi wale wachezaji, kama tunavyojua ikiwa mmecheza vizuri mnarudi na hamu, basi papatu papatu wameipindua gari yangu ilikuwa na wachezaji mpira na karibu watu 40 waliumia na mwenyewe nimehudumia na wala sijawalalamikia, kwa sababu ukitaka uzuri unadhurika.

Pamoja na hayo, barabara nzuri naendelea kusifu, isipokuwa ninachosisitiza vibali vya kupuuzi kwa michezo mingine wizara lazima iwe na mkakati, kwa sababu sio wengi wanaopenda mchezo ule. Kwa hivyo, tunasifu juhudi za Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kwa bahati nzuri timu yake inafanyakazi vizuri na mtu humsifu ndugu yake, kwa sababu Katibu Mkuu ni ndugu yetu, Mkurugenzi Mipango pia ni ndugu yetu pamoja na wengine wengi ni ndugu zetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimepeleleza kitu kimoja sisi Wawakilishi tunapenda sana kulalamika na hatusifu. Kwa mfano, kwa upande wa wenzetu wa Upinzani ni wajumbe wawili tu ndio waliosifu na sijui wamepata nini, lakini waliobakia wote wanalalamika tu.

Kwa kweli hili si kwa Wawakilishi tu, ninakumbuka mnamo miaka ya 1980 au 1985 kama sikosei, wakati Baraza la Kwanza la Wawakilishi kuanza, walikuwa wanayo timu ya mpira kama sisi na walikuwa na wachezaji wao kama vile tunavyowafanya akina Dau Hamad Maulid. Sasa wale wawakilishi wakawa wanalaumu kwamba hamchezi vizuri na tunafungwa sana.

Kutokana na hali ile siku moja kocha alikasirika akaona awaingize wote wale Wajumbe wa baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kucheza mpira vizuri na

wapate sifa. Mhe. Mwenyekiti, kumbe ukiingia uwanjani na kucheza mpira ni tabu kweli ni tofauti na utizamaji.

Kwa hivyo, na sisi tuone kwamba serikali inapanga kwa kutegemea bajeti yake na wala Bajeti ya Zanzibar haiko kwenye kapu, isipokuwa inategemea yale mapato ambapo sisi pamoja na wengine kwa juhudi ya kuyaenga enga na kuyaenzi, ili yaingie kapuni na kuweza kufanya maendeleo. Hivyo, bado waheshimiwa tuendele kuomba katika majimbo yetu na tusimamie mpaka pale tuone matatizo yanapungua hasa ya usafiri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka kwenye utangulizi sasa nianza mchango wangu kwenye ukurasa wa 12 kwa sababu sina sehemu ya kuzunguka Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara. Kwa kweli kwanza naisifu na Mhe. Mjumbe ambye ni rafiki yangu amesema tubadilike, yaani UUB iwe na utaratibu kama ule ambao wanafanya wenzetu wa Tanzania Bara *TANROAD*.

Lakini utaratibu huu hapa upo kwa sisi ambao tunaishi vijijini tunaona, kwamba hivi sasa maeneo ya ukataji majani, kutengeneza mitaro au misingi pamoja na mambo mengine tayari hawa jamaa wanaifanya hiyo kazi, hivi sasa barabara zote hazina majani na safi sana. Mhe. Mwenyekiti, nafikiri hawa mawakala waliowachukua na kuwapa kazi, basi wanafanyakazi vizuri sana.

Kwa hivyo, ninachokiomba kwa idara hii ni kushughulikia mafao yao, kwa sababu wale nafikiri wanafanyakazi kwa kukatiana maeneo. Sasa hali hii inasemekana na wala sina uhakika, kwamba hao wasimamizi wa hivyo vipande wanavyowakatia hao wafanyakazi wanakuwa na tabu sana ya kuwapa fedha na wakati wanapowapa huwa sina kasoro. Hivyo, ili sifa hii iendelee basi wasimamie vizuri na wala wasionekane kwamba labda wanafanyakazi na malipo yao hawayapati, kwa sababu hii kazi watendaji wake ni wale wananchi wa vijijini. Mhe. Mwenyekiti, nadhani ni vyema kuwalipa vizuri kwa ajili ya kuwafanyiakazi nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa huo na mimi nisijekusahau yale ambayo mjumbe mwenzangu ameyazungumza. Mhe. Rais alikuja tarehe nimeisahau Muyuni Kijini, maana Kijini mwanzo na Muyuni kule chini, alimwita Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi siri pamoja na mimi ndani cha chumba ambacho kimetengenezwa vizuri katika hiyo skuli iliyofunguliwa.

Kutokana na hali aliyoiona ile barabara Mhe. Rais, basi alisema ifanyiwe matengenezo angalau iwe inapitika wakati serikali inaandaa mpango madhubuti wa kuijenga barabara hiyo, lakini hadi leo bora kwa mwenzangu Mhe. Said Khelef Ali analiona *dozer* pamoja na *grader* yamelala, nadhani yanawapa matumaini.

Mhe. Mwenyekiti, kule Kijini hata yale maelezo mazuri si kutoka kwa mtu au kitabuni ama pahala popote na siku ile ya maazigo alikuwepo Mkuu wa Wilaya pamoja na Mhe. Naibu Waziri. Kwa hivyo, mimi nina wasi wasi kwamba kauli ya Mhe. Rais wizara iliipuuza, sasa wakati anapokuja kufanya majumuisho Mhe. Waziri anieleze mambo mawili, Mhe. Naibu Waziri ameshindwa kazi au Mhe. Rais amewadanganya wananchi. Katika hayo mawili achague moja ambalo nitaweza kunisaidia kuwaambia wananchi. *(Kicheko/Makofi)*

Vile vile inaonekana wizara hii inapopanga mipango yake hajulikani mkubwa nani, kwa sababu haiwezekani Mhe. Rais ameshasema kwamba hapa wasaidieni angalau waweze kupita. Mhe. Mwenyekiti, jambo la kushangaza ni kuwa malighafi ya barabara kwa Kijini hasa kifusi, yaani hwendi hata kilomita mbili uchimbe na uweke pamoja na kushindia mambo yamekisha na wala haina gharama kubwa.

Sasa unapowaambia Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi wanasema fedha, lakini tunazo njia karibu tano za kupata fedha na wala hakuna hata moja ambayo imeelezwa kwenye kitabu hiki kwamba itawasaidia Kijini. Kwa mfano, kuna masuala ya kuiweka kwenye bajeti barabara ile haikutajwa, tunao Mfuko wa Barabara haioneshi, pia kuna Mfuko wa Rais, kuna Mfuko wa Miradi ya Wananchi, yaani haioneshi popote.

Mhe. Mwenyekiti, mwenzangu alisema kumbe kutangulia sikufika, kwa sababu barabara hii kwa muda mrefu inazungumziwa. Kwa kweli tumefika pahala pa mwenzangu alihoji kwamba kuna barabara ya kutoka kwa Mabata kwenda juu na siku zote inapigwa *grader* na wala huulizi fedha zake zinatoka Mfuko upi ama wa Rais, Mfuko wa Barabara, iko kwenye bajeti au inatoka wapi na kwa Mhe. Waziri sisemi, kwa sababu huwezi kupika bila ya kujibakishia.

Kwa hivyo, sehemu nyengine lazima tuulizane inakuwaje, wizara inakuwa vipi mpaka kufanya mambo ambayo wapo watu wanayataka kwa muda mrefu hayapatikani kwa wengine muda mdogo yakawezekana.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho, kwa nini barabara ya Kijini haifanyiwi hata matengenezo ya dharura na *grader* haipigiki kwa sababu jiwe lake gumu. Lakini tuangalie hata *dozer* haipigi, kwani malighafi ya kifusi ipo na wala haina masharti tena bila ya kuomba, yaani unaamua tu unachimba hapa au pale tena bila ya kuharibu mazingira.

Sasa naomba hili Mhe. Waziri anipatie maelezo mazuri, tena naamini anaweza kunijibu na anajiamini, kwa sababu waziri yeyote kwa hapa Zanzibar kama hajiamini basi kazi haifanyi, kwani inaweza kuwa nia anayo lakini akiambiwa

na huku bado na yeye anasema ndio huku bado. Kwa hiyo, lazima mawaziri mnatakiwa mujiamini na mnapotoa maamuzi yanakuwa maamuzi, nasema kuna mawaziri wanatoa maamuzi yao lakini hawajiamini na maamuzi yao nina ushahidi mmoja, unajua unapokuwa na kikao unajiwa na watu ambao wewe huwajui. Juzi kanijia mtu analalamika ananiuliza kama ninavyouliza Waziri na Mkurugenzi nani mwenye nguvu kwa pale nilimwambia waziri ana nguvu akanambia haiwezekani nikamwambia kwani wewe nani.

Akanambia mimi nina kampuni *Alkubra Marine Society* nimeomba kuingiza *crane* ndani ya Zanzibar nikakubaliwa kwa tarehe hiyo apo ambayo unaiona tarehe 25 April. 2010 akasema na jibu limeshatoka la Waziri kwa barua hii, lakini anashangaa mpaka leo hajabiwi kimya aliponiuliza mara ya tatu waziri na Mkurugenzi nani ana nguvu nilimwambia Mkurugenzi ana nguvu. Haiwezekani waziri aliyeaminika ana maamuzi keshatoa maamuzi kwa maandishi haya hapa baadae Mkurugenzi akawa na nguvu itakuwa ndio ile bado hujiamini.

Kwa hivyo hilo nilikuwa natoa mfano lakini sio mfano lazima tuonyeshe kwamba waziri ana mamlaka aliyopewa makubwa kuliko Mkurugenzi, wote wameteuliwa naomba nifahamike wote wameteuliwa lakini wanapishana, kwa hivyo Mhe. Waziri Kijini kule siwezi kuzuia shilingi najua atatengeneza lakini kwa hapa ili nikupe nguvu wewe na ujiamini basi lazima hapa unipe maelezo. Kwamba barua yako itaheshimika au haiheshimiki.

Mhe. Mwenyekiti, sisi wengine utangulizi wetu unakuwa mkubwa sasa bora niamini kwamba wanaikubali wakati nimeitaja barabara ya Kijini na nimesifu juhudi za wizara, nasema bado sina matatizo baaada ya kupata majibu tu kwamba barabara ya Kijini tu hata kwa msaada itasaidiwa, lakini hata hivyo na hiyo kampuni ya *Alkubra Marine Society*, basi naunga mkono mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wa Jimbo la Matemwe mia kwa mia na nakushukuru sana Mwenyekiti maana nafikiri leo sipati. *(Makofi)*

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Menyekiti nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi, kwanza mimi nataka nimpongeze Rais wa Zanzibar Dk. Amani Abeid Amani Karume ni rais pekee ambae amejikita kwenye miundo mbinu ya barabara na ametekeleza zaidi ya nusu ya yale ambayo ameahidi, hili halitaki tochi barabara nyingi kweli zimejengwa na barabara hizi ndizo ambazo zimesukuma sekta ya utalii katika Zanzibar hii. Muda aliobakia sio mrefu lakini kwa kuzingatia hayo nilikuwa namuomba Mhe. Waziri wa Wizara hii jadweli au kiambatisho namba moja ambacho naomba nikisome.

Kiambatisho hiki kinasema kwamba. Kipo page 58 kinasema "*Barabara zilizojengwa katika kipindi cha Mhe.Dk. Aman Abeid Aman Karume".*

Wenzangu wamelisemea hili na mimi naomba nilisemee lakini kwa ufafanuzi zaidi mimi ningeomba kwa sababu hii ni hotuba na haya ni maandishi, leo hii akija mtu akikwambia twende Kipangani Kangagani akenda kuona hiyo barabara iliyojengwa wakati wa Mhe. Amani Abeid Karume haipo, sasa mimi nilitaka jadweli hii au kiambatisho hiki akigawe katika mafungu matatu kwa usahihi na hiyo *heading* barabara zilizojengwa, jamani zilizojengwa ni *past tense* zishajengwa hizi na tukisema kujenga tunaamini kwa sababu tunajua, sasa kama zilizojengwa hapa kuna barabara nyingi hazijajengwa.

Ama iandikwe hivi barabara zilizojengwa mkwaju au koma, zinazoendelea kujengwa na zinazotarajiwa kujengwa hii jaduweli hii ndio itakuwa sahihi kwa maana ya kwamba wataalam mbali mbali walishiriki katika kuitayarisha bajeti hii na kuisoma nina hakika Waziri mwenyewe kabla ya kuletwa hapa ameisoma mara tatu au mara nne, hilo la kwanza.

Lakini la pili nataka niende haraka haraka Mhe. Zainabu Omar Moh'd alizungumzia kuhusu *Road reserve* jamani lazima tujifunze, sasa hivi serikali inalipa fidia vitu ambavyo vingefanyiwa marekebisho mapema havikufanyiwa marekebisaho, ilizungumzwa hapa njia ya Mfenesini Bubwini gharama za kuondoa mabomba kwenye kamati tumeambiwa ni milioni mia nne, *contractor kuna bulldozer* pale na *grade* lakini anasema niingie nisiingie akiingia mabomba yanafyetuka mtu wa Bubwini hapati tena maji. Lakini mimi naamini kabisa ingekuwa kuna *Road reserve* ni ile barabara yenyewe lakini kuliani na kushotoni kuna eneo la kutosha kwa ajili ya *services* ya maji, umeme, gesi, simu hata redio umeona barabara ya Masingini ilivyoleta tabu kuna mkonga kutoka kule kuelekea hapa, barabara ile ya Amani Dunga inataka kutanuliwa sasa, mkonga unatoka hapa kwenda Masingini kwenye Mtambo wa Redio pale lazima ung'olewe au *centre line* ibadilishwe ni gharama nyengine mpya kabisa hizo.

Sasa mimi naamini kabisa ingekuwa mambo haya yameangaliwa mapema basi tusingegharimika kiasi hiki, sasa watu wa barabara wapo haya ndio mambo ya kutafakari ukienda kule barabara kama unasafiri kutoka kokote kule utakuta barabara ipo, lakini kwa ndani karibu mita tatu kuna kialama kimewekwa kwamba wewe utakayekuja kujenga angalia kwamba hii ndio mipaka yetu tena ni alama za kudumu sio guzo la kuweka halafu mtu akaling'oa. Mimi nafikiri ni wakati hii Zanzibar ni nchi tunaendelea kama wenzetu ni wakati sasa hivi kila barabara inayotaka kujengwa hizo za Ole/Konde, Ole/Kengeja utaratibu huu uwekwe mapema, leo isijekuwa tumejenga laini moja ya Ole/Kengeja maendeleo yanakuja hayo serikali mpya inakuja hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya miaka mitano usije ukashangaa kwamba badala ya lami moja kukawa na lami mbili sasa kama hukuweka *Road reserve* utaipata wapi ya pili, utabomoa tena majumba ya watu kama alivyosema Mhe. Said Ali Mbarouk jumba kubwa kama hili linavunjwa ukuta wa mbele unaambiwa ndio tumeshavunja apo, yule aliyebakia kwenye chumba cha kulala akitema mate basi anaitemea gari inayopita nje. Mimi ninasisitiza kwamba suala la *design* ya barabara ukichukulia *Criteria* zote basi ziangaliwe kwa sababu tunakwenda na wakati.

Mhe. Mwenyekiti nimepata taarifa nzuri kwamba ile ahadi ya muwekezaji mmoja *Azam Marin* ya kuleta meli, meli imeshafika meli mpya inaitwa Kilimanjaro II kama hivyo, ahadi ya muwekezaji huyu kwenye Kamati ni kwamba meli hii itafanya shughuli zake nyingi sana kati ya Unguja na Pemba yaani huyu ni muokozi mwengine, sasa Mhe. Waziri na watendaji wako kama meli imeshafika fanyeni *process* zenu kama ni kuijaribu lakini aiaze kazi haraka. Na tunaomba kwamba kama ni muokozi wa usafiri wa Pemba na Unguja basi awe muokozi kweli hatutaki kumpangia bei lakini asije akapanga bei kwa sababu ya upya wa meli tena iwe mtu anadoda tu anataka kupanda meli lakini haipandiki, itakuwa yale malengo yake na nia yake haitawezekana watu bado wataendelea kupanda madau, kupanda majahazi kumbe meli nzuri mpya ipo.

Kwa hivyo hizi ni habari za faraja tunamshukuru na vile vile na wengine waige, lakini wanaosafiri kuja Dar es Salaam kuja huku *Azam Marine* huyo huyo amejenga *terminal* moja nzuri sana pale safi kabisa kwa ajili ya meli zake tu, nasema hilo halina ubaya wowote kila mtu anajaribu kutengeneza shughuli zake za biashara amejenga pale kila mtu anajua unaingia pale ukishakuwa na tiketi ake tu kahawa bure, juice bure, maji bure vitu kama hivyo na unaingia kwenye AC unaomba lile boti lichelewe. Kuna watu wanakata tiketi ya boti ya saa kumi wanaingia pale tokea saa nne na hawatoki, sasa mimi nasema hii sio faraja mbaya.

Mhe. Waziri tuna taarifa kwamba Mmiliki wa *Azam Marine* alitaka kufanya kitu kama hicho hapa Unguja bandari hii lakini kukawa na vikwazo kwamba afanye lakini itumike na kwa wawekezaji wengine hili mimi nafikiri lisiwe ni sharti jamani, amefanya mwenyewe kwa gharama zake serikali imempa nafasi kila mtu ana haki yake, sasa na yeye aachiwe afanye. *Investment* anayejenga kwenye ardhi yetu na kwenye bandari yetu na kama wengine wanataka kufanya waendelee kufanya lakini sharti kwamba lazima ashirikiane na wengine katika jengo lake lile mimi nafikiri hili lingeangaliwa upya, na sisi kupata *terminal* kama ile nafikiri dada yangu Mhe. Waziri wa Utalii na Uwekezaji atakwenda kama aliyekuwa na joho hivi ni vitu vinavyoonekana wazi sifa inakwenda kila pahali.

Sasa hivi kila mtu anasema umeona Dar es Salaam ilivyojengwa na hapa tuigeni jamani hili sio jambo baya, serikali haigharamiki chochote zaidi ya idhini na pengine kuangalia tu hicho kinachofanyika ni hicho kilichokusudiwa, hili nilikuwa nataka niliweke wazi na hatua zichukuliwe tena haraka kabla ya kura ya maoni haijaanza *(Kicheko).*

Mhe. Mwenyekiti, Waziri katika jadweli alikuwa anatuonyesha ndege ambazo zimekuwa zikitua katika uwanja wa ndege wa Zanzibar, lakini kuna baadhi ya *Airline* sikuziona sasa sijui imekuwaje. *Zan Air* imo kuna jadweli hapa namba 9 jina la ndege yaani kampuni za ndege zinazotumia viwanja vya ndege vya Zanzibar kwa mwaka 2009/2010. Kuna ndege moja maarufu sana hapa siioni *Indigo* lakini vile vile *Tropical* wanaita *Air* Makunduchi kama hivi, *Air Kajengwa*. Ilikuja ndege moja ukiingia tu unachagua unataka korosho, unataka juice, unataka maji ikawa watu wote wanakimbilia. Sasa hizi sikuziona sijui kompyuta kama alivyosema Professar Ali Denge imeruka au imerukishwa.

Mhe. Mwenyekiti mimi kama mjumbe wa Kamati taarifa niliyokuwa nayo ni kwamba *New terminal* jengo jipya la uwanja wa ndege litakalojengwa linajengwa na rafiki zetu wa kudumu Serikali ya China na ni msaada, hata hivi karibuni katika vyombo vya habari wakati wanatiliana saini basi msaada huu ulikuwa bara na Zanzibar hizi ni habari nzuri, mimi natahadharisha sana kwamba siku hizi kila kitu ni *modern technology* msaada huu tunaukaribisha tena umechelewa. Lakini ninachoomba ni kwamba wizara inayohusika na mambo haya wawe na hadhari sana isiwe tumepewa msaada tena sisi tumepewa tu, kuna rafiki yangu mmoja alinambia kwamba mtu anaweza kukupa msaada akakwambia basi nakufungia hili bomba la kutangazia *Air Port* pale wanaosafiri kwenda Tanga basi wanaingia geti namba ngapi, lakini msaada ule ile betri yake ni bei ya lile bomba ulilopewa bure mara saba.

Msaada huo tunaopewa ni mzuri tunaupenda lakini *technology* ya siku hizi kila siku inaendelea katika *instillations* ya vitu vitakavyowekwa mle lazima tuwe makini sana, tusijekuwa kwa sababu ya msaada tukapewa vitu vya siku tatu lakini ukitaka kuvitengeneza vikakushinda, ama ukaving'oa ukatafuta vipya au ukaacha hapa pamoja na kwamba kuna *internet ya Airport* basi wasafiri kwenye *departure* kama hukuwa makini unaweza kujitia kwa mwenye kahawa pale ndani, ukifanya mchezo unashtukia ndege imeshaondoka huna habari maana yake unaitwa tu hivi watu wa Tanga, jamani *international Airport* sio mchezo hivyo. *(Kicheko)*

Mhe. Mwenyekiti nyie si mnasafiri kila siku sasa ile kofi kama hukuisikia au watu wa Tanga na pale pana zogo wewe unakunywa kahawa huku ndege imeshaondoka unalaumiwe wewe kumbe lawama ziko kwenye *system* za *Airport.* Mhe. Waziri hayo ni mambo mdogo sana lakini kasoro yake ni kubwa

mno mtu ameshatoka hoteli kashafika na mizigo yake na pengine hiyo mizigo imeshaingia kwenye ndege anakosa ndege kwa sababu hakuna matangazo anayosikia, *this is very serious* siku moja nilisema hapa, jamani hii haijakuwa *International Airport* labda kwa jina lakini si uhalisia wa mambo. Nikatoa mfano kuna mtalii mmoja yupo *departure* kwenye kukalia viti vile masikini ya mungu msumari skuruu wanajua hao wenyewe, yeye anakaa pale yeye anajua ni kiti tu kukaa msumari ukamtoboa ndio *Aiport* hiyo hiyo ya Zanzibar.

Baada ya kutokea tokeo lile ndio kuwa na shauri la kubadilisha viti *International Airport* wakati huo hata vyoo havipo nyie mashahidi wapi jamani, watu wanatoka mahotelini huko ameshakula samaki aliyeoza anafika pale tumbo linambirua anakwenda wapi, sasa vitu vidogo kama hivi jamani ama kweli jina sio hoja. Ndio *International Airport* jamani lazima ufanye *hundred percent* lakini angalau zifanane ni vitu vidogo vidogo kama hivi vinakuangusha sana, maana yake sisi tunakujua wewe tu wewe tena unawajua watendaji wako huko.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui amesema kwamba uwanja wetu wa ndege umetengenezwa ki- *International standard* una urefu wa kutosha, mambo ya *tax way*, mambo ya *packing* ukipita kule juu unaweza kusema uwanja ambao haujatumika hata siku moja, sasa mambo madogo madogo kama haya yasitufukuzie wateja *income* inayopatikana pale Uwanja wa Ndege mkiambiwa hapa mtashangaa.

Mhe. Mwenyekiti. Mhe. mjumbe muda umekwisha.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Muda umekwisha Mhe. Mwenyekiti, basi la mwisho Mhe. Mwenyekiti, mimi kama ni mjumbe wa kamati nimeshuhudia kitu ambacho sikipendi hata kidogo tatizo la mkandarasi wa barabara za serikali, tumekuta kesi mwenyekiti wangu shahidi *engineer* wa serikali na *engineer* wa Mecco kila mtu ana ujuzi wake hawa tumekuta hawaivi pamoja mpaka mwenyekiti akauliza kulikoni. Kuna mtu kamchukulia mwenzake huyu afisini kwa fulani haendi na huyu akienda huku huyu anakimbia sasa tutakwenda vipi namna hii, ndio maana saa nyengine hizi kazi za barabara zinakuwa zinapitwa na wakati kwa sababu utengenezaji wa barabara ni muda. Sasa kama leo *engineer* huyu na huyu hawakai pamoja na ukiangalia kosa la nani unajua kosa la fulani lakini hataki kukubali kwamba kosa lake.

Mhe. Mwenyekiti katika hili mimi nasema serikali tuwe makini sana vitu vidogo vidogo hivi visitupe kiburi kwamba sisi ni serikali, kumbe ungeliweza kusema tu mfanye hivi lingelifanywa gharama hatimai inakuwa kwa serikali. Baada ya kusema hayo japo kuwa nina mengi lakini nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Ali Moh'd Bakari: Mhe. Mwenyekiti na mimi nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi kutoa machache kwa muda ambao upo, kwanza niseme kwamba wizara hii kwa ujumla wake ina jukumu la kusimamia usawa wa maendeleo au miundo mbinu katika nchi ambayo hatimae italeta maendeleo, au italeta nafuu kwa wananchi kwa shughuli zao mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti ukiangalia suala hili la mawasiliano ya barabara hapa Unguja unakuta barabara nyingi ambazo zimeshajengwa na nyengine zinaendelea kujengwa, kule Pemba kuna ahadi ya barabara nyingi ambazo sasa hivi zinaendelea au ziko njiani kutaka kujengwa. Sasa ili tuseme usawa na nchi imeendelea basi ni lazima katika maeneo yote ya nchi kuwe na usawa wa mambo mbali mbali ili mtu mwengine anapokuja awe mgeni au mwenyeji akute kilichopo hapa na kule ndicho kilichoko na kilichopo kule na hapa ndio kilichopo, hapo ndipo unapoweza kuona usawa ama maendeleo ya nchi yamefikiwa katika hatua fulani.

Mhe. Mwenyekiti karibuni tulisafiri pamoja na wewe mwenyewe binafsi tukenda nchi ya mbali huko lakini tulipofika kule wewe mwenyewe binafsi uliona ni kiasi gani mpaka kule vijijini, yale ambayo yako mijini na vijijini kule yapo, sasa katika kuiendeleza nchi watu hawaangalii wafanye kitu gani kila kitu kinahitajika hata kama kuna watu wanne bado wanahitaji yale yale yaliyoko mjini kwa hivyo na wao wanafanyiwa. Kwa hivyo katika kuyafanya haya Mhe. Mwenyekiti, lazima Mhe. Waziri aone kwamba na sisi kule kwetu tunapokuwa tunakuja hapa barazani tunalalamika juu ya mambo fulani aone kwamba ni haki yetu kulalamika, hatulalamiki kwa sababu ya choyo lakini tunalalamika kwa sababu ni haki yetu na sisi tunataka tufanyiwe kama yale ili na sisi tujikwamua katika hali fulani tuliyokuwa nayo.

Mhe. Mwenyekiti mfano wa hizi barabara tatu za Pemba huu mradi labda kabla yeye hajakuwa waziri au hata muwakilishi ilikuwa suala hili lipo nashukuru alhamdulillahi kwamba sasa hivi linashughulikiwa na yeye akiwa waziri, lakini bado kuna msururu mkubwa mno sisi kule kwetu tuna matatizo, ukitoka pale Konde kama unakuja Wete ni mwendo wa dakika kumi na tano. Lakini unachukua karibuni masaa mawili hujafika kutokana na ule ubovu wa barabara, sasa hivi barabara imekwenda kuchimbuliwa mpaka leo kukinyesha mvua inaachwa sasa hii ni kuonyesha kwamba hata kama jitihada zipo lakini bado sio za makusudi ni hali ya kuridhishwa tu.

Mhe. Mwenyekiti mimi natoka Pemba kwa hivyo nataka yale yaliyopo hapa Unguja na Pemba yafanywe katika maeneo yote, Mkoani kuna matatizo ya barabara na sisi tunakwenda mimi nimezaliwa Tumbe kule lakini nakwenda Mkoani kuna jamaa zangu na marafiki zangu nikifika nakuta kuna matatizo ya barabara, pahala ambapo nilikuwa nakwenda kwa dakika tano nachukua zaidi

ya saa moja na mtu mwengine anapotoka Mkoani kuja kwetu anapata shida. Sasa naomba Mhe. Waziri kwamba barabara zetu za Pemba zote ambazo zimepangwa kushughulikiwa afanye jitihada ahakikishe kwamba anazishughulikia kila eneo tuna matatizo yanayofanana, kwa mantiki hii na sisi tunataka tupate usawa wa barabara na Mawasiliano kama wenzetu wa Unguja, kwanza kule sisi barabara zetu ni fupi sana.

Mhe. Waziri kama atajipanga vizuri yeye na watendaji wake ili akahakikisha zile barabara leo Mhe. Moh'd Ali Salim kasema mambo makubwa, mwisho kamalizia kwa kusema mimi sipo tena hapa ndani kwa sababu sikuchukua fomu lakini anaweza kuja mtu mzuri zaidi kuliko mimi, sasa akija mtu wa aina hiyo sawa lakini akija mbaya zaidi kuliko yeye itakuwa ile barabara inakaa sasa ibakie huruma zenu sababu yeye anapiga kelele lakini si kila mtu atakuwa kama yeye, anaweza kuja mzuri kweli kweli zaidi ya yeye lakini akija mbaya je.

Mhe. Waziri kwa kuwa wewe ni mwenzetu na hiki kitabu chako umekitengeneza vizuri kutekeleza ilani yako ya chama chako, sasa basi na hizi barabara zitengeneze kama ulivyokiremba kitabu chako ili na sisi tuone tunafanyiwa hakim na kule.

Mhe. Mwenyekiti kule kwetu kama jimbo langu mimi kuna vijiji ambavyo gari hazifiki kule kun watu watapata ujauzito watataka kujifungua na kutoka pale Shumba kwenda Micheweni inapelekea wakati mwengine mtu kujifungua kwenye mikorosho, kwa sababu ya barabara ni mbovu na hakuna kabisa barabara labda Mchangamdogo. Kwahivyo nakuomba suala hili la mradi wa barabara katika yale maeneo yetu basi atutilie fusi angalau yakitokea haya mtu aweze kujihami asipate muadhara, unajua kujifungua kwenye mikorosho ni tatizo nalo saa nyengine mkunga yupo lakini taimu nyengine unapelekwa na baba yako utajifungua vipi. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri hili jambo atusaidie kwa sababu ni matatizo makubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, idara ya usafiri na leseni idara hii imepiga hatua sana na inafanya kazi kwa uadilifu na uangalifu sana, lakini mimi ninachotaka kushauri kuhusu idara hii Mhe. Mwenyekiti waangalie hizi skuli zinazofundisha vijana sasa hivi wanafundisha watoto wadogo mno magari ambao miaka yao ni midogo, saa nyengine unakuta kapakia familia yake nzima yuko barabarani na ameshapata leseni. Sasa mimi naomba kuwe na viwango vya mtu kupata leseni hata kama anachukua gari kafundishwa kule kwao ipo lakini na miaka lazima iangaliwe, mtu anaweza kusabibisha ajali halafu wakalaumiwa mpaka watu wa leseni kumbe hawana makosa kwa sababu wao wanataka mtu anayejua gari lakini na viwango vya kuamini kwamba ameshafikia umri wa miaka ya kupata leseni pia ni muhimu sana kuangaliwa.

Kwa sababu kesho na keshokutwa utakuja kujibu masuala ambayo hayana msingi wowote kuyajibu hapa ndani, lakini tatizo likitokea basi utalazimika ulijibu kwa hivyo mimi nadhani hatua za tahadhari juu ya jambo hili lichukuliwe sana ili kuepusha matatizo.

Mhe. Mwenyekiti nataka niingie kwenye Shirika la Meli, meli ya Mapinduzi imeuzwa na serikali ina wajibu wa kuhakikisha kwamba inapata usafiri, huu usafiri wote uliokuwepo ni wa watu binafsi. Mhe. Mwenyekiti hapa karibuni hawa wenye daladala waligoma tu kwa sababu ya kuongezwa pesa kiasi fulani serikali ikakataa wao wakagoma, ulikuwa ni mgomo mkubwa mno. Sasa mfano huo huo lazima uchukuliwe kwa vyombo vyengine vya usafiri ambavyo vya watu binafsi mtu ambae ana chombo chake sawa sawa na mungu na viumbe wake anaweza kufanya lolote wakati wowote anaotaka mwenyewe, akiona kwamba jambo fulani hakuridhika nalo lakini na serikali imeamua labda imeamuamua afanye hivi kwa maelekezo ya serikali kwa sababu ya wananchi wake, akikataa inamaana pale kitakachotokea ni mgongano baina ya yeye serikali na vyombo vyake, lakini atakayeathirika na mwananchi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Shirika la Meli lijitahidi kupata meli za serikali ili kutoa huduma za usafiri kwa sababu watu vyombo vyao kila wanalolifanya wanafanya mambo kwa kuzingatia maslahi yao, hawafanyi mambo kwa kumfurahisha mtu. Nchi zetu hizi kama alivyosema Dokta Subeti ni nchi za visiwa lazima tuzingatie hilo, serikali nayo inakuwa na uwangalifu juu ya jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, ikishakuwa serikali hii meli hata moja hawana, ndege hatuna lakini hata utovu wa meli, watu binafsi wana meli mabovu hapo, serikali nzima ishidwe kupata meli bovu ikahudumikia watu, kwa kweli hili ni tatizo. Mimi nadhani mameli kama yale yaliyokuwa yanawahudumikia watu yamo, serikali inaweza kuyapata. Kwa hiyo serikali iyangalie kwamba ipo haja ya serikali kupata meli ili iweze kuhudumikia wananchi wake ndani ya visiwa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kitu kimoja pale kwenye Shirika la Bandari juzi kiliniathiri sana. Kwanza nataka nisifu utendaji mzima wa Waziri na watendaji wake wote katika wizara yake. Kwa kweli wanafanyaka kazi kwa uangalifu. Na popote pale penye uzuri basi na dosari haziwezi kukosekana hata kidogo, lazima na athari zipatekane. Hii ndio sifa ya binadamu, hapawezi kuwa na uvuri mtupu peke yake pakawa hapana kasoro ndogo ndogo. Mimi naamini kasoro ndogo ndogo zipo ni kiasi kurekebisha mambo ili kusudi tukapata hayo tunayoyatarajia.

Mhe. Mwenyekiti, pale Bandarini mimi unajua nimezaliwa na ndugu yangu pacha ambaye tumefanana sana, kiasi kwamba kama hutujui huwezi kujua Ali ni yupi na Abuu ni yupi. Sasa juzi tulikuwa tunakwenda kule Bandarini lakini kila mmoja anagari yake. Tulipofika pale akanambia mimi nataka niingize gari yangu ndani kule akaniuliza nitaweza. Nikamwambia ukifika pale wewe sima ni sheha wa Bububu. Tulipo pale yule ndugu yangu yeye *branch* Meneja wa *Barclay Bank* lakini kava miwani kama mimi na kila kitu kama mimi. Alivyofika pale akamuona mlinzi katia rungu kama wale askari wa kijapani, alipofika akateremka kwenye gari anajiamini kabisa. Akamwambia mimi nataka niingize gari yangu akamuuliza wewe nani kwani. Akamwambia mimi sheha wa Bububu akamwambia ingia, hapa hapo alipomwambia ni sheha tu akamfungulia mlango akaingia.

Mhe. Mwenyekiti, sasa angalia tokeo lililotokea. Mimi nilikwenda akanambia aah! Bona kuna mtu kaingia kama wewe. Nikamwambia mimi siye si unaona nguo tofauti. Akenda akamwangalia akamuona kweli yule ni mwengine.. Akaniuliza kwani wewe unasemaje. Nikamwambia nataka kuingiza gari yangu. Akanambia si yule sheha kaingia, kwa nini usiingie na wewe ndani. Nikamwambia mimi ni Mwakilishi. Akanambia gari yako haina stika. Mimi nikaachwa nje. Sasa hebu angalieni eti Sheha tena wa kujibandikiza yeye kaingizwa ndani mimi Mwakilishi niko humu ndani nawawakilisha watu sikuingia, hili ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, nilifanya hivi makusudi kwa sababu siku moja nilikwenda pale nikazuiliwa. Kwa hivyo nikamwambia ndugu yangu wewe jitambulishe kwamba wewe ni Sheha na yeye akafanikiwa kuingia kwa usheha wa kujibandikiza. Mimi mwakilishi wa kweli sikuingia. Nawaombeni wahusika wa Shirika la Bandari hili jambo liangalieni kwa sababu tunadhalilishwa, tunaadhiriwa. Sisi wengine wakati mwengine tunavichaa tunaweza tukajibu maneno tukaambiwa Mwakilishi fulani kashafanya hivi keshafanya hivi. Kwa hivyo ni lazima *status* zitu tupewe.

Na hii inaonesha kwamba nchi hii kwenye hizi *entry front* wanaothaminiwa ni Masheha. Sisi hata tukwenda sehemu gani, tumeshakwenda mimi na Mhe. Subeti na Mhe. Omar Ali Shehe na Mhe. Omar Ali Dadi tukaenda pale, tukadhalilishwa, tulikuwa tunasefiri mara moja tunakwenda Pemba, tukadhalilishwa sana. Mimi nadhani mambo haya ni mambo ya kuyarekebisha sana. Sheha mpeni *status* yake na sisi tupeni *status* zetu. Kwa sababu kila mmoja anahaki yake sasa ikiwa sheha ni bora katika nchi hii sawa na awe bora lakini na sisi tunazo haki zetu.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba huu uimarishaji wa Bandari ya Mkoani kama walivyosema wenzangu wengi mimi nasema kama alivyosema Mhe.

Mnadhimu wangu kwamba bandari hii ilikuwa itangazwe kwamba ni bandari ya Kimataifa baad ya kukamilika kwake. Mimi nadhani Mhe. Waziri naomba simamia hilo zile kasoro ambazo wenzengu wamezitaja ziondoshwe. Kwa kweli bwawa lipo na siku za mvua pale hakuna raha. Isije ikatangazwa kwamba ni Bandari ya Kimataifa kwa sababu ya lile bwawa pale. Itangazwe kwamba ni bandari ya kimataifa kwa maana ya uzuri na mazingira yake.

Mhe. Waziri pamoja na imani yako na watendaji wako nakuomba nilishuhulikie jambo hili ili kusudi haya malalamiko madogo madogo yawe hayapo. Si vizuri kila siku watu wazima tuwe tunakuja kuongeza suala la Bandari ya Mkoani haipendezi hata kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na muda wako nasema ahsante sana. Naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti na mimi nashukuru sana kupata nafasi hii ya dakika za mwisho. Katika michango yangu nitachangia kwa ufupi ufupi sana kutokana na wakati.

Kwanza nashukuru Mhe. Waziri katika utangulizi wa kitabu chake kampa haki yake Mhe. Rais wetu wa Zanzibar Dokta Amani Abeid Karume kwa kazi kubwa aliyoifanya wakati akiwa yupo katika Wizara ya Mawasiliano baada ya kupata huu Urais na anavyoendelea. Hilo ni kweli isipokuwa tu baadhi ya mwahala kidogo Mhe. Waziri alikuwa aeleze hali halisi ilivyo, lakini kwa bahati mbaya hakujaaliwa nipata wakati nitaeleza.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana uchache wa wakati naomba kuanzia katika Shirika la Bandari. Mhe. Waziri katika maelezo ya kitabu chake amesema kuwa wizara imeweze kukamilisha mradi wa miundombinu ya Bandari ya Malindi na pia utanusi wa Bandari ya Wete na ujenzi wa Bandari ya Weshe.

Kwa ufupi ni kuwa Bandari ya Malindi ndiyo bandari yetu tegemeze na ndiyo Bandari Kuu katika visiwa hivi vya Unguja na Pemba. Ili bandari ifanye kazi yake kwa ufanisi kabisa kama ingelikuwa kweli miundombinu ilimeshakamilika kama Mhe. Waziri alivyoeleza ingelikuwa afadhali. Kwa fikra zangu naona bado kuna mambo katika bandari hii yanahitaji kuongezwa.

Kwanza ni lazima kuwe na banda lakini katika kitabu chake kaeleza tu kwamba litajengwa hapo fedha itakapopatikana. Shida tuliyokuwa nayo pale tunaona wananchi wetu wanapata tabu sana katika kusafiri kutokana kuwa hakuna banda hasa upande wa Bandari Kuu. Namuomba Mheshimiwa kwa vyovyote vile badala ya kuweka fedha itakapopatikana lakini atafute namna ya kuona

kuwa lile banda limejengwa angalau iwe na hadhi kibanda kama ilivyo bandari ya Mkoani na Wete.

Jambo jengine ili shughuli za ufanisi ziendelee vizuri nakumbuka nilipokuwa katika kamati ya PAC nilipopitia katika Bandari ile tulielezwa mara tu baada ya ujenzi wa ile gati kumalizika, shirika lilikuwa na mpango wa kujenga jet upande huu wa majahazi mpaka itokee kule ili zile meli za abiria na mizigo zinazoingia zipitie kwenye gati hiyo badala ya kwenda pale ambapo panakuwa na makontena. Ule mpango pia naona bado sikauwona. Nilitaka kujua kama kweli Wizara au shirika lina mpango ule au ndio umefutika.

Katika Bandari ya Malindi ili kuimarika zaidi ni pamoja na huduma za chelezo kwa sababu yanayokuja pale ni mameli. Chelezo kipo lakini tumeambiwa kitarefushwa mpaka kina kikubwa cha maji ili hata meli kubwa ziweze kuingia. Wakati huo Shirika limeahidi kupeleka wakati wake katika masomo ili matengezo zaidi ya uwezo wa sasa uweze kuongezeka. Lakini sijaona hatua yoyote.

Bandari ya Wete Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyoijua tumeambiwa imemaliza utanuzi. Bandari ile tunaijua historia yake baada ya kujengwa tu ilikuwa na tuta kubwa sana. Tuta lilipozibwa ikanyanyuka juu sana, mpaka sasa hivi inatisha. Tunavyoona mpaka sasa hivi gari zinavyoingia sivyo zinapotokea kutokana na kuwa bado gati ni nyembamba. Kwa hivyo kwa makusudi namuomba Mhe. Waziri, gati ya Wete ni gati inayotumika sana na sote tunafahamu hilo, isipokuwa bado haijawa ya kutoa huduma kwa masaa 24 irefushwe mpaka kina cha maji ambapo meli zinaweza zikakaa wakati wote na zikafanya shughuli zake. Ifanywe kuliko hali ilivyo hivi sasa, kuwa meli ikifika inapewa watu wanatoa mizigo yao na haiyondoki mpaka maji yajaye ili iyelee. Naomba hii gati ishuhulikiwe kikamilifu iwe inafanya kazi masaa 24. Upanuzi ule mimi binafsi naona haujawa wa kutosheleza. Iko haja ya ile gati kuangaliwe katika hali nyengjne ya muundo ili iweze kutoa huduma zaidi kwa maslahi ya wasafiri wetu pamoja na maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nina hakika amepokea taarifa nyingi sana za malalamiko ya wananchi kuwa ile gati inataka iongezwe lakini bado hakujawa na taarifa yoyote. Basi sijui kama wale wananchi watakuwa tayari hata wao kutoa michango yao kwa kuona matengenezo haya yanafanywa. Mheshimiwa atatushauri vipi kuwa atakubali na hilo kwamba atatoa mchango wake au tusubiri mpaka serikali itakapopata msaada.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuhusu Bandari hii hii ya Malindi. Hii Kampuni ambayo mwenzangu Mhe. Ame Mati Wadi ameizungumza *Marine Services* hii ina meli tatu na meli hizi zinasafiri Zanzibar/Dar-es-Salaam/Tanga na Pemba

inachukua mizigo na abiria inasaidia sana. Hii Kampuni kwa makusudi ili kuimarisha shughuli ya Bandari yetu kubwa ndio waliomba kuleta *crane* yao, barua ilifika serikalini ikamfika Mhe. Waziri au mtendaji wake mkuu na Mhe. Mkurugenzi wa Bandari akajibiwa kuwa serikali haina matatizo ichukuliwe hatua. Lakini nasikia mpaka leo *crane* ile bado haijafika. Kwa sababu Kampuni iliandika tu haijawa na matayarisho au kuna sababu za msingi ndio maana *crane* ile haikufika.

Mhe. Mwenyekiti, nende katika barabara. Sasa hivi nashukuru kuna barabara nyingi sasa hivi Pemba zimefanyiwa matengenezo, kusini wana wafadhili wao na Kaskazini Pemba, Konde/Wete, Gando/Wete na Wete/Chake kuna mfandhili wake na kuna barabara nyengine tano za vijijini ambazo hizi zinafadhiliwa na MCC. Katika barabara hizi ni pamoja na barabara iliyokuwemo katika jimbo langu inayotoka Bahanasa, Baya, Makongeni na Mtambwe, lakini hasa ni Uondwe.

Mhe. Mwenyekiti, ukisoma hichi kitabu kule kwenye jaduweli unatona kuwa matengenezo ya barabara hizi yanaendelea. Lakini mpaka hivi sasa baada ya wale watu kupima mle watakamopita na kutathmini mali ya watu hakuna jengine lolote linaloendelea. Tukisema kuwa ujenzi unaendelea ni taarifa ambayo haikualiana na ukweli ulivyo. Ningemuomba Mhe. Waziri kwa kuwa ujenzi unaendelea tuchukue hivyo hivyo kuwa unaendelea, naomba anisaidie kitu kimoja. Hii barabara haipitiki hata kidogo na inatutenga sana kutokana na mashimo makubwa yaliyotokea.

Namuomba Mhe. Waziri afanye angalau haja ya dharura kuziba yale mashimo tu alangalau wananchi waweze kupita kuweza kujipatia huduma mbali mbali. Wagonjwa hivi sasa waliokuwa wanahitaji kwenda Wete na kadhalika inabidi kuwachukua kwa vitanda. Si wakati tena huu wa kuchukuzana kwa vitanda. Hata hiyo azma ya Mhe. Rais wetu wambaye keshokutwa anastaafu tunamuombe maisha marefu tena maisha mazuri na atakuwa ameweka histori ya aina yake kama baba yake, tuone kuwa na huku nako angalau watu wanakenda mpaka mwezi wa September kama hilo shirika la MCC litashuhulikia hizi barabara.

Halafu wakati huo huo kuna barabara hii ya Bwagamoyo inayokwendea Kele, nashukuru sana kuwa Idara ya Utunzaji na Utengenezaji wa barabara imeiona hili, imewapa sijui ni Kampuni au ni nani. Kwa taarifa ya kitabu tayari barabara hii imeshatiwa kifusi, ndio kitabu kinavyoeleza. Lakini ninavyojua mpaka juzi kwa sababu ya mvua nyingi zilizokuwepo. Kule gari la kiparapara au greda lilikwenda mpaka kiasi kilomita moja na nusu likarudi. *Grading* haijafanywa na wala suala la kifusi halijazungumzwa kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nakuomba kwa taarifa kama hizi tunapozitia ziende wa wakati. Najua Wizara imeazimia kuitengeneza hii barabara. Lakini kuna ile kwamba imeshatengenezwa kila mtu ataona hivyo, kuna hatari baadaye yakatokezea mambo mengine kesho kutwa tunaingia katika uchaguzi mpya na kunakuja serikali mpya na kumbukumbu hizi zitabakia.

Mhe. Mwenyekiti, kuna barabara moja hapa Unguja ilitengenezwa na Alhamdulillah ni nzuri kutoka Tunguu mpaka Kinyasini. Kwa taarifa nilizonazo kuwa ilipitia Uzini. Kwa bahati mbaya watu wa uzini ambao walioathirika na barabara ile mpaka leo hawajapatiwa fidia zao. Namuomba Mhe. Waziri kama hili ni kweli atusaidie.

La mwisho kutokana na wakati ni kwamba Mhe. Rais wetu Dokta Amani Abeid Karume alikwenda Ndijani kufungua shule ya Nasari na aliona barabara ya Ndijani ilivyo na akaahidi kuwa ile barabara itatengenezwa, lakini mpaka hii leo nazungumza hapa nasikia tu kumeweka kifusi kidogo lakini hakuna hatua yoyote inayoendelea. Mhe. Rais akitoa agizo maana yake ni kuwa litekelezwe. Naomba tuende juu ya mstari kwa maneno yetu. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa ya kuchangia kuwa mtu wa mwisho katika bajeti hii. Mimi sikuwa na niya ya kuchangia lakini kuna jambo limenigusa sana imenibidi nichangie. Mheshimiwa hili jambo tumezungumza muda mrefu na kanipa ahadi nyingi, sasa leo nataka anipe ahadi na walionituma wasikie.

Kwanza niwapongeze Wizara, yeye mwenyewe Waziri, Naibu, Katibu, Wakurugenzi na watendaji wake wote kwa kuleta hotuba iliyokuwa nzuri, ni fupi lakini imeshiba maendeleo katika Wizara hii. Mimi nina mambo manne nataka nichachangie katika hotuba hii. Baadhi ya wenzangu wameyazungumza lakini na mimi kwa upande wangu nataka niongezee mawazo yangu.

Kwanza Ukurasa 36 kifungu 95 Shirika la Bandari. Nimpongeze Mkurugenzi na wafanyakazi wake wote kwa jitihada kubwa anayoifanya pale bandarini. Waswahili wanasema bandari ni uso wa nchi, mgeni yoyote akiingia pale akiona mandhari ya bandari basi anahisi na kwenye mji wote utakuwa ndiyo hivyo hivyo. Sasa namshukuru kwa jitihada zake lakini kuna mambo machache yanatoa haiba kwenye bandari ile na naomba niyazungumze yafanyiwe kazi.

Nimezungumza kwamba hivi sasa katika kitabu humu kuna utaratibu wa kujengwa jengo la kisasa la abiria. Tunashukuru kwa sababu lililokuwepo pale ni dogo. Lakini kila nikiangalia bandari ilivyo najiuliza jengo hilo litajengwa pahala gani ili liwe la Kimataifa na lipendeze. Namuomba Mhe. Waziri atuelekieze. Mimi kwa mawazo yangu nilikuwa naomba hapa ambapo

pamevunjwa jengo la Silver ambapo panaambiwa pawekwe magari pangependeza sana kujengwa jengo la abiria na packing ingetafutiwa sehemu nyengine, lakini kama wanapopazuri zaidi watanieleza.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo si zuri pale bandarini. Wenzetu sasa hivi ukwenda Viwanjwa vya Ndege vya Kimataifa hupekuliwi tena mabegi au ukapigwa kama mswaki ndani ya mbavu za nguo humu. Unaingia pahala unatia mzigo wako mnakutana mbele unakwenda zako. Lakini hapa petu yanavutwa mabegi yanatiwa mikono ndani ni mambo ya kizamani sana. Tupo karne ya 21 naomba kitafutwe chombo kiwekwe pale, unatiwa mzigo wako unapita upande wa pili *alarm* imelia unarudi unavua saa, unavua viatu mpaka unapita kiusalama. Lakini utakuta sasa hivi unakwenda na begi watu wanalitia mikono, wafungue zipu ndogo, kubwa, waguse vitu ambavyo havigusiki ndani ya begi.

Naomba pale tufanye mambo ya kitaalamu tutoke na mambo yale sasa hivi kwenda mtu unampitisha kitu ndani ya mbavu si utaratibu mzuri. Mtu anakwenda pale na mkewe na watu wengine wanaona mambo yale japo kwanza unatakiwa samahani, hetu twendeni na wakati sasa hivi. Naomba Mheshimiwa hili Wizara na Serikali inasikia na sisi twendeni na wakati. Wenzetu wanakuja pale, tunakwenda nchi za nje tunaona. Sasa na sisi tugeuke lililokuwa zuri tulifuate.

Pia kwenye bandari kuna tatizo la wageni hawa sehemu ya uhamiaji bado kile kibanda ni kidogo sana. Juzi nilimkuta mzungu kainama mwenzake ndio kaweka karatasi juu ndio anajaza, hapana hata meza. Inakuwa si utaratibu mzuri. Wenzetu Uhamiaji wajengo jengo watu wanafika wanachukua *permit* wanajaza wanaondoka kistaarabu kabisa. Lakini mtu anainama mgongoni anafanywa ndio meza, hili si jambo zuri, naomba nalo pia litizamwe ili bandari yetu nayo iwe ya Kimataifa.

Pia tulizungumza siku za nyuma kwa kuwa pale kazi nyingi zinakwenda na hatari zinatokezea basi tupate gari la kuzima moto, liwe la kudumu ili ukitokezea moto wasiitwe watu kutoka kiinua miguu pale pale wanafanya hiyo kazi. Lakini kitabu cha bajeti ya mwaka jana, mwaka huu sikuliona. Naomba na hili Mheshimiwa kama la muhimu basi Wizara kupitia Shirika la Bandari uwezo wanao walete gari moja la kuzima moto liwe la kudumu, imetokezea hatari japo mtaa wa karibu, Funguni, Malindi linaweza likasaidia, lakini na Bandarini litakuwepo.

Nadhani la mwisho kabisa kwa sehemu ya Bandari palikuwa na jengo la vigae sehemu ya wanayopandia watu meli kwenda Pemba. Muda mwingi jengo lile jina silijui wanalijua wenyewe nilisikia kwamba linakesi ipo Mahakamani kuna utaratibu haujakaa vizuri naona miaka inakuwa mingi. Nataka nipate kauli hili

jengo limeishiaje. Hiyo kesi imekwisha au limeshekuwa la Bandari sasa hivi au bado utata unaendelea. Ili na pale napo ni pazuri kupatumia kwa abiria wanaokwenda Pemba.

Sasa nije kwenye suala la barabara. Kwanza ukurasa wa 20 kifungu 45 barabara ya Amani Mtoni, tunashukuru kwamba fedha zimeletwa na aliyetoa ahadi na tunaambiwa kwenye kitabu hiki itajengwa. Lakini hapo pa kumalizia unataka kuingia Amani ni pahala pametiwa kifusi kuingia barabara ya pili. Hapo ni pahala penye kero kubwa na Waziri anatia kifusi kila muda wa wiki mbili. Ningeomba kwa kuwa lami ipo hebu apaweke lami apunguze ule usumbufu wa kutia kifusi. Pale ni pahala pafupi sana kama mita tano mpaka sita lakini kila wiki peshachimbika watu wanarovywa tope wameshavaa wanakwenda makazini. Naomba na pale apatizame ili tuondoshe hili tatizo.

Jengine niliwahi kwenda kwake nikamchukua kwenda kuniangalizia barabara yangu ya Mwachalale ni njia, pahala pafupi sana, pana kero kwa muda mrefu. Wazee waliomba habari ya kupitisha barabara na kibali nimepata. Mitihani ulionikuta kule kwamba hilo eneo lililoharibika ubavuni kwake kuna njia inapita kwenye nyumba ya mtu, Ile nyumba sasa ishapasuka. Imenibidi ukuta ule mimi nigharamie kuujenga ukuta mwengine wa ile nyumba na pahala padogo pa kutia fusi gari sita tu.

Mhe. Mwenyekiti, tumemwambia Mheshimiwa, tumekwenda tumekagua lakini tulipoanza bajeti akanambia ngoja nende Dodoma, kenda Dodoma karudi. Juzi namgusa ananambia ngoja nende tena, kenda karudi tena, nasikia nakesho anakwenda. Namuomba kabla kesho hajenda leo anipe kauli kwamba je, tukimaliza tutakwenda kumaliza au hutaki nirudi jimboni. Kama hataki nirudi naanambiye la kama tumekosana pahala basi ustadhi Hamza yupo mwambiye. Eh! bwana mwambie upande ule sasa asipite tena. Basi mimi nitatafuta njia nyengine. Lakini na sisi tupendane, wewe unataka kurudi na mimi nataka kurudi. Gari sita za kifusi mwaka wa pili!. Naomba Mheshimiwa nipate kauli nzuri kwamba safari hii sendi Dodoma kwanza tutamalizana halafu utakwenda Dodoma.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea sehemu ya barabara kuna matatizo katika barabara zetu kubwa hizi za kwenda Mkokotoni ya kwendea Makunduchi. Juzi nilikwenda Kizimkazi lakini mapande wa kuanzia Bungi mpaka Pete kuna mashimo mabaya sana. Nilisehauri kama hakuna kitengo cha kuziba mashimo barabara au kuifanyia matengenezo madogo madogo basi kingeundwa kwa kuweza kuzihifadhi barabara zetu kuu. Hili ndio lililotokezea Bububu matokeo yake sasa inatengenezwa yote kwa pamoja. Nadhani tukipata kigengo cha kutengeneza barabara zikiharibika mashimo madogo madogo inaweza ikasaidia katika kuweka barabara zetu kuwa nzuri. Si hivyo usipoziba ufa utajenga

ukuta. Namuomba Mheshimiwa kama kitengo hana cha kutengeneza barabara basi aandae kitengo hicho ili tuweze kutengeneza barabara zetu.

Nije kwenye ukurasa wa 30 kifungu cha 78 ujenzi wa jengo jipya katika uwanja wetu wa Kimataifa Zanzibar. Nashukuru wenzangu wamezungumzia mimi nimebakisha mambo mawili na naomba nitoa mawazo yangu ili Mheshimiwa aweze kuyafanyia kazi.

Pale kuna eneo la Uwanja wa Ndege kuna vijiji vya karibu Mazizini, Chukwani, tuliwahi kupita Kamati tukakuta kwamba baadhi ya maeneo ya Uwanja wa Ndege yanavamiwa. Tukashauri Wizara ingewezekana ungezungushwa uzio eneo lote la Uwanja wa Ndege, si lazima ukuta ni senyenge na majiti. Kwa bahati mbaya upande ule ambao watu wanavamia bado senyenge haijajengwa na watu bado wanajenga.

Ningemuomba Mheshimiwa na hili akalifanyia kazi isijekuwa baadaye mkaanza kushtakiana baina ya raia na serikali au raia na Uwanja wa Ndege. Itakuwa si jambo zuri. Kwa sababu majirani wale wale likitokezea tatizo Uwanja wa Ndege ndio wa manzo kuweza kusaidia. Ningelimuomba kabla ujenzi haujawa mkubwa Shirika likafanya utaratibu ili likaweza kuondosha matatizo haya ya ujenzi wa kiholela na kuvamiwa sehemu ya Uwanja wa Ndege.

Suala la pili baada ya kuongeza ran way kuwa ndefu zaidi tulisema hii njia ya zamani itafungwa watu apite Mbuyu Mnene kwenye njia mpya, lakini bahati mbaya jana nilikuwepo maeneo yale nilikuta bado gari zinapita kuendea sehemu ya Maungani. Ningeshauri kwamba ishakuwa njia imetengenea basi pale pengezibwa ili watu wakatumia njia ile ile mpya kuliko watu kupita pita mpaka kuje kutokezea ajali, ingawa hatuombi itokezee lakini itakuwa ni uzembe mkubwa wakati njia ipo na pale pameshapigwa marufuku lakini bado gari zinapita. Ningeshauri na hilo ni jambo dogo lakini linaweza likazua jambo kubwa. Kwa hivyo lifanyiwe utaratibu pazibwe watu watumie njia ya Mbuyu Mnene.

Nikiendelea na kuchangia nije kwenye ukurasa wa 29 kifungu 73 Uimarishaji wa Huduma za Viwanja vya Ndege. Wenzangu wamezungumza sana na mimi nitazungumza sana uwanja wa Pemba. Hivi karibuni tulikwenda sisi Pemba lakini bahati tulifika na mvua kwenye Uwanja wa Ndege kwa hivyo tulizunguka kama mara tatu pale uwanja muendeshaji hauwoni. Hata ilipoanuka mzua ndio tukatuwa. Sasa hizi taa sio lazima zitumike usiku lakini na siku za wakati wa mvua pia zinasaidia kwa kutua.

Pia sasa hivi usafiri wa ndege Pemba na Unguja umekuwa mkubwa sana kushinda huwo wa meli. Ningelishauri uwanja pia ungeengezwa urefu kidogo ili tukatoka kuingia na ndege za watu wa 3,4,6 inakuwa si jambo zuri, angalau ndege ndogo kidogo watu 40, 50. Naomba na hili tulizingatie, na kwa nchi yetu viwanja ni viwili tu Unguja na Pemba. Na hili katika mipango yenu na wataalamu wenu muombe wafadhili uwanja uongezwe kidogo.

Mheshimiwa na jengo pia lina usumbufu, jengo dogo sana, watu wanakuwa wengi bado linavuja, jenereta hapana. Tungeomba na huku mtafute wafadhili jengo lijengwe vile vile. Pemba na sisi tunakwenda kazi za Kamati ni lazima kwa kila mwaka tunakwenda mara mbili. Tunasumbuka sisi na wenzetu wa kule Pemba. Naomba hili lizingatiwe, taa, jengo, jenereta ili tuweze kufikia malengo yaliyokusudiwa na ndege kubwa za saizi ya kati zipate kwenda kutuwa. Tupunguze kwenda chata kubwa 10, 15. Kwanza chata inatisha mimi napanda sina la kufanya tu, ukija upepo unaupata, ikija mvua unahisi, sasa inakuwa matatizo tu. Kwa hivyo naomba tutengeneze uwanja wetu uwe mkubwa hivi vichata wapande watalii wanapokwenda kutembea sehemu za visiwani huko.

Mwisho kabisa katika uchangiaji wangu nije katika kifungu cha 91 ukurasa 34, Sekta ya Usafiri Baharini. Kwanza niungane na mwenzangu aliyemaliza kupongeza kwamba wenzetu hivi sasa wewekezaji wa sekta hii wanaleta meli mpya. Tunaomba hivi sasa kila anayetaka kuleta usafiri wa baharini aje na meli mpya. Kwa sababu meli kuukuu hivi sasa zinatesa watu, hivi juzi nilivyokwenda Pemba nilikwenda na wanangu nikaona gharama ya ndege ni kubwa nikawatia kwenye meli ya usiku. Nikaona mimi nikifika kule asubuhi nitawapokea. Wamepanda meli usiku kucha na mchana kutwa, saa 10:00 ndio wamefika Wete. Sasa hiyo tena imekuwa si meli, bora sisi tupakie makaa, ng'ombe, ndizi, lakini kwa abiria unawatesa. Mtu kucha yumo ndani ya meli na nusu ya kutwa. Hapa na Pemba jamani.

Mhe. Mwenyekiti, hizi meli nyengine si meli tena tuzifanye za mizigo. Meli sasa hivi inayokuja ije mpya, mtu anakwenda Pemba kwa nusu saa, au masaa mawili basi. Lakini leo kutwa kucha ndani ya meli mwisho cha kukila walikuwa hawana. Haya ni matatizo Mwenyekiti. Naomba Mhe. Waziri hili waliangalie na hao wanakuja kusajili meli basi ziwe meli za uhakika ili kuondosha usumbufu kwa wananchi wetu. Lengo ni kwamba yeye apate faida lakini na sisi pia tunaopakiwa ndani ya meli tupate kustarehe na tufike kwa usalama.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache niliyokusudia kusema azma ya ujumbe niliopewa nimemwambia Mhe. Waziri kwa hiyo nangoja jibu lake.

Baada ya hayo nitaunga mkono hapo akishanipa jibu wakati wa majumuisho. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti: Nawashukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano yenu. Leo jioni nategemea tutafanya majumuisho ya wizara hii nitawaombeni mfike ili tumsikilize Mhe. Waziri anapofanya majumuisho ili kupunguza buti pale pasipokuwa na haja.

Sasa naahirisha Kikao hichi mpaka jioni saa 11:00.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011
Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe tunategemea kukamilisha wizara hii kwa hiyo nitawapa waheshimiwa wawili nafasi ambayo wameomba sana asubuhi walikuwa na dharura kwa hiyo kila mmoja nitampa dakika 10 ili tuweze kumwita Mhe. Naibu Waziri na baadae Mhe. Waziri kwa majumuisho.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na pili naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na wafanyakazi wa wizara yake kwa hotuba hii ambayo ni nzuri, lakini kwa kazi nzuri za kuimarisha miundombinu ambayo ameifanya katika kipindi hiki.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba miundombinu ina umuhimu mkubwa sana katika uchumi na maendeleo ya nchi, lakini miundombinu inapata umuhimu mkubwa zaidi katika kipindi hiki ambacho nchi yetu inaingia katika soko la pamoja. Mhe. Mwenyekiti, soko la pamoja maana yake ni kwamba sasa watu watapata uhuru wa kutembea kati ya nchi zetu hizi tano, lakini si kwa ajili ya kufanya biashara ya mazao tu lakini kwa biashara ya ajira. Kwa hivyo, ajira inakuwa ni biashara kwa sababu nayo inakuwa katika soko.

Mhe. Mwenyekiti, ili soko la pamoja lipate ufanisi lazima soko hilo liwe na *support* kubwa ya miundombinu. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu miundombinu ndio inayowezesha soko kuwa *effective* kwa maana ya kwamba watu watalifikia soko kwa urahisi. Lakini soko la pamoja linatakiwa liwe *efficient* kwa sababu watu watapata taarifa ya soko pahala popote walipo wakati ambao wanahitaji. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii ya Mawasiliano na

Uchukuzi ndio kazi yake hiyo. Kwa hivyo, wajibu wa nchi wakati wa kuwa na soko la pamoja ni kujiangalia wenyewe ile nchi *cooperative advantage* yake ukilinganisha na nchi nyengine iko wapi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa historia yetu ambavyo inatueleza Zanzibar *cooperative advantage* yetu iko katika *location* kama kitovu cha biashara na hasa kwa sababu ni kisiwa ambacho kiko kati kati ya nchi ambazo zinafanya biashara. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, maana ya kusema hivyo ni kusema kwamba usafiri huu wa majini na usafiri wa anga una umuhimu mkubwa sana katika nchi yetu ili kuhakikisha kwamba na sisi tunayo nafasi ya kuzitumia fursa ambazo zinapatikana katika soko la pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, tutakapoingia katika soko la pamoja kwa sababu ushukuru kati ya nchi hizi na nchi za nje utakuwa ni mmoja. Kwa hivyo, suala la kupunguza ushuru ili kuvutia biashara litakuwa halipo, wafanyabiashara wataangalia ni pahala gani ambapo watapata *service* ya haraka kwa ajili ya kuendesha biashara zao.

Mhe. Spika, tunayo bahati nzuri sana kwamba Zanzibar sisi tuna uwezo wa kutoa mizigo kwa uharaka kuliko nchi yoyote katika East Africa na kwa hivyo hiki kinaweza kuwa ni kivutio lakini hakitoshi. Hakitoshi iwapo hakutokuwa na miundombinu madhubuti sana ya bandari ya kuwafanya watu wavutike ili walete mizigo yao, itoke kwa haraka na iende katika sehemu ambazo wanakusudia. Maana ya kusema hivyo Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba lazima *focus* yetu *emphasis* wakati Tanzania ikiingia katika soko la pamoja tuitumie sana bandari yetu.

Mhe. Mwenyekiti, bandari sikusudii Bandari ya Malindi, lakini nakusudia bandari zilizo katika nchi yetu ya Zanzibar maana mtu aliyeko Mombasa Bandari ya Malindi kwake yeye sio muhimu sana kuliko bandari iliyoko Pemba. Kwa hivyo, unaweza uka-*focus* ukasema kwamba tunaingiza *investment* zetu katika kuimarisha Bandari ya Malindi, Mpigaduri zote ambazo ziko Unguja, lakini ukasahau kwamba kwa watu walioko Mombasa pengine basi bandari ya Pemba zitakuwa zina unafuu mkubwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, sisi hatuna viwanda na sasa hivi hatuwezi kujidanganya, hatuwezi ku-*compete* na wenzetu kwa viwanda. Lakini Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia katika Afrika Mashariki nchi ambayo imejidhatiti kwa kuwa *operators* wazuri wa hivi vyombo vinavyokwenda baharini ni Zanzibar kuliko hata Tanzania Bara kuliko hata Kenya ingawa kote kuna bandari. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, *opportunity* hii tukiipoteza tukalemaa hatuwezi kuwa na *advantage* nyengine katika soko hili ambalo tunaingia sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa Shirika la Meli linahitaji kufufuliwa upya si kwa sababu ya kibiashara lakini zaidi kwa sababu za kiusalama katika nchi. Lakini ukiwa na shirika zuri la serikali ndilo linaloimarisha sekta binafsi na yako mashirika ya serikali ambayo yamefanikiwa. Shirika la Mabasi la pale London kubwa linamilikiwa na serikali na liko *very efficieny* lakini Mhe. Mwenyekiti, limepewa uhuru wa kufanya kazi. Tatizo liliko katika Shirika la Meli kuna *over employment* ambayo huwezi kuinasibisha kwamba hili ni kosa la Shirika la Meli.

Kwa mfano, suala la *employment* katika nchi ni suala la kitaifa. Mimi nakumbuka ndani ya Shirika la Meli wana mpango wa kufanya *sign on* na *sign off* ya kwamba unakaa unasaini kwa muda mfupi halafu unaondoka anakuja mwenzako. Kubadilishana huku kutawapa fursa watu wengi zaidi na watakao kaa kwa muda wa miezi tisa au tuseme mwaka mmoja basi angependa abakie tena mwaka mwengine.

Kwa hivyo, *efficiency* ya kazi yake inaongezeka lakini leo baharia ukimfanya kama mtu ambaye ameajiriwa Mhe. Mwenyekiti, ndio ukaona sasa *income* inayoingia pale na *expenditure* ya Shirika la Meli ni sawa sawa au siku nyengine *expenditure* inakuwa kubwa zaidi. Kwa hivyo, lawama zote za kudorora kwa Shirika la Meli liko kwenye serikali. Juzi imeuzwa Meli ya Mapinduzi imo taarifa humu ya pesa zilizopatikana ndani ya kitabu, mimi sijaiona aliyetoa taarifa anasema kwamba pesa tunazo ni Mhe. Waziri wa Fedha Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini sasa Dr. Mwinyi wewe ni Waziri wa Fedha, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi ambaye anashughulikia meli ni yule pale.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, pesa zinakwenda kwengine anaye *operate* meli yuko kwengine utamlaumu vipi. Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema natoa rai kabisa fedha zilizouziwa MV. Mapinduzi zipelekwe Wizara ya Mawasiliano waende wakafanye *reform* yao wanayotaka yakuwastaafisha wale ambao wanataka kustaafu na wako wengi sana,ili tuliwekee shirika na wafanyakazi ambao ni kiasi ya kuiendesha shirika ili tuanze *from the scratch* kulifufua na kuliendeleza shirika hili liweze ku-*compete* ndani. Vile vile liweze kusaidia Zanzibar kuweza kupata fursa na soko la pamoja la East Africa. Mhe. Mwenyekiti, kama hatukufanya hivyo itakuwa hatukulitendea haki.

Mhe. Mwenyekiti, bandari ndio *support* ya uchumi wetu na kazi iliyofanywa bandari si ndogo kubwa sana, lakini tunahitaji tu-*improve* bandari zaidi. Mhe. Mwenyekiti, bandari ile pale haitoshi hata kidogo wafanyabiashara wakivutika leo kuleta mizigo zao hapa basi hatuna pakuweka mizigo yao. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hakuna muda mimi nakushukuru sana kwa kunipa muda huu ingawa nilikuwa nina mengi sana.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie kwa kusema kwamba ili Zanzibar angalau tuwe na fursa na sisi ya kushiriki kwa manufaa ya umma huu katika Soko la East Africa kwa sababu hatuna viwanda, hatuna *service* kubwa basi sisi tuwe ni *service providers* wa mambo ya usafiri ili kuweza ku-*connect* sehemu hizi nyengine kibiashara na ni hapo tu ndipo Zanzibar inaweza ikanufaika. Kwa maana hiyo tuiangalie bajeti sana ya Mawasiliano na Uchukuzi na kipaumbele kipewe katika Mawasiliano na Uchukuzi. Baada ya Wizara ya Elimu basi iwe ni Mawasiliano na Uchukuzi. Baada ya kusema hayo nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu mwenye kutuwezesha kwenda na kurudi wote tukafika hapa salama. Pia nakushukuru na wewe kwa kunipatia hiyo nafasi kidogo na mimi nizungumze.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokupotezea muda wako mambo mengi yameshazungumza sana. Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye bandari kidogo nataka nizungumzie katika mambo ya usafiri. Mhe. Mwenyekiti, kwenye bandari huwa kunasafiri watu aina tofauti wakiwemo wagonjwa wa aina zote, bandarini bado hapajakidhi haja watu ambao kuwa hawajiwezi ambao ni walemavu wanapata shida na dhiki kubwa hata mimi mwenye nimeshapata shida kama hiyo. Mhe. Mwenyekiti, hapo zamani nilipokuwa bado sijapata cheo hiki nikisafiri mara kwa mara nilikuwa nauona ule mtihani unaonifika. Mhe. Mwenyekiti, hivi nimeshakuwa hapa Barazani basi huwa napata shida kwani pale hapana zile *will chair* za kusaidia wagonjwa waliokuwa hawajiwezi.

Mhe. Mwenyekiti, ukiitizama bandari yetu ya Mkoani masafa ya kutoka kwenye banda la abiria na kuja kwenye meli ni masafa makubwa sana, watu hawa wanapata shida sana. Mhe. Mwenyekiti, labda wale waliokuwa wana magari na watu wa kuwasaidia lakini wale waliokuwa hawana kutoka pale mpaka kwenye meli ni mtihani mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia na hii gati yetu inayosimama meli hizi za *Sea Express* ukitizama gari inakushusha nje lakini wewe uliyekuwa una mtihani wa mwendo kule bondeni ni mbali sana. Mhe. Mwenyekiti, kuna siku niko hapa Barazani nataka kupelekwa hospitali tukakosa ndege ikabidi nisafiri kwa boti kwenda Dar es Salaam basi tulipofika pale tumeshateremka gari waliambiwa walete kiti cha kunisaidia mpaka kule kwenye meli, walisema kwamba magurudumu hayazunguki. Mhe. Mwenyekiti, tulipofika pale ikabidi mimi ni mtihani kwenda pale na msongamano wa watu lakini nikajitahidi mpaka nikafika pale na kuingia kwenye meli. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli katika sekta zetu zote humu tunamosafiri mambo haya yanataka yaangaliwe kwa ni wengine huwa hawajiwezi.

Mhe. Mwenyekiti, siku moja tuliingia kwenye boti ya Sepideh na Mhe. Spika alikuwemo siku hiyo, mle kwenye boti mliingizwa mgonjwa anatoka Dar es Salaam anarudishwa Unguja basi tulipofika pale mgonjwa yule alibebwa kwa godoro. Mhe. Mwenyekiti, watu wote walikumbatia godoro hilo lisije likanyofoka mgonjwa akaanguka. Kwa hivyo, tunaomba katika sehemu za kusafiria muangaliwe watu ambao hawajiwezi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nitakuja katika sehemu ya barabara. Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana na nampongeza sana Mhe. Waziri na watendaji wake wote pamoja na Afisa Mdhamini wetu aliyekuwepo Pemba anatusaidia sana kama kupata tumepata, tunashukuru kwani ilikuwa njia hazipitiki hata kidogo. Lakini tunashukuru sana njia tayari na nampongeza sana Mhe. Waziri njia ya Ole – Kengeja akaweza kuifanyia utaratibu na tukaambiwa itajengwa na sasa nimeona tayari gari limeshakuja kusafisha bado huko kujengwa. Mhe. Mwenyekiti, zitakapojengwa njia zile Mhe. Waziri tujue kwamba wale watakaovunjiwa majumba yao, wakaharibiwa vilimo vyao ni kwamba waweze kupewa fidia yao kwa wakati ili kuondoa lawama isiwe tunatengeneza njia lakini tukawaudhi wenzetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuhusu barabara za vijijini ni nyingi sana zitakazojengwa ambazo zilizokwishapita kwenye miradi na zilizokuwa hazimo kwenye miradi. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri zile zilizokuwa hazikuingia kwenye miradi aweze kutusaidia kwa kutia kifusi, kwani njia hazitembeleki ni mabovu sana. Mhe. Mwenyekiti, juzi moja niliondoka hapa nikenda Pemba nilikwenda njia ya kupitia Mchanga Mdogo kutokea Mzambarauni pale tuliambiwa kuwa TASAF waliitengeneza kwa kuitia kifusi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nilipopita katika njia ile hapana sehemu iliyotiwa kifusi, sijui walipewa milioni ngapi maana utakuta kifusi kimetiwa kama hapa na hapo nje, unatoka kama hapa mpaka hapo Kikwajuni hakuna kifusi mawe yamesimama, njia imekatika ni hatari tupu. Kwa hivyo, tunaomba njia zile Mhe. Waziri azione kwa jicho la huruma maana mna wenzetu ni wakulima, wazalishaji na mambo mengine hata huyo ng'ombe nae anachoka ikiwa njia ni mbaya. Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Waziri azione njia za ndani kwa watu wote kuweza kupata mahitaji yetu bila ya matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli tunajenga barabara na tunazifurahia lakini nasema barabara zikishajengwa basi na huduma ipate ya barabara kwani zinafufuka. Mhe. Mwenyekiti, barabara hii ya *COGEFAR* tunayopita tukiisifu sana ni nzuri, mara moja tulikuja hapa tukaichangia kule Mipirani ilikuwa ina mahandaki ya mashimo, kidogo tulisikilizwa yale mahandaki yakafukiwa. Lakini tayari njia ile imeshatitia na imeshaanza kupasuka na tayari mashimo yanajirejea. Kwa hivyo, mimi naomba tusisubiri mpaka mashimo yakawa

makubwa tunaiomba Wizara ya Mawasiliano itakapona matatizo kama yale iweze kuyakilimbilia mbio mbio kuondoa yale matatizo madogo madogo tusisubiri mpaka njia ikaharibika ikawa haipitiki.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nije kwenye barabara ya Wete Mjini hiyo ni barabara tunaitembea kila wakati mara iko Mjini. Mhe. Mwenyekiti, kwa hakika ni mtihani mkubwa ukenda na gari basi spana mkononi kwa sababu barabara imechafuka kweli kweli, imepasuka, imechimbuka. Mhe. Mwenyekiti, kwa vile tayari imeshatiwa katika mradi inataka kujengwa basi angalau wizara hii watutilie viraka kwa sababu sisi wengine kazi zetu ziko kule.

Kwa hivyo, sisi ndio tunaoziona zile tabu za njia hizi zilizokuwa mbovu, hivyo naomba watu wa mawasiliano waweze kutuzibia vile viraka angalau zile njia zipitike mpaka muda ukifika basi zitatengenezwa. Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi nilikuta nataka nizungumze tu kidogo kwa ajili ya hali za watu ambao ni wagonjwa pamoja na mimi mwenyewe naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri mia juu ya mia na Mwenyezi Mungu amjaalie arudi tena aje atuendelezee hapa palipobakia.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe naomba wafuatao watuwie radhi sana sitoweza kuwaita kutokana na muda nao ni:-

1. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
2. Mhe. Asaa Othman Hamad
3. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
4. Mhe. Haji Faki Shaali
5. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
6. Mhe. Juma Duni Haji
7. Mhe. Ame Ussi Juma na
8. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Kwa hivyo, nawaomba radhi sana kwa sababu ya muda.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria katika kikao hiki jioni hii.

Mhe. Mwenyekiti, labda pengine kwa kumbukumbu zangu kuweka hesabu sawa nafikiria Mhe. Haji Faki Shaali ameshachangia ndio maana nilikuwa nakutizama.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo kwa baadhi ya wajumbe ambao wamechangia katika maeneo ya Shirika la Meli pamoja na usafiri na leseni.

Kabla ya hapo Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kuchukua nafasii hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria kikao hiki cha Baraza jioni hii. Vile vile naomba niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Chaani nao kwa kunichagua kwa kura nyingi kuingia katika Baraza hili. Hata hivyo, naomba nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri katika kipindi hiki tunachomalizia kwa Wizara hii ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi pamoja na watendaji wote wa wizara hii kwa upande wa Afisi Kuu na pia kwa upande wa Afisi Kuu Pemba nimshukuru Mhe. Afisa Mdhamini pamoja na watendaji wenzake kwa mashirikiano yakutosha ambayo wamenipa ili kuniwezesha kufanya kazi vizuri kwa kushirikiana nao pamoja. Mhe. Mwenyekiti, wenzetu leo wanatushukuru jinsi ambavyo kazi tulizozifanya ukilinganisha na miaka ya nyuma ambapo tulikuwa tukipata lawama nyingi katika wizara yetu kama mnavyokumbuka Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo napenda nitoe maelezo machache ambayo kidogo yamenigusa sana haidhuru hayahusiani na mambo haya niliyoyataja kumkumbusha Mhe. Ame Mati Wadi kwamba barabara yake ya Kiashangwe Muyuni imo katika kitabu cha Mhe. Waziri ukurasa wa 70 Nam. 14 inazungumzia barabara hiyo ya Muyuni hadi Kiashangwe itajengwa kupitia Mfuko wa Barabara. Pengine Mhe. Mwakilishi kwa sababu unajua sasa hivi tunakabiliwa na uchaguzi, pengine hakupata muda wa kuangalia hakuliona hilo.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba wizara yangu hadi sasa imechukua hatua za kutafuta utekelezaji wa mpango huu wa kitaifa. Napenda kulijuilisha Baraza lako tukufu kuwa hatua za utekelezaji tayari zimeanza kuchukuliwa katika hatua yangu kwenye ukurasa wa 7.

Mhe. Ali Denge Makame kuhusu hoja ya magari ambayo hayana viwango na hayapendezi machoni mwa watu. Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba wizara yangu kuipa ruhusua kuchukua abiria gari baada ya kuwa na kiwango hicho na haizingatii sana umbile la gari lakini kinachozingatiwa pale ni uzima pamoja na mambo mengine ambayo yanaifanya kuwa na sifa gari kufanyakazi katika maeneo hayo.

Mhe. Zakiya Omar Juma, Mhe. Ali Moh'd Bakari pamoja na Mhe. Ali Denge Makame hoja kuhusiana na umri wa madereva kupewa leseni wakiwa wadogo. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba wizara yangu kupitia Idara ya Usafiri na Leseni

inatoa leseni kwa wananchi wanaotaka kutokana na umri wao kutimia inategemea na madaraja yafuatayo.

Mhe. Mwenyekiti, daraja la "M" kuanzia umri wa miaka 16, daraja la "AB1 na C1" kuanzia umri wa miaka 18, daraja la "B, C, D1 na E" kuanzia umria wa miaka 21, daraja la "D1 kuanzia umri wa miaka 25. Dereva mwenye uwezo wa kuendesha magari ya abiria ni daraja "B", daraja "C" dereva ana uwezo wa kuendesha magari ya mizigo, daraja "B" dereva ana uwezo wa kuendesha magari ya *private hire*. Mhe. Mwenyekiti, daraja la "A" dereva ana uwezo wa kuendesha vyombo vya maringi mawili na daraja la "M" dereva ana uwezo wa kuendesha vyombo vya maringi mawili chini ya kiwango cha *50 CC.*

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu inaliangalia suala hili la udogo wa madereva sisi ndio maana kabla ya kupewa leseni kila mtu anatakiwa alete kitambulisho kinachoonesha umri wake au cheti cha kuzaliwa na hasa kwa sasa Mhe. Mwenyekiti, kwamba watu wote wa Zanzibar wanatakiwa wawe na ID kwa hapa petu ikimaanisha kitambulisho hiki cha ukaazi itaonesha dhahiri kwamba huyu mtu ana umri gani na kinajieleza vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na kutoa maelezo ya Waheshimiwa Wajumbe kwa upande wa Shirika la Meli waliochangia ni Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Waziri Kivuli, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, Mhe. Subeit Khamis Faki, Mhe. Zakiya Omar Juma, Mhe. Ali Moh'd Bakari. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba michango ya Waheshimiwa Wajumbe ilizungumzia uuzwaji wa Meli ya MV. Mapinduzi na upatikanaji wa meli mpya.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Meli ya MV. Mapinduzi imeuzwa kwa US$ 410.000 tokea tarehe 30/04/2010 kwa Kampuni ya *Dari East African Enterprises Limited* ya Dar es Salaam fedha hizo zimewekwa katika mfuko maalum wa hazina chini ya Wizara ya Fedha. Nafikiria hilo amelizungumza Mhe. Abasi Juma Muhunzi na ameomba kwamba fedha hizi pengine ni vyema zingepelekwa katika shirika ili tuweze kupata kuwalipa wafanyakazi ambao wamekuwa *over load* katika shirika hili. Mhe. Mwenyekiti, wazo la Mhe. Muhunzi tunalichukua na sisi tutashirikiana na wizara husika kuona kwamba kama kutakuwa na uwezekano huo wa kuzipata fedha hizo nafikiria itasaidia hili tatizo la wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba shirika hili lina wafanyakazi wengi kuliko inavyohitajika, lina wafanyakazi karibu mia moja na sitini na nne kati ya wafanyakazi hao wanaohitajika ni asilimia mia moja. Kwa hivyo, pengine wafanyakazi 64 tunaweza tukipata fedha hizi kuwapa fedha zao za kiinua mgongo kuweza kulifanya shirika likenda zaidi kibiashara.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba mawazo yote ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wajumbe hasa kubadilisha muundo wa shirika na kuweza kufanya kazi kibiashara tunalichukua na tutalifanyia kazi na serikali inakubaliana na masharti karibu yaliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe hasa ukizingatia maelezo yaliyotolewa na Mhe. Waziri Kilivuli ameainisha karibu maeneo manne. Eneo la kwanza serikali itafute mbinu za kufuta madeni ya shirika. Moja ni hili alilolitoa Mhe. Muhunzi jengine ni kwamba serikali itafute mbinu za kupunguza wafanyakazi nalo pia tunafanya hivyo kwa sababu sasa hivi wanapostaafu hatuajiri tena. Kwa hivyo, wale ambao wanapungua hawatoengezeka tena bali tunaendelea kupungua.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la tatu ni kwamba serikali itafute mtaji wa kuwapa hawa Shirika la Meli. Mhe. Mwenyekiti, hili nalo tunalifanyia kazi na ndio pale ambapo tumesema kwamba hili lazima liwe shirika na liweze kupata nafasi ya kuwa na mkopo wa kukopa benki. Huo utaratibu tayari tumeupeleka.

Mhe. Mwenyekiti, jengine la nne ni mageuzi ya kimuundo ya shirika ya uendeshaji yaani shirika liende kibiashara zaidi. Mhe. Waziri Kivuli mawazo yako tunayachukua na tutayafanyia kazi na tunakushukuru sana kwa kuwa karibu na wizara yetu kwa ushauri, si pale tu ambapo umeeleza hapa, lakini hata kabla ya hapa umekuwa ukitushauri na mawazo yako tunayachukua.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache na mimi nataka niseme kwamba naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu la Wawakilishi naongezea idadi hapa, Mhe. Suleiman Hemed na yeye kaleta. Napenda kuchukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na uhai. Lakini pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba leo tarehe 6 mwezi wa 7 tutakamilisha bajeti hii ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi badala ya kwanza ilikuwa tarehe 8, ikaja tarehe 7, lakini kutokana na dua mbali mbali za wajumbe muhimu humu imewezekana leo tarehe sita. Kwa sababu tuna kazi maalum lazima twende kwa haraka.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe 31 wamechangia bajeti yetu hii, nawashukuru sana. Wajumbe wenyewe ni kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi) ambaye pia ni Mwakilishi anayeagwa Jimbo la Muyuni.
2. Mhe. Omar Ali Shehe (Waziri Kivuli Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi).

3. Mhe. Ali Suleiman Ali, sijui kama na yeye anaagwa au anaendelea.
4. Mhe. Omar Ali Jadi
5. Mhe. Said Khelef Ali anaaga na yeye Jimbo la Bumbwini
6. Mhe. Haji Mkema Haji
7. Mhe. Said Ali Mbarouk
8. Mhe. Asha Moh'd Hilal
9. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum
10. Mhe. Hija Hassan Hija
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman, homa za uchaguzi zimepita kwa hivyo, kachangia vizuri sana.
12. Mhe. Mohammed Ali Salim
13. Mhe. Haji Faki Shaali
14. Mhe. Ali Denge Makame
15. Mhe. Subeit Khamis Faki
16. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
17. Mhe. Zakiya Omar Juma
18. Mhe. Ame Mati Wadi
19. Mhe. Hamad Masoud Hamad
20. Mhe. Ali Moh'd Bakari
21. Mhe. Salim Abdalla Hamad
22. Mhe. Ali Abdalla Ali
23. Mhe. Abass Juma Muhunzi
24. Mhe. Raya Suleiman Hamad
25. Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi.

Mhe. Mwenyekiti, hawa wamechangia moja kwa moja lakini pia kutokana na uchache wa muda Waheshimiwa wengine wamechangia kwa maandishi nao ni:-

1. Mwajuma Faki Mdachi
2. Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi
3. Mhe. Moh'd Kombo Mkanga
4. Mhe. Asaa Othman Said
5. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
6. Mhe. Suleiman Hemed Khamis

Mhe. Mwenyekiti, na wewe pia nakutarajia mema katika mwaka huu pamoja na mimi mwenyewe niliyesimama hapa, bila shaka hatutarajii mabadiliko makubwa katika Waheshimiwa Wawakilishi kwa Baraza letu lijalo.

Waheshimiwa Wajumbe nimeona nianze kwa jambo moja la jumla ambalo Waheshimiwa wa pande zote mbili wamelizungumza. Kuna mambo mawili lakini hilo moja nitalieleza baadae.

Suala hili lilianza kuzungumzwa na Mhe. Ali Suleiman Ali Mwakilisi wa Kwahani na likaungwa mkono kwa kuzungumzwa na Waheshimiwa wengi kuhusu daladala za Dungu. Wameiomba serikali ifikirie kwamba isiziondoe ziendelee kutoa huduma. Na kwa sababu siku zote Serikali ya Chama cha Mapinduzi ipo katika kulinda maslahi ya wananchi, ipo kwa ajili ya watu na kufikiria matatizo yao. Basi kutokana na maombi ya Waheshimiwa Wawakilishi tumeamua kuwa daladala zote za Dungu ambazo tayari ziko nchini zilizosajiliwa na ambazo bado hazijasajiliwa hadi leo tutaziruhusu ziendelee na shughuli za daladala.

Lakini ambazo hazijaingia nchini kuanzia leo tarehe 6/07/2010 haturuhusu iingie kwa shughuli za daladala. Hii nafikiri tunaenzi juhudi kubwa ya Serikali ya Mapinduzi kwa miaka kumi ya Mhe. Amani Abeid Karume lakini pia ni ishara njema kwa rais ajae. *(Makofi)*

Baada ya utangulizi huo Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nianze kwa kujibu baadhi ya hoja. Kwa sababu kutokana na mfumo mpya kwa mwaka huu isingelikuwa rahisi kuzijibu hoja zote. Wizara yetu sisi ni kubwa, ina mambo mengi muhimu kwa wananchi na wawakilishi walikuwa na hoja sahihi za kuzungumzia maendeleo ya wananchi wao.

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na ujenzi) alianza kwa kutoa hoja kwamba ahadi ya Mhe. Rais kwa ujenzi wa barabara za Kwamtipura – Amani na Boshwa – Tazari kuwa lini zitatekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kutoa maelezo kwamba, barabara zilizotolewa ahadi na Mhe. Rais ni nyingi mno kiasi kwama hatuwezi kutekeleza zote kwa wakati mmoja. Hata hivyo, sisi tunapopitisha bajeti yoyote ile, tunatekeleza ahadi ya Mhe. Rais. Nataka niwaambie tu kwamba barabara hizi zote zitatekelezwa na zimo katika Ilani ya Uchaguzi wa CCM wa 2010/2015. Lakini nataka niwaambie kwamba, kila fedha zikipatikana barabara hizi tutazishughulikia. Kwa hivyo, ahadi za rais ni nyingi nyengine hamkuzisema hapa, lakini ni vyema rais anayetoa ahadi kwa wananchi, kwa sababu kama huwezi kutoa ahadi huwezi kujipa *challenge* ya kufanya mambo.

Hata sisi Waheshimiwa Wawakilishi kama jimboni kwako hutoi ahadi utakuta hufanyi mambo yoyote ya maendeleo. Kwa hivyo, tukitoa ahadi tunatekeleza.

Barabara ya Kiashange – Muyuni imo katika mpango wa matengenezo kwa kutumia Mfuko wa Barabara, waheshimiwa naomba muangalie kiambatanisho nambari 5(b) barabara Nam. 14 ukurasa wa 70 utaikuta barabara hiyo. Nafikiri hii hata Mhe. Ame Mati alizungumza suala hili.

Kuhusu Idara ya Mipango Pemba kuwa haiko katika ubora na mwanasheria wake. Jibu ni kwamba, tayari wizara imeshafanya ukarabati wa nguvu na tayari ofisi hizo zimeingizwa samani kama vile viti, meza na kapeti. Mbali ya hizo, wizara imeajiri wafanyakazi wawili waliomaliza Chuo Kikuu kwa ajili ya idara hiyo. Yaani tumeajiri wasomi wawili kwa Pemba kwa Idara ya Mipango ambao watasaidia kuimarisha ofisi yetu ya Pemba. Hivi sasa wakati wowote wizara tutaajiri mwanasheria wake kwa ajili ya ofisi ya huko Pemba.

Kuhusu ujenzi wa *Jetty* karibu na Mnara wa Nungwi Waheshimiwa Wawakilishi walizungumza. Jibu lake ni kwamba, wizara yangu inalielewa na inalifuatilia kwa karibu kwa kushirikiana na Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji na vyombo vyengine vinavyohusika ikiwemo Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ. Suala hili tunajua ni tatizo lakini hatuwezi tukalipatia ufumbuzi sisi Wizara ya Mawasiliano pekeetu. Kwa sababu pia ruhusa ya ujenzi wa *jetty* haiko katika wizara yetu.

Hoja ya Kampuni ya *Al Ghubra Marine Service* na kuleta *crane* katika Bandari ya Malindi. Waheshimiwa ni kweli kwamba wizara ilitoa barua ambayo ilipelekwa kwa *Management* ya Shirika kwamba, wizara haina pingamizi na uletaji wa *crane.* Lakini *managementi* iliipokea barua na kwa utaratibu. Lile ni shirika lina Bodi yake ya Wakurugenzi. Kwa hivyo, baada ya kuipokea ile barua wameipeleka kwenye bodi, kwenye kikao chao cha tarehe 20 na 30 ya mwezi wa 6 hilo suala wamelizungumza kwa kina na bodi imetaka kujua kutoka kwa *management* madhara na faida za kuruhusu wawekezaji binafsi kuweka *crane* katika Bandari ya Malindi na kwa vile zaidi Shirika la Bandari hivi sasa lina mpango wa kununua zana nzito zikiwemo *crane.*

Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi tuvute subira tuangalie hatma ya maamuzi ya Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Bandari, wala hakuna ambaye kapinga amri ya waziri wala hakuna huyu mkubwa, huyu mdogo tunataka tufuate taratibu ili suala hili likae sawa.

Mhe. Ramadhan Nyonje pia, Mhe. Haji Faki Shaali na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, wamesema mfumo wa mabadiliko ya uendeshaji wa viwanja vya ndege na kuwa na usimamizi mzuri. Mhe. Mwenyekiti, mchakato wa mabadiliko wa mfumo huo tayari umeanza ambapo rasimu ya sheria ya kuanzishwa Shirika la Viwanja vya Ndege Zanzibar imeshatayarishwa na kupitishwa na wadau mbalimbali. Hatua inayofuata ni kuwasilishwa serikalini kwa hatua zaidi.

Wizara yetu katika kipindi cha mwisho mwisho tulitayarisha rasimu mbili za sheria. Sheria ya Viwanja vya Ndege kuwa Shirika na Sheria ya kuunda Mamlaka ya Barabara Zanzibar. Lakini kwa bahati mbaya muda haukutosha

mwaka huu kwa hivyo tusingeliweza kuja katika Baraza hili tukaleta sheria ya mabadiliko hayo. Lakini *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akipenda kwa wale watakaokuwepo basi mwakani nafikiri sheria hii itakuwa tayari.

Mhe. Ramadhan Nyonje, Mhe. Omar Ali Jadi na Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum, Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mhe. Subeit Khamis Faki na Mhe. Ali Abdalla Ali walitoa hoja kukosekana kwa taa katika barabara ya kurukia na kutulia ndege, uzio na majenereta ya akiba na uimarishaji wa Zimamoto katika Kiwanja cha Ndege cha Karume Pemba.

Ni kweli Mhe. Mwenyekiti, hatua mbali mbali za utekelezaji zimeanza kuchukuliwa ambapo mazungumzo na Kampuni ya *Siemens* yamefanyika kufanya utafiti wa kujua gharama halisi za mahitaji ya uwekaji wa taa katika kiwanja hicho na hatimaye kukamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha za mradi huo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*). Ujenzi wa uzio katika kiwanja hicho unaendelea kwa kupitia sera za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Zimamoto huduma zake zitaimarishwa.

Tumepeleka maombi ya mkopo kutoka *ADB*, lakini kabla ya kupewa pesa lazima kuwe na mchanganue halisi wa hayo mahitaji yenyewe. Kwa hivyo, Kampuni ya *Siemens* wataalamu sana wa uwekaji wa taa, tumewatumia hawa watufanyie tathmini halisi ili tuweze kujua mahitaji katika kiwanja chetu cha Pemba.

Mhe. Omar Ali Shehe (waziri kivuli), yeye alikuwa na hoja kupungua kwa makisio ya matumizi ya kazi za maendeleo kwa asilimia kumi na nane na ongezeko dogo la kazi za kawaida na makusanyo ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Mhe. Mwenyekiti, jibu ni kwamba, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba ni kweli kwa mwaka 2010/2011, kumekuwa na ongezeko dogo kwa matumizi ya kazi za kawaida na makusanyo. Hii inatokana na hali halisi ya viazio vya mapato katika wizara yetu na makisio tuliyopewa. Kwa upande wa kazi za maendeleo, mchango wa serikali kwa mwaka 2009/2010 ulikuwa ni shilingi 5,750,000,000/- na kwa mwaka 2010/2011 ni shilingi 9,100,000,000/-, sawa na ongezeko la asilimia 58.

Kwa upande wa fedha za wahisani mwaka 2009/2010 ilikuwa ni shilingi 58,834,350,000/- na kwa mwaka 2010/2011 ni shilingi 43,621,230,000/- sawa na upungufu wa asilimia 25. Hii imetokana na kukamilika kwa Mradi Mkuu wa Barabara ya kutulia na kurukia ndege ambapo peka yake ulikuwa ni shilingi 34,589,063,000/-.

Kuhusu hoja ya kwamba serikali imefikia hatua gani katika utekelezaji wa mpango mkuu wa taifa wa usafiri. Jibu ni kwamba, Mhe. Mwenyekiti, naomba kumfahamisha Mhe. Mwakilishi na Baraza lako tukufu kwamba, wizara yangu imejitahidi sana kuchukua hatua tofauti kutekeleza mpango huu wa kitaifa. Napenda kulijulisha Baraza lako tukufu kuwa, hatua za utekelezaji tayari nimeshazieleza katika hotuba yangu kwenye ukurasa wa saba.

Hoja ya kuwa wizara izingatie ukarabati wa uzio wa Kiwanja cha Ndege cha Karume Pemba. Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu kwamba tayari wizara imetenga fedha kwa ajili ya uzio huo wa Karume kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 76 ukurasa wa 30 katika kitabu cha hotuba.

Pia Mhe. Mwakilishi alitaja changamoto zinazozikabili Shirika la Bandari ambazo hivi sasa shirika linashughulikia kwa mujbu wa uwezo wake wa kifedha. Kuhusu vifaa vya kufanyia kazi, katika bandari zetu za Unguja na Pemba, suala hilo tayari hivi sasa limeanza kushughulikiwa kwa kununua vifaa vipya.

Kuhusu kudidimia kwa sehemu ya Gati ya Mkoani, wizara yangu kupitia Shirika la Bandari imepanga kulishughulikia suala hilo kama ilivyoelezwa katika kitabu cha hotuba. Kuhusu ujenzi wa bandari mpya ya Mpiga Duri, mpango huo unaendelea kushughulikiwa na wizara yangu hivi sasa tunaangalia njia za upatikanaji wa mtaji kwa kuendeleza mradi huu. Tunahitaji karibu shilingi milioni 500 kwa ajili ya mradi wa Mpiga Duri.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Suleiman Ali alizungumzia kwamba, alisikia kwamba chombo cha *Seagull* kiligonga jahazi Dar es Salaam na kukimbia bila ya kuokoa watu na nahodha anatafutwa. Mhe. Mwenyekiti, ukweli ni kwamba, mnamo siku ya tarehe 28/06/2010, Boti ya *Seagull* ilikuwa katika *charnel* ya Bandari ya Dar es Salaam kuelekea Zanzibar, ililiona jahazi likija kwa kasi kutokana na upepo mkali. Nahodha wa meli hiyo alifanya kazi ya ziada kuepuka ajali hiyo, ambapo alianza kwa kuiarifu *signal station* na kusimamisha chombo hicho ili kulipisha jahazi.

Lakini jahazi hilo lilishindwa kuelekea njia na kuigonga Boti ya *Seagull.* Jahazi hiyo ilichanika na kuzama hapo hapo. Chombo cha *Seagull* kiliwaokoa watu watatu waliokuwemo kwenye jahazi hiyo na baadae kuendelea na safari ya kuja Zanzibar ikiwa na baadhi ya watu waliookolewa katika jahazi hiyo. Jahazi hiyo inajulikana kwa jina la ‘Usilolijua’, ilisajiliwa Mafia usajili wake nambari M647. Mheshimiwa kidogo habari hukuzijua vizuri. Kuvuma kuwa nahodha anatafutwa si habari za kweli, kwani bado anaendelea na kazi kwenye meli hiyo na hakuna taasisi inayomtafuta au iliyomzuia kufanya kazi zake.

Mhe. Omar Ali Jadi na Mhe. Said Khelef Ali hoja ya kuchelewa kuanza kwa ujenzi wa barabara ya Mfenesini – Bumbwini kwa sababu za uhamishaji wa bomba la maji ambalo gharama zake ni shilingi milioni 5. Jibu ni kweli kuwa mkandarasi amechelewa kuanza kazi hiyo kutokana na kuchelewa kuondoshwa kwa vikwazo kwenye eneo la barabara hiyo ikiwemo bomba la maji ambalo liko karibu sana na barabara.

Napenda kuwajulisha Waheshimiwa kwamba, si kweli kuwa gharama za uhamishaji wa bomba hilo zilikuwa ni shilingi milioni 5. Gharama halisi kwa uhamishaji wa huduma za jamii maji na umeme pamoja na fidia za vipando, mazao na nyumba katika barabara ya Mfenesini – Bumbwini ni kama ifuatavyo:-

Huduma za maji ni shilingi 364, 540,000/-, huduma za umeme shilingi 35,691,178/-, mazao shilingi 95,434,164/- na nyumba shilingi 258,393,000. Kwa ujumla tunahitaji shilingi 758,742,000/- ili tuweze kuondoa miundombinu hiyo kabla gharama za ujenzi wa barabara hiyo kuanza. Wizara yangu katika jitihada za kuona hali hiyo inaanza mapema, tayari tumeshafanya mazungumzo na wahusika wa Mamlaka ya Maji na Shirika la Umeme na tunatarajia kwamba, shughuli hii itaanza hivi karibuni.

Kuhusu hoja ya kwamba *UUB* ijenge daraja la Zingwezingwe kwa kutumia fedha kutoka Mfuko wa Barabara. Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kwa kushirikiana na Mfuko wa Barabara italizingatia ombi la Mhe. Said Khelefu ili wananchi wa Zingwezingwe nao wapungukiwe na tatizo hili.

Pia alitaka kujua kwamba nani anamiliki mnara ulioko Bumbwini ambao umekaa kwa muda mrefu haufanyi kazi na kwamba walinzi wa mnara huo hawalipwi mshahara wao kwa muda mrefu. Kwanza Mhe. Mwenyekiti, ujengaji wa minara ya kampuni zote unajengwa baada ya makubaliano ya wenyeji au mwenye kiwanja na kampuni, lakini kama kuna kazi za ulinzi pia ni wajibu wa mtu huyo muhusika na kampuni kuingia mkataba. Mnara ule aliouzungumza Mhe. Said ulijengwa na kumilikiwa na Kampuni ya *EXELLENTCOM* ambayo makao makuu yake yako Dar es Salaam. Kwa hivyo, wizara yangu kwa hakika inaratibu lakini suala hili lilikuwa la kampuni na wahusika moja kwa moja.

Kwa bahati mbaya snaa kampuni hii ni moja katika makampuni yaliyopata athari iliyotokana na kuporomoka kwa uchumi duniani. Mara tu baada ya mtikisiko wa uchumi kuanza ulimwenguni, kampuni ya *EXELLENTCOM* imeshindwa kuendelea kutoa huduma. Wiazara kupitia kamati maalum ya minara imekuwa ikifanya mawasiliano ya mara kwa mara na kampuni hii ili kujua hatima ya minara yao. Lakini majibu ni kwamba, wanaomba kupewa

muda na wako mbioni kutafuta hatua mbadala kujikwamua. Hivyo suala la mnara huo wa Bumbwini linaeleweka na limo katika utaratibu wa kupatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Suala la mlinzi wake, wizara yangu itafanya mawasiliano na wahusika kujua kwa nini mshahara wake umecheleweshwa. Lakini namuomba Mhe. Mwakilishi kuhakikisha kuwa huyo mlinzi anao mkataba wa ajira pamoja na kuelewa kwamba kampuni hiyo imekubwa na mtikisiko wa kiuchumi duniani. Kampuni hii asili yake ni Arabuni, lakini nafikiri haikufanya kazi swana kwa sababu ya mtikisiko.

Mhe. Haji Mkema Haji alitoa hoja ya vifaa vya uokozi kwa vyombo vya kienyeji havipatikani, alitaka itolewe elimu kwa mabaharia wa majahazi. Jibu ni kwamba, vifaa vya uokozi katika vyombo vya kienyeji ni *life jackets*, *life rings* na simu za mkononi. Vyombo vyengine ni *first aid kit* zana za kuzimia moto. Chombo kabla ya kupasishwa na kupewa leseni lazima vifaa hivi viwemo chomboni. Vifaa hivi vinapatikana madukani hapa Zanzibar hata katika maduka ya vifaa vya uvuvi.

Kuhusu elimu ya mabaharia wa majahazi ni kuwa Afisi ya Mrajis wa Meli imeshaanza kuchukua hatua ya kutoa mafunzo mbali mbali kwa mabaharia na kuwafanyia mitihani kabla ya kuwapa vyeti. Aidha, kwa kushirikiana na Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar, Afisi ya Mrajis wa Meli inakusudia kuwapatia mafunzo ya zimamoto mabaharia hao.

Kuhusu hoja ya kuwekwa kwa udongo unaochimbwa barabarani kwenye eneo la bonde la mpunga Koani ambalo limeharibu eneo ambalo wananchi wanalima mpunga. Jibu ni kwamba, mkandarasi aliyeomba eneo hilo kwa ajili ya kuhifadhia udongo kwa sheha wa shehia hiyo ambapo pamewekwa udongo huo na alipewa eneo hilo kwa muda. Kwani udongo huo utatumika kuimarisha maeneo mbali mbali ya barabara hiyo likiwemo eneo ambalo anachimba kifusi kwa hivi sasa. Hii inazingatia matakwa ya kimazingira ambapo eneo hilo ni hifadhi ya muda tu wa udongo huo. Kwa hivyo, udongo huo si wa kudumu na baadae wenyewe watauchukua na kuufanyia kazi kama walivyokusudia.

Kuhusu ujenzi wa Daraja la Mwera kwamba hauendi vizuri. Mhe. Mwenyekiti, daraja hili linajengwa kutokana na mkataba wa ujenzi na wataalamu mbali mbali wamekuja kuliangalia wakiwemo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wamefanya *design* na litajengwa kama tulivyokubaliana katika mradi huo.

Kuhusu barabara ya Koani – Jumbi kuwa iko katika hali mbaya. Ni kweli Mhe. Mwenyekiti, barabara hiyo iko katika hali mbaya, lakini napenda kumjuilisha Mhe. Mjumbe kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inalijua tatizo la

barabara hiyo. Barabara hiyo imo katika mradi wa barabara tatu za vijijini Unguja ambazo serikali imeshatiliana saini na *BADEA* mkopo wa shilingi za Kimarekani milioni 8 na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inatakiwa kuchangia shilingi 2.36 milioni. Kwa hivyo, barabara hii ni miongoni mwa barabara hiyo ikiwemo na barabara ya Miwani na barabara ya Jendele – Ungujaukuu. Nafikiri Mhe. Haji Mkema Haji bado mambo yako yatakuwa mazuri tu. Yaani hii nyengine itakuwa moja Kizimbani – Kiboje nyengine Cheju – Kaebona. Hilo pia ni Jimbo la Koani.

Mhe. Said Ali Mbarouk anasema hoja yake ya mwanzo kwamba kasi ndogo ya utekelezaji wa upanuaji wa barabara Wete – Gando. Mhe. Mwenyekiti, mradi huo wa utekelezaji ulianza kwa kasi ndogo, ulitokana na matatizo ya kifedha yaliyopelekea mkandarasi kutoweza kulipwa fedha za *advance payment*, ambazo zingemsaidia sana mkandarasi ku-*mobilize* vifaa na zana za kutosha kwa ajili ya kazi za utekelezaji wa mradi huu. Matatizo haya hivi sasa yamepatiwa ufumbuzi na serikali kwa kushirikiana na mfadhli wa mradi huo. Kuanzia Julai mwaka huu, barabara hiyo inatarajiwa kujengwa kwa kazi na ari mpa. Naomba kumhakikishia Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Gando kuwa ujenzi wa barabara hii hivi sasa utaendelea tena kwa kasi zaidi bila ya kusimama mpaka mwisho wa utekelezaji wake.

Kuhusu upana wa barabara hiyo, ni kuwa tokea wakati wa hatua ya mwanzo barabara hizo na wakati wa kuandaa mradi huo iliamuliwa kuwa barabara hiyo imepangwa kujengwa kwa ikiwa na upana wa mita sita na sio mita kumi na nane. Hakuna barabara ya Unguja hata moja yenye mita kumi na nane. Na sehemu ya wapita kwa miguu yenye urefu wa mita moja hadi mbili kuanzia Wete mjini hadi eneo liliopo kambi ya mshauri mjenzi yaani ya kilomita moja. Baada ya kilomita moja hiyo kuelekea Gando upana wa barabara hiyo umepangwa kuwa kilomita 5.5 na mabega ya mita 1.2. Si wizara wala mshauri wanaoweza kubadilisha upana huo. Napenda kuthibitisha kwa Baraza lako hili kwamba, barabara hii itajengwa na kuwa na upana huo huo ambao umo katika mpango wa mwanzo.

Kuhusu kuwekwa kwa kifusi au mchanga katika maeneo yanayotumika kwa kilimo ni kuwa mkandarasi hapaswi kufanya hivyo bila ya ridhaa ya mwenye shamba au eneo. Tutaendelea kuelimisha na kumtaka mkandarasi huyo kama anayo tabia hiyo aache mara moja.

Kuhusu tathmini ya nyumba na mazao ni kuwa wizara huziomba taasisi za wizara zinazohusika na masuala ya mazao kufanya tathmini. Kwa mfano, sisi tunapotaka kujenga barabara kwa mazao tunawafuata watu wa kilimo kutufanyia tathmini na kwa nyumba ni watu wa Idara ya Majenzi. Itakuwa si vyema sisi ambao tunahusika na kazi hiyo tukajifanyie tathmini wenyewe,

tunaweza tukawalipa kidogo au kuongeza zaidi kwa maslahi yetu. Kwa hivyo kazi hii inafanywa na taasisi nyengine za serikali.

Mhe. Said Ali pia na Mhe. Rashid Seif Suleiman na Mhe. Ali Moh'd Bakari alizungumzia uwiano wa barabara kati ya Unguja na Pemba.

Naomba kulieleza Baraza lako tukufu kuwa, kijumla barabara zetu zinapotaka kujengwa huwa tunaomba ufadhili wa Washirika wa Maendeleo kwa kufanya *"Feasibility study* na *detailed design"*. Baada ya uchambuzi yakinifu huo na utayarishaji wa michoro kuwa umewaridhisha wafadhili wanaohusika, wao ndio huamua barabara zipi wazingharimie. Katika miaka ya 90 wizara ilifanya upembuzi yakinifu kwa barabara zote za Unguja na Pemba na baada ya kupatikana kwa ripoti hiyo, wizara hutumia kuiuza kwa wafadhali wao ndipo huchagua barabara gani kujenga.

Sisi kama wizara tunapenda barabara zote zijengwe kwa wakati mmoja. Mfano mzuri wa maelezo haya ni kuwa, tulipopata ufadhili wa MCC, wizara iliwasilisha maombi ya barabara 16 Unguja na Pemba. Hata hivyo, wao wakaamua kuchukua barabara 5 za Kaskazini Pemba ambazo ndizo watakazozifadhili. Serikali haina uwezo wala mamlaka ya kuwalazimisha wafadhili wagharimie barabara ambazo hawakuzichagua.

Kwa upande wa miradi inayogharimiwa na serikali pekee, wizara mara zote huhakikisha kuwa kuna ujenzi wa barabara moja Unguja na moja Pemba kama ilivyo hivi sasa.

Suala jengine muhimu ni uwiano wa mtandao wa barabra Kijiografia. Kisiwa cha Pemba ni kidogo kuliko cha Unguja. Mtandao wa barabara wa visiwani bila shaka unatafautiana kwa ukubwa, Unguja mtandao wa barabara wa kilomita 680 ikiwa ni asilimia 59.13 ya mtandao wa barabara ya Zanzibar na Pemba ina mtandao wa barabara wa kilomita 470 sawa na asilimia 40.86. Hivyo, ni dhahiri kwamba kutakuwa na tofauti kidogo.

Hata hivyo, katika bajeti ya miaka miwili hii au ya miaka miwili mfululizo, miundombinu ya barabara iliyojengwa Pemba ni mingi zaidi kuliko ya Unguja. Kwa mfano, kwa mwaka 2010/2011, mtandao wa barabara tunazotarajia kujenga Pemba ni mkubwa zaidi kuliko za Unguja, Pemba ni asilimia 78 na Unguja asilimia 22.

Kuhusu Bandari ni kweli kuwa taa ya mnara wa Kigomasha haiwaki kwa sasa, taa hiyo pamoja na ile ya Matumbini zimekuwa na matatizo tokea kufungwa kwake. Hata hivyo, Shirika la Bandari hivi sasa lina mpango wa kubadilisha taa zote za minara na kuweka taa za aina nyengine mpya.

Kwa upande wa gati ya Wete, shirika limeifanyia matengenezo gati hiyo katika mwaka 2004/2005 kwa kuiongeza upanda kutokea mita 3 hadi 6 na mpango wa kuirefusha hadi kina kirefu bado upo. Ushauri wake wa kuonesha gharama za miradi katika Bajeti umepokelewa na tutaufanyia kazi siku za baadae.

Mhe. Asha Moh'd Hilal yeye alikuwa na hoja ya usumbufu wanaoupata wafanyabiashara wa Zanzibar wanaposafiri na Shirika la Ndege la *Emirates* kwa kulipa ushuru Dar es Salaam na kupanda ndege ya *Precision Air* ambapo hulazimika kulipia uzito wa ziada katika mizigo yao.

Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe, hoja hii ya Mhe. Asha Moh'd Hilal tunaichukua, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi tutaifanyia kazi kwa kushirikiana na mashirika ya ndege ikiwemo *Emirates* ili wananchi wetu wasipate usumbufu na matatizo katika safari zao.
Suala la vyombo vya baharini kujaza abiria kupita kiasi lilizungumzwa na Mhe. Asha Moh'd Hilal, Mhe. Zainab Omar Moh'd, Mhe. Rashid Seif Suleiman na Mhe. Subeit Khamis Faki. Mhe. Mwenyekiti, jibu ni kwamba Afisi ya Mrajis wa Meli imeweka maafisa katika bandari zetu zote wanaosimamia idadi ya watu wanaoingia katika vyombo. Tatizo la kuzidi abiria kwa sasa limedhibitiwa kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, kuna mazingira yanayoonesha kuwa boti imezidisha abiria kama vile idadi ya watoto wengi wanaosafiri na wazee wao hasa kwa usafiri baina ya Unguja na Pemba au abiria wanapopanda vyomboni kukiwa na vurugu. Jambo la msingi ni kwa vyombo vya ulinzi kusimamia kuepusha vurugu.

Hata hivyo, bado tumewahi kuishirikisha Kamati yetu ya Mawasiliano na Ujenzi kuangalia zoezi hili na walikwenda na wenyewe wakajiridhisha kwamba hakukuwa na abiria waliozidi isipokuwa kila mmoja ana mtoto wake mgongoni.

Kuhusu serikali kununua vifaa vya uokozi ni kuwa kwa sasa hakuna vifaa vya uokozi vilivyonunuliwa. Hata hivyo, kuna Mswada wa Sheria ya Uokozi unaondaliwa kupelekwa ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo suala hili la uokozi limezungumzwa kwa pande zote mbili za Jamhuri yetu ya Muungano. Katika sheria hiyo kuna mapato yatakayokusanywa kwa ajili ya kuhudumia shughuli za uokozi. Aidha, Mamlaka itakayoanzishwa ya Kusimamia Usalama wa Baharini Zanzibar itakuwa na uwezo wa kukusanya mapato maalum kwa ajili ya shughuli za uokozi.

Mhe. Zainab Omar Moh'd alitoa hoja kwamba tunapojenga barabara tuweke *road reserve* ili kuepuka gharama wakati wa upanuzi wa barabara. Mhe. Mwenyekiti, tumeupokea ushauri wa Mhe. Zainab na tutaufanyia kazi. Katika sheria yetu mpya ya barabara suala hili tumelizingatia kwa kina.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine Mhe. Zainab Omar Moh'd alituomba kwamba tusipende sana kukata milima wakati wa ujenzi wa barabara. Nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba wizara inajitahidi sana kuepuka ukataji wa vilima kusikokuwa kwa lazima ili kupunguza athari ya kimazingira, lakini pia tutakuwa tayari kupunguza masafa ya ukubwa wa barabara zetu.

Kuhusu hoja ya kujengwa *round about* mbili za Machomane na branchi ya Benki ya Watu Zanzibar Chake Chake. Napenda kumjibu kwamba ombi lake tunalizingatia na wizara italifanyia kazi na kuona jinsi gani tunaweza kufanikisha zoezi hilo la ujenzi wa *round about* mbili Pemba. Ikiwezekana zisiwe mbili tu, tutaangalia pia na eneo la Wete kama inawezekana napo tuweze kuweka *round about.*

Mhe. Hija Hassan Hija wasi wasi juu ya ubora wa barabara. Mhe.Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba ubora wa barabara utasimamiwa vizuri na barabara yote itakuwa katika kiwango kilichokusudiwa. Tatizo la *drift* iliyoharibika ni tatizo la kiufundi na tayari iko katika hatua ya kufanyiwa marekebisho. Napenda nimuarifu Mhe. Hija kwamba wataalam kutoka Kenya wanatarajiwa kufika tarehe 12 mwezi huu, kuja kujifunza jinsi gani sisi tumefanya na wao wakaendeleze utaalam huo, huko huko anakosema yeye kumefanyika vibaya Mtambile/Mwambe.

Kuhusu tatizo la nyumba nne za Muambe ambazo zimeingia maji kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema mwenyewe Mhe. Hija Hassan Hija mimi ni mtu wangu wa karibu sana na nilishawahi kumwambia siku moja twende Pemba mimi nikenda akanambia yeye yuko kwenye boti. Sasa bahati mbaya pengine sijui alikuwa wapi. Lakini kwa suala hili nakubaliana na Mhe. Hija kwamba ziko nyumba nne zinaingia maji wakati wa mvua na tumeshachukua hatua zifuatazo: Walikwenda watu wangu Afisa Mdhamini na Mhandisi kuziona wakishirikiana na Serikali ya Wilaya ya Mkoani, wakifuatana na Mkuu wa Wilaya ya Mkoani, wakifuatana na Sheha wa eneo husika. Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi hawa watu walikwenda lakini bado hatujatoa chochote.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nimuombe tena Mhe. Hija Hassan Hija mimi Mwenyezi Mungu akipenda kesho nakwenda Dodoma, lakini tukubaliane kwamba nikitoka Dodoma tupange mimi na yeye tarehe 13 tukutane Pemba tukaangalie, tarehe 14 tutarudi zetu Unguja na kwa kurejea gharama zitakuwa juu yangu, kwa kwenda ujitegemee mwenyewe. Ukikubali hivyo basi mimi sina mashaka nikitoka Dar es Salaam tutakutana Pemba moja kwa moja tukaangalie athari ya hizo nyumba na hatua gani tuchukue ili kuimaliza kadhia hii. Ninatarajia kwa sababu tulivyo utanikubalia tu ili suala hili liweze kumalizika. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija pia alizungumzia tatizo la fedha barabara ya Mgagadu/Kiwani. Alisema milioni 400 zimetumika lakini kazi haioni. Ukweli katika hizi fedha milioni 400, milioni 200 zimetolewa kwa barabara, lakini milioni 200 zimetumika kwa kununua vifaa vya ujenzi wa barabara, yaani kila eneo tulichukua fedha kidogo kidogo kununulia vifaa vikiwemo kutoka Kampuni ya Nishizawa tulinunua *low loader* na *dump truck.* Kwa hivyo, vifaa hivi vipo ambavyo vitafanya kazi huko Mgagadu na sehemu nyengine za idara hii pia vitafanya kazi hiyo iliyokusudiwa.

Halafu Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Haji Mkema Haji, Mhe. Hamad Masoud Hamad, Mhe. Zakiya Omar Juma na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui walizungumzia hoja ya uharibifu wa mazingiara katika eneo la Mwambe.

Mhe. Mwenyekiti, kweli wakati wa upanuzi wa barabara kama inavyojulikana ni lazima uharibifu wa mazingira utatokea na hili limeonekana mapema na mradi umeweka msimamizi maalum ambaye anaangalia maendeleo ya mradi na uharibifu unaotokea, ili baada ya mradi kukamilika hatua za marekebisho zifanyike. Ni kweli eneo la Mwambe lina uharibifu wa mazingira, lakini kwa mujibu wa mikataba yetu hata kama tutajenga sisi wenyewe kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara, basi baada ya mradi huu tutakwenda kushughulikia tutapanda na migomba mle na mambo mengine ili kuhifadhi mazingira katika eneo lile.

Mhe. Rashid Seif Suleiman alizungumzia kwamba kazi mbili zinafanywa na eneo moja kwa hivyo ni vigumu sana kutekeleza kazi hizi hasa za uzibaji wa mashimo. Mhe. Mwenyekiti, tunapenda kumuarifu kwamba vitengo vyote vipo na tunajaribu kurekebisha kasoro zilizojitokeza ili kuweza kuviimarisha. Kuna vitengo vya matengenezo tu na kuna vitengo vyengine vya shughuli nyengine katika Idara yetu ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara.

Kuhusu barabara ya Wesha – Ndagoni na akataka Mhe. Rashid Seif Suleiman ipewe mazingatio maalum. Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu tayari imeliona tatizo hilo na tayari imewekwa katika mpango maalum wa matengenezo kupitia fedha za Mfuko wa Barabara. Namuomba Mhe. Mwakilishi aangalie kiambatanisho Nam. 5B barabara Nam. 6 Wesha – Mkumbuu ataona suala hilo limo kama tulivyolipanga.

Ujenzi wa barabara ya Amani – Mtoni nafikiri hili liliulizwa na Mhe. Ali Denge Makame. Barabara hii imo katika mpango wa mwaka 2010/2011 ambayo inapatikana katika kiambatanisho Nam. 4 barabara Nam. 12. Kazi zinazohusu barabara ndogo ndogo zitazingatiwa wakati wa utekelezaji. Aidha, ujenzi wa matuta sehemu mbali mbali ni mpango wa wizara kuweka utaratibu maalum kwa matuta sehemu zote zinazotaka kuweka matuta.

Mhe. Ali Denge Makame pia alizungumzia magari ambayo hayana viwango hayapendezi machoni mwa watu. Inawezekana gari ina viwango lakini huipendi. Maana hata binadamu inaweza kuwa mtu mzima ana afya nzuri lakini humpendi kwa sura yake. Sasa Mhe. Denge gari usiitathmini kwa sura yake, itathmini kwa viwango vyake. Kwa hivyo, sisi kama wizara tunaangalia uzima wa gari na kama iko freshi tunairuhusu itembee barabarani. Tusiangalie gari kwa kuangalia umbo lake la mbele.

Mhe. Moh'd Ali Salim alizungumzia kwamba barabara zinafanywa na nguvu kazi badala ya mashine. Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa barabara za *NORAD* unajumuisha kazi kwa kutumia mchanganyiko wa zana na nguvu kazi kwa lengo la kuwapatia ajira wananchi zinamopita barabara hizo. Tayari vifaa vimenunuliwa na mradi huu na vitabaki idarani kama ni vyetu mara baada ya mradi kukamilika. Vifaa hivyo vilivyonunuliwa ni:

1. Kijiko – 1
2. Magari – 2 *(tipper)*
3. Magari – 5 (madogo)
4. *Roller* ndogo – 9
5. *Mixer* - 15
6. *Vibrator* – 5
7. *Fuel Bulldozer* (ndogo) – 3
8. *Genereto*r *& welding machine* – 1
9. *Water Bowser* (ndogo) – 3
10. Pikipiki - 10

Kuhusu lini barabara ya Mizingani – Wambaa itaanza kusafishwa. Mhe. Mwenyekiti, barabara ya Mizingani – Wambaa tayari kazi za usafi na matayarisho ya ujenzi wa *culvert* utaanza tarehe 12/7/2010 na tayari wananchi 50 wa Shehia za Mizingani na Chumbageni wameshapatiwa ajira hiyo. Pengine ulipoondoka ilikuwa bado lakini mambo yako mazuri na wiki iliyopita wameshafanyiwa mkataba wa ajira.

Kuhusu hoja ya kuangaliwa/kutengenezwa barabara ya Mbuguani – Tironi. Mhe. Mwenyekiti, barabara hii imo katika mpango wa matengenezo ya mwaka 20010/2011 ambayo itagharimiwa na fedha kutoka Mfuko wa Barabara. Tunaomba uangalie kiambatanisho Nam. 5 sehemu B, ukurasa wa 72 barabara Nam. 12.

Kuhusu kazi ya matengenezo ya Gati ya Mkoani itafanywa kwa kutumia mafundi wa Shirika la Bandari. Mhe. Haji Faki Shaali, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui na Mhe. Hamad Masoud Hamad. Ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Zanzibar kufanywa kwa umakini na uwekaji wa vifaa vya kisasa. Mhe. Mwenyekiti, ujenzi huu utagharimu Dola za

Kimarekani zipatazo milioni 70.4 zikihusisha ujenzi wa jengo sehemu ya kuegeshea ndege na *aerobridges* ambazo tutakuwanazo kama 3 kubwa na moja ndogo. Kwa hivyo, nafikiri itakuwa ya kileo kabisa. Hizi fedha ni mkopo nafuu kutoka *Exim Bank* ya China. Pia tutakuwa na *access road* katika eneo lile la Uwanja wa Ndege pale. Mhe. Mwenyekiti, tunataka kufanya mambo na sisi tuonekane kama tuko duniani. *(Makofi)*

Jengo hilo la kisasa litatumika kwa safari za kitaifa na kimataifa, lakini zitatofautishwa kama ilivyo katika Kiwanja cha Mwalimu J. K. Nyerere Dar es Salaam. Wizara itahakikisha kuwa vifaa vitakavyowekwa vitakuwa vya kisasa na kuendana na wakati.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui alitaka uanzishwe utaratibu wa kuwapatia kazi za matengenezo na kuruhusu kufuatwa *road design* na *road safety*. Mhe. Mwenyekiti, mpango huu wa kuwapa wazalendo kazi wizara ilianza tangu mwaka 2009/2010 na unaendelea kuokoa kuimarisha siku hadi siku. Kama Mhe. Mazrui na wewe kampuni yako inajenga barabara tunakuruhusu uombe kazi kwa wizara yetu.

Mhe. Haji Faki Shaali alisema hoja zake wananchi waliopoteza mali zao kwenye meli ya MV Fatih nani atawalipa. Halafu Zanzibar haimo kwenye orodha ya wanachama wa *IMO* wala *associate members* (wanachama washiriki) na nani anawakilisha Zanzibar katika mkutano wa *IMO*.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya kwanza kuhusu fidia ya mizigo iliyopotea katika MV Fatih ni kuwa mwenye meli ndio anayewajibika kulipa fidia ya mizigo kwa kushirikiana na Kampuni ya Bima. Meli hiyo ilikuwa na bima ya ukamilifu kuhusu mizigo na mambo mengine. Hata hivyo, mwenye meli bado hajalipwa fidia ya mizigo kutoka Kampuni ya Bima jambo ambalo limesababisha mwenye meli kushindwa kuwalipa waliopoteza mizigo katika ajali hiyo.

Kuhusu uwanachama wa *IMO* kwa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi nimekuwa nikijibu suala la Zanzibar kuwa mwanachama wa *IMO* au mwanachama mshiriki. Nachukua nafasi hii tena kuwaeleza Waheshimiwa Wajumbe kuwa uwanachama wa *IMO* lazima uwe ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa. Kuhusu uwanachama ushiriki, wizara inaona kwamba hakuna haja ya kujiunga kwani hakuna faida inayopatikana. Kupitia uwanachama wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Zanzibar inapata ushiriki wa kutosha na inapata fursa ya kupiga kura.

Maana niwaambieni siri moja kwamba mara nyingi vikao vya *IMO* vya Tanzania sisi Zanzibar ndio tunavyoongoza kuliko Bara. Hata juzi mimi

nilishiriki na kuongoza kikao kilichofanyika Philippines Manila kuanzia tarehe 21 mpaka 25 mwezi huu, lakini pia mwezi wa 5 tulipata fursa ya kuhudhuria kikao kilichofanyika London na nilishiriki na sisi Zanzibar ndio tuliongoza. Kwa hivyo, wenzetu kule si aghlabu sana kushiriki, wanakuja maafisa wao lakini sio sana. Sasa sisi tunapata hiyo nafasi na ndio tunakuwa kiongozi mshiriki. Kwa hivyo, bado tunafaidika na kuwepo katika *IMO*.

Mhe. Zakiya Omar Juma alikuwa na hoja kwamba tuanzishe shirika la ndege letu wenyewe. Ushauri tunaupokea na sisi hamu yetu kuhusu jambo hili ni kubwa sana.

Lakini pia alizungumzia Chuo cha Utalii kwamba kuna haja Mhe. Rais pale kujenga barabara. Mimi nakubali ipo na nilikuwepo na napenda nimhakikishie kwamba Mwenyezi Mungu akipenda kabla kuondoka sisi Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi hapo mwezi Oktoba, basi barabara ile tunataka iwe imeshatiwa lami pamoja na barabara ya Ikulu Kibweni. Kwa hivyo, haya mambo yapo na tunayafanyia kazi. Kuhusu suala la madereva Naibu Waziri wangu ameshalijibu.

Mhe. Hamad Masoud Hamad alizungumzia kutokuelewana kati ya Mhandisi wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na Mhandisi wa Kampuni ya *MECCO*. Mhe. Mwenyekiti, napenda niwahakikishie wajumbe wako kwamba ni kweli suala hili lilikuwepo lakini tumeshalipatia ufumbuzi wizara imeshamuondoa mhandisi wetu. Sio kwamba tumemuondoa kwa sababu hiyo, lakini wafadhili wa mradi huu wasingependa kwamba mradi ule usimamiwe na wizara yetu sisi katika matumizi bora na utawala bora. Kwa hivyo, mradi huu sasa unasimamiwa na Kampuni ya *Black and Veatch* ya Afrika ya Kusini na wameleta mhandisi wao, matatizo hayo yamekwisha na kazi zinaendelea vizuri.

Mhe. Ali Abdalla Ali udhibiti wa eneo la Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar na kufungwa kwa barabara ya Fumba ya zamani. Mhe. Mwenyekiti, napenda nimhakikishie kwamba ujenzi wa uzio unaendelea na sehemu mojawapo ya udhibiti wa eneo hilo itakuwa ni huo uzio kwa sababu utafunga kabisa eneo lile na halitotumika kwa kupitisha magari na shughuli nyengine.

Lakini pia Mhe. Ali Abdalla Ali alikuwa na ombi la kutiwa lami katika eneo la barabara ya Amani – Mtoni. Suala hili Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu imeshalifikiria, Mhe. Ali nafikiri alituona, hivi karibuni tutaitia lami kutokana na kero ambayo wananchi wa eneo lile wanaipata. Kwa hivyo, Mhe. Ali na wananchi wengine watuelewe kwamba hili suala tunalifanyia kazi.

Kuhusu ombi lake la kupatiwa kifusi gari 6. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nimwambie yeye kama ataweza yeye kabla hajenda Dodoma sijui ataondoka lini basi aonane na Mkurugenzi wa Barabara kifusi gari 6 atapata, hata akitaka kwenda kesho Jumatano basi atapata kifusi gari 6 ili kwenda Mwachealale wakamalize shughuli yao ya barabara.

Mhe. Ali Suleiman Ali Na Mhe. Omar Ali Jadi hili tayari nimeshalijibu la magari yenye matairi mawili kwamba tumesharuhusu.

Mhe. Haji Faki Shaali alizungumzia kupungua kwa meli za kigeni katika bandari ya Zanzibar. Ni kweli kwamba idadi ya meli imepungua na kilichopungua ni idadi ya meli, lakini ukubwa wa meli umeongezeka.

Wakati ule tunajenga bandari kulikuwa kuna vimeli vidogo viko pale Dar es Salaam au Mombasa vinatuletea mizigo moja kwa moja Mombasa/Dar es Salaam/Unguja kwa hiyo zikawa zinaonekana meli nyingi. Lakini sasa hivi tunapokea meli moja kwa moja kutoka nchi ambazo zinapakia mizigo. Kwa hivyo, zinakuja zile meli kubwa na idadi imepungua kwa sababu mizigo yote inakuja moja kwa moja. Ndio maana ukiangalia mapato ya Shirika la Bandari yamekusanywa kwa asilimia 103 kwa sababu yale malengo yamefikiwa kutokana na ukubwa wa meli na wingi wa mizigo.

Mhe. Mwenyekiti, hili liko sawa na bidhaa mchanganyiko kwamba siku hizi zinapungua sasa hivi wateja wengi wanaleta bidhaa kwenye makontena ambazo ni za usalama zaidi na inasaidia zaidi katika maendeleo ya nchi yetu.

Kuhusu Bandari ya Mkoani kuwa ya kimataifa. Mhe. Mwenyekiti, tayari imeshatangazwa kwamba ni mlango wa kuingilia *(entry point)* tangu mwaka 2003 na azma ya serikali kuiendeleza bandari hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kila wakati tunasema kwamba sisi wizara tunawashawishi sana wafanyabiashara wapeleke bidhaa zao moja kwa moja Pemba na wakikubali tuko tayari sisi kuondoa vifaa vyetu vya Unguja kupeleka kule kwa gharama zile zile ambazo tunawatoza hapa Zanzibar. Kwa hivyo, hili nalo wafanyabiashara ni juu yao kuamua lakini tutaendelea kushawishi na kila wakati ili tuweze kufikia malengo.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui alizungumzia mradi wa kujenga jengo jipya la abiria katika Bandari ya Malindi kama inavyoonekana katika kitabu. Ni kweli tuna mpango pale wa kujenga jengo jipya la kuhudumia abiria katika Bandari ya Malindi. Lakini hili huku mbele pia nimelizungumzia kwamba tuna mjadala unaendelea. Mhe. Mwenyekiti, mfanyabiashara Salim Said Bakhressa alitaka kujenga lakini hoja yake ilikuwa kwamba akijenga yeye atumie peke yake.

Sasa eneo letu la bandari sio kubwa sana, tukasema kwamba kama huyu tunamruhusu ajenge atumie peke yake kesho na *Sea Express* wakisema na sisi turuhusiwe tunataka kujenga tutumie peke yetu, akija *Flying Horse* nae hivyo hivyo, inawezekana baadae tukaonekana kwamba labda tuna mtu tunamlinda wengine hatuwataki.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nichukue jukumu la kukubaliana na wenzangu kwamba tumwite Ndugu Salim Said Bakhressa tuzungumze nae, tutaweza kumruhusu ajenge akate upande mmoja atumie mwenyewe lakini upande mmoja watumie wengine ambao watakuwa pia wana huduma za kimeli. Nafikiri hili kama atalikubali basi hii shaka yote itaondoka. Kweli pale Dar es Salaam kajenga vizuri wakati mwengine unaona choyo kwamba huyu ni Mzanzibari mwenzetu kajenga kule vizuri kuliko hapa. Kwa hivyo, nafikiri hili jambo tukilimaliza litakuwa ni jambo jema sana na linaweza kuleta faraja kwa wananchi. *(Makofi)*

Mhe. Zakiya Omar Juma pia alizungumzia mnara wa Kigomasha na Nungwi tayari tumeshajibu. Mhe. Ame Mati Wadi alizungumzia suala la *crane* tayari tumeshalijibu. Mhe. Hamad Masoud Hamad alishauri kumruhusu Ndugu Salim Said Bakhressa ajenge nimeshalijibu hilo. Mhe. Ali Moh'd Bakari ushauri wa kuwa na utaratibu mzuri wa kupitisha Waheshimiwa Wajumbe bandarini badala ya Masheha tunauchukua. Waheshimiwa Wawakilishi nafikiri nao mna hadhi zenu kuliko masheha. Kwa hivyo, hili tutalifanyia kazi.

Mhe. Salim Abdulla Hamad ushauri wake wa kujenga jengo jipya la abiria katika Bandari ya Malindi tunauchukua tutaufanyia kazi. Lakini shirika halina mpango wa kujenga *jetty* karibu na Gati ya Majahazi, hili bado hatulifanyii kazi.

Mhe. Ali Abdalla Ali pia aliuliza lile jengo la vigae pale bandarini linafanya nini. Lile jengo bado lina kesi haijamalizika na kesi ile wasimamizi wakuu ni Wizara ya Fedha sio Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Lakini sisi tunawaomba Wizara ya Fedha ile kesi waimalize hata nje ya Mahakamakwa sababu eneo lile tunalihitaji sana kwa shughuli zetu za kibandari. Kwa hivyo, tutashukuru sana kama Wizara ya Fedha watamalizana na huyu mtu ambaye habari zilizokuwa hazijathibitishwa zinasema huko aliko kafungwa. Sasa sijui kama ni kweli au si kweli. Lakini pia kwa ujumla inawezekana kuna mambo sikuyajibu kwa sababu ya muda naomba Waheshimiwa Wajumbe muelewe kwamba lengo langu ilikuwa ni kuyajibu masuala yote yaliyozungumzwa na waheshimiwa.

Mhe. Salim Abdulla Hamad pia alizungumzia madaraja yake na njia yake ile nyengine. Lakini ni kweli kifusi tumepeleka, hiyo gari uliyosema imerudi

ilikuwa ndio siku ya mwisho tumalizie lakini haikuweza kwenda. Kwa hivyo, Mwenyezi Mungu akipenda baada ya hali ya hewa kutulia tutamalizia. Maana mwaka huu Pemba mvua imenyesha sana kuliko miaka mingi kwa hivyo kazi kidogo zimetuwia vigumu sana lakini tumefanya vizuri. Kwa sababu tumezifanya vizuri barabara nyengine hazikuweza kuharibika kwa mvua.

Mhe. Moh'd Ali Salim Wambaa tutaishughulikia kwa dharura lakini kama nilivyokwambia mwanzo watu wetu wanakwenda wanaanza kazi rasmi tarehe 12 mpaka 15. Laini kule Kwa Azani lazima tukakushughulikie kwa sababu ni kubaya sana, mimi mwenyewe nimeshuhudia kwamba ni kubaya sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hayo naomba nitoe hoja kwamba nimemaliza na nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe. Mhe. Mwenyekiti, hichi ni kikao cha 20 na cha mwisho kwa Baraza hili. Sasa basi nimuombe Mwenyezi Mungu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wote wenye nia ya kugombea waweze kushinda na kurejea tena Barazani hapa. Amin.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tulivyoingia mwaka 2000 walimu wetu walikuwa kina Mhe. Ali Suleiman Ali, Mhe. Ame Mati Wadi, walikuwa wakitwambia ukichangia usisimame hivyo, usisome kitabu sana, lakini bahati nzuri tumeweza. Kule tulikuwepo kina Mhe. Said Ali Mbarouk tulikuwa sana katika kamati moja mimi na yeye. Kwa hivyo, tunawashukuru na walioingia mwaka 2005 na sisi tumewapa kozi kidogo, sasa sote kwa umoja wetu tuje tutoe kozi kwa wawili tu pengine watakaokuja. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri hoja imetolewa na naona imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mhe. Waziri umetumia muda vizuri. Sasa kama ilivyo kawaida niwahoji basi wale wanaokubaliana na hoja hii ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza lako limejadili na kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya wizara yangu. Naomba kutoa hoja.

Kifungu 03	-	Ofisi Kuu Pemba	90,500,000
Kifungu 04	-	Idara ya Mipango na Sera	82,000,000
Kifungu 06	-	Idara ya Anga	1,130,000,000
Kifungu 07	-	Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara	6,000,000
Kifungu 08	-	Idara ya Usafiri na Leseni	345,000,000
		Jumla ya Fungu	**1,653,500,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 26 - Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi

Kifungu 03	-	Ofisi Kuu Pemba	1,100,418,000
Kifungu 04	-	Idara ya Mipango na Sera	

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Kabla sijatoa maelezo juu ya hoja ambayo nataka kuitoa, hapa nitajulikana Ramadhan Nyonje Pandu, nitajulikana Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Sasa nataka kujenga hoja juu ya hotuba yangu ambayo nimeizungumza kama Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Sasa hapa nitajulikana kama Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi au Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu.

Mhe. Mwenyekiti: Mjumbe wa Baraza.

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na naomba kutoa maelezo yafuatayo. Kwanza kwa kuwa nilichangia kwa niaba ya kamati naomba niseme mimi binafsi kama Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi sikuridhika na majibu ya Mhe. Waziri juu ya hoja niliyoizungumzia kuhusu Kampuni *Al ghuruba Marine Service Limited*, juu ya uletwaji wa *crane* katika Bandari ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alijibu tu kwamba serikali ina mpango wa kuleta hiyo *crane* mpya. Lakini kama nimekuelewa vizuri au kama sikumwelewa atakuja kunifafanulia zaidi. Wakati tunasubiri serikali ilete, hatujui lini. Kuna watu wenye kampuni ambao ni wazalendo wa hapa ambao wako tayari kabisa, wakiambiwa kesho au keshokutwa leteni basi siku ya tatu au ya nne inafika. Sasa wakati tunangojea serikali na wenzetu hawa wako tayari na hawa ni wazalendo wawekezaji na kipaumbele tunawapa wawekezaji wazalendo tunavyosema.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri ajaribu kunifafanulia zaidi kuhusu hoja yangu, kwamba mimi sijaridhika na hja hiyo na sijaona mantiki ya kusema serikali iwasubiri mpaka itakapoletwa nyengine.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza Mhe. Ramadhan Nyonje mambo yote anayo, ya Uwakilishi wa Jimbo la Muyuni ndiye, Mwenyekiti wa Mawasiliano na Uchukuzi ndiye na Mjumbe wa Baraza pia ndiye.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu hoja yake ya hii kampuni ya kuleta *crane.* Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba kampuni ilileta barua wizarani, sisi tukasema hatuna pingamizi na hilo. Kwa hivyo, hatukumwambia mwenye kampuni kuwa leta, tukawaambia Shirika la Bandari. Shirika la Bandari kuna *management* na kuna Bodi ya Wakurugenzi. Bodi ndiyo ambayo inatoa maamuzi kwa mambo yote makubwa ya Shirika la Bandari.

Wakimaliza utaratibu kama ni jambo kubwa sana basi wanamletea waziri kupata baraka zake, kwamba Je, Mhe. Waziri tumeamua hivi na tunataka kufanya jambo hili, ruhusa inatolewa au la. Kwa hivyo, waziri anasema endeleeni.

Sasa kwa suala hili *management* baada ya kupelekewa barua wakaifikisha kwenye bodi ya wakurugenzi. Katika kikao chake cha mwezi wa sita, bodi ya wakurugenzi ikataka kujiridhisha kwa kupitia wataalamu hawa *management*. Je, hili jambo mnalotaka tulianzishe faida zake nini na hasara zake nini. Je, mfano tukimruhusu huyu mmoja si na wengine watataka waweke *crane* zao hapa bandarini.

Pili, wakasema wako katika hatua ya mwisho ya mazungumzo na PBZ kupata mkopo wa vifaa, ikiwemo *crane*, boti na mambo mengine. Kwa hivyo, bado wamewaachia kazi *management*, wala serikali haijasema kwamba haitaki kuweka *crane* za watu binafsi, bado tunasubiria jibu la bodi. Katika utawala bora ni vyema hivyo wanavyofanya wao, kuliko kusema tu sisi leteni, wekeni na halafu matatizo mengine yakitokezea wanaweza kusema kwamba bodi hawakushirikishwa.

Kwa hivyo, Baraza hili naliomba sana lielewe kwamba hakuna uamuzi wa kukataa uliofanywa kuhusu *crane.* Lakini bado maamuzi ya bodi ni muhimu nayo.

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru, na mimi nawashukuru sana bodi. Kwa sababu Mhe. Ali Suleiman Ali yumo katika bodi, nafikiri ataona umuhimu wa kuwa na *crane* hizi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini Mhe. Waziri amenichanganya kidogo. Barua yake ambayo ninayo, inaidhinishwa kuletwa hiyo *crane*, huku anasema tunasubiri maamuzi ya bodi, sielewi, tunasubiri maamuzi ya bodi, tunafuata barua hii au vyenginevyo aniambie kwamba barua hii imeandikwa kwa makosa.

Mhe. Mwenyekiti, niruhusu nisome hii barua. Barua hii ameandikiwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari Zanzibar kuhusu ruhusa ya kuingiza *crane* kwa ajili ya meli za Al Ghuruba Marine Services Limited. Wizara imepokea barua kutoka Kampuni ya Al Ghuruba Marine Services Limited ya Zanzibar ya kutaka ruhusa ya kuingiza *crane* mpya kwa ajili ya meli za kampuni hiyo. Kutokana na ombi la kampuni hiyo, huyu mwandishi anasema nimeagizwa na Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasilinao na Uchukuzi, nikujulishe kuwa ruhusa ya kuingiza *crane* hiyo inatolewa.

Sasa inatolewa, sijafahamu. Kwetu mimi Jambiani, inatolewa hiyo ruhusa inatolewa au inatolewa ruhusa haitolewi. Inatolewa ruhusa au inatolewa ruhusa haitolewi. Sijui kama umenipata vizuri. Nifafanuwe zaidi.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana, umefahamika.

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu: Haya. Hivyo, unaombwa uwasiliane na kampuni husika kwa hatua za kuingiza *crane* hiyo. Naomba kuwasilisha kwa hatua zako, wako mtiifu Makame S. Ussi kwa niaba ya Katibu Mkuu.

Sasa hapa kuna watu watatu inawezekana kuna *confusion.* Kuna mtu aliyeagizwa, kuna Katibu Mkuu kwa niaba ya wizara. Sasa sijui tunakwenda wapi. Huyu kama barua ameipata, basi inaonekana wizara imeshakubali yale yote. Sasa kama wizara imeshakubali huku kunatokea bodi inazuwia ni matatizo. Contradiction Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Ali Suleiman Ali upo kwenye bodi. Mhe. Mwenyekiti naomba hili suala, kwa sababu huyu mmeshamtia tamaa halafu leo mnamnyang'anya kwa mkono mwengine, ni matatizo. Mimi naomba pamoja na maamuzi ya bodi, bodi ina watu tena wasikivu na wenye fikra, wenye mawazo na busara na ni watu wanaopenda maendeleo ya Wazanzibari. Kwa hivyo, kuletwa *crane* moja au mbili basi haijaathiri utendaji wa shughuli za serikali. *Concept* ya biashara huria iko wapi Mhe. Nassor Ahmed Mazrui nifahamishe, kwa sababu ulikuwa katika sijui *board of chamber*

Mhe. Mwenyekiti: Fupisha basi swali lako Mhe. Mjumbe.

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu: Haya. Sasa naomba ile dhamira au dhana ya biashara huria iko wapi, wakati wafanyabiashara wanazuiwa wasilete vitu,

maana yake kuna kuwa na *monopoly* katika biashara. Sasa Mhe. Mwenyekiti naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, labda Kiswahili changu mimi kwetu Donge na kwao Jambiani hatuelewani. Lakini nasemaje, hiyo barua haikupelekwa kwa kampuni, hamna kabisa humo kwamba kama anavyosema kuwa kampuni imeshatiwa tamaa, sioni na hebu ainukuu tena na aseme kwamba kuna nakala kwa kampuni ya Al Ghuruba.

Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa ni mawasiliano ya ndani kati ya wizara na Shirika la Bandari. Tumeruhusu au tumesema sisi tunaruhusu, lakini hatujawaambia kwamba waambieni walete. Tumesema wasilianeni na kampuni hii ili muweze kumalizana. Lakini bandari ndio wakatuambia wakaipeleka kwenye bodi yao ya wakurugenzi, hawawezi wakakaa kikao cha bodi ya wakurugenzi na sisi lengo letu ni kwamba kama bodi inakubali basi sisi hatuna matatizo ndio maana tumetoa ruhusa hiyo. Kwa hivyo, mimi silioni kosa liko wapi hapo.

Sisi kama wizara kama wao bandari hawawezi kuagizishia, sisi hatuna matatizo na mtu mwengine kuweka, lakini kama wao wana mpango wao mzuri wa kuagizia *crane* na bodi ikathibitisha hivyo, basi sisi hatuna matatizo na bodi hawajakataa. Kwa sababu bodi yenyewe imekutana imetaka kujiridhisha. Sasa bodi bado haijajiridhisha sisi tutakurupuka vipi kutekeleza jambo hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nadhani kimsingi hiyo barua imekubalika, hilo suala linafanyiwa kazi. Kwa hivyo, kinachofuatia ni utaratibu wa utekelezaji wa hiyo barua na katika utaratibu huo lazima bodi nayo iwe na mkono wake. Nadhani tuendelee tu.

Kifungu 04 Idara ya Mipango na Sera

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, mimi nina jambo dogo sana. Wakati nilipokuwa ninachangia Mhe. Mwenyekiti, nilipendekeza na nilimuomba Mhe. Waziri huduma za uwakala wa meli aziondowe katika Shirika la Meli, kwa sababu zile pesa za uwakala ni pesa zinazopatikana bila ya matatizo yaani zinaingia kirahisi sana. Sasa kuziingiza katika shirika ni kwenda kuzitupa, ingekuwa kile chombo cha mamlaka kiko *independent* zisiingie kule, basi zingefaa katika kuendesha nchi. Lakini matokeo yake pesa ya uwakala wa Shirika la Meli inayopatikana inaingizwa katika Shirika la Meli, haingii katika *circulation* tena ya nchi. Kwa hivyo, inakuwa hazisaidii kujenga nchi, badala yake zinaingia katika shirika na zinaangamia nchi haifaidiki. Naona suala hili kwa bahati mbaya hakulitolea kauli.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, nilianza mwanzo kusema kwamba pengine kuna mambo ambayo sitoyasema kwa sababu ya muda, lakini sio kwa kuyadharau. Kama tunavyosema siku zote hata kwenye bajeti yetu hii kwamba lengo letu ni kufanyia mabadiliko muundo wa Shirika la Meli. Sasa kuna mambo tutakapofanya muundo mpya wa shirika yatajitokeza, tutaangalia kama je, kuna umuhimu wa kuwa na uwakala kwenye Shirika la Meli au uwakala uwe mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa hivi, Waheshimiwa Wajumbe wote hapa, sote tumesema kwamba kuna umuhimu wa kuendelea na Shirika la Meli kutokana na mazingira ya nchi yetu. Sasa hivi Shirika la Meli lina wafanyakazi 164, mahitaji halisi ya Shirika la Meli ni wafanyakazi 100, ni karibu sijui zaidi ya 40 kwamba hawahitajika. Lakini sasa huwezi kumfukuza mtu kazi hivi hivi tu, kuna taratibu zake na sheria zake. Ndio maana tunataka kuanzisha mfumo mpya wa Shirika la Meli. Ukisema sasa hivi wakala unauondoa leo bila ya kulifanyia muundo mpya utaliuwa hilo Shirika la Meli, maana wafanyakazi watafanya nini, watapatawapi mishahara.

Mhe. Mwenyekiti, nilimsikia Mhe. Abass Juma Muhunzi alikuwa na hoja ya msingi, kwamba matokeo ya wafanyakazi wengi wa Shirika la Meli, wasilaumiwe Shirika la Meli. Taratibu za ajira zamani zilikuwa mbovu au zilikuwa mbaya sio mbovu. Sasa wafanyakazi wamekuwa wengi, pale unaweza kukuta mabaharia wa nchi kavu na mabaharia wa melini. Kwamba wengine wako juu hata miezi sita na wengine wako baharini, sio ile *sign off sign in* hapana. Wao hawana kazi tu pale kwa muda.

Kwa hivyo, jamani Mhe. Haji Faki Shaali nakuomba sana hili jambo kwa ujumla wake linafanyiwa mchakato lote zima kwa ajili ya Shirika la Meli. Tupate vyombo, tujuwe idadi ya wafanyakazi na tujuwe pia mfumo wa ajira. Sio vizuri kwa mfanyakazi wa meli tangu ana miaka 18 mpaka miaka 60 ndio anastaafu, kwenye meli haiwi hivyo. Lakini kutokana na mfumo wetu wa ajira sasa hivi uko hivyo, kwamba mtu mpaka afike miaka yake 60 pale ndio aondoke, wafanyakazi wa meli hawafanyi kazi hivyo duniani.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, mimi sijaridhika sana, lakini kwa sababu waziri kasema tusubiri muundo mpya wa shirika. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatupa maisha marefu ili tushuhudie kitu hiki kikitoka na mimi furaha yangu ipatikane.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mhe. Mwenyekiti, kimsingi mimi nilikuwa nina hoja katika maeneo mawili. Nimpongeze rafiki yangu kwa sababu na mimi ni mpiga kura wake kule Chumbuni, nimwambie tu kwamba hoja ya mwanzo ya kimazingira katika

uharibifu wa nyumba nimekubali tuende tarehe 13 na kwa sababu wewe umekubali kutoa nauli, mimi nitatoa mbuzi kwa ajili ya safari hiyo.

Hoja ya pili, naomba kupata majibu sasa hivi na bila shaka tutaelewana. Kuhusu ujenzi wa barabara ya Mgagadu Kiwani ambayo mliitengea shilingi milioni 600, mkatumia milioni 453 sawa na asilimia 76. Kwenye bajeti haikuelezwa kwamba fedha hizi ni pamoja na vifaa. Sasa nani aliyewapa idhini milioni 200 kutafuta vifaa na milioni 200 mkajengea, kwa sababu hili ndio lililofanya ile barabara isimalizike hadi leo. Naomba ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa mamlaka ambayo waziri anayo na sheria ya Zanzibar na uwezo wa kuhamisha kifungu kutoka kifungu kimoja mpaka kwenye kifungu chengine. Lakini kuna fomu maalum tunazijaza zinakwenda Wizara ya Fedha na Uchumi. Kwa hivyo, fungu hili unaweza kuliona limetumika sana, kumbe fedha zile zimetumika kwenye fungu jengine.

Kwa bahati mbaya mambo yamekukumba kwako wewe. Wewe nafikiri umechukulia bajeti kuu ya serikali, watakapohamisha fungu ni lazima waandike kwamba fungu la barabara ya Mgagadu Kiwani ndio limetumika. Lakini inawezekana fedha kama nilivyokuambia zimetumika kwa vifaa vyengine.
Kwa mfano, hata tulivyonunua lami sisi. Tulichukua fungu kutoka, ni fedha za mfuko wa barabara, lakini fungu la barabara Pemba, tukachukua na barabara Unguja waziri akasaini ndio tukapewa hizo fedha tukaagiza lami tani 1,000. kwa hivyo, haya ni mambo ya kawaida, kwa sababu ujenzi wa barabara ni vifaa, lami, mafuta na mambo mengine, bila ya vitu hivyo huwezi kujenga hata hiyo ya Mgagadu Kiwani.

Kwa hivyo, Mhe. Hija Hassan hili usiwe na wasi wasi nalo, kama hujaridhika na wewe uko katika kamati ya PAC, uje siku moja tukuoneshe vocha na mambo mengine yalivyotumika katika shughuli hizi, ziko kwa uwazi kabisa hazina matatizo yoyote.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, unajua *Wallah* mimi sio mtaalamu wa ujenzi wa barabara. Lakini pale nilimsikia akiniambia tumenunua vifaa, vifaa kwa maana ya nyenzo. Hivi sasa ananiambia ni mambo ya lami na mengine. Sasa ni lami au ni vifaa vya kujengea, maana yake kama ni lami, sawa labda kuna lami ya barabara ya Mgagadu Kiwani na kama kuna vifaa vya kujengea ni maalum kwa barabara hii tu na kwa nini msichukuwe sehemu nyengine tukafanya kote kwa ajili ya barabara zote, kwa nini mchukuwe hapa tu

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Mhe. Hija Hassan Hija hajanielewa kidogo. Ile ya lami nimeitolea mfano tu, kama tulivyochukua kwengine. Hivyo vifaa pia sio kwa barabara ya Mgagadu tu, ni sehemu ndogo sana ya fedha, tumetumia karibu milioni 900 kwa hivyo vifaa. Sasa barabara ya Mgagadu tumechukua milioni 200 tu, nyengine tumechukua katika vifungu vingine ili kupata fedha hiyo milioni 900 kwa ajili ya kununua vifaa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nadhani waziri kwa sababu ana maandalizi ya Dodoma kesho, na kwa sababu tunakwenda Pemba basi haya yatakaa sawa. Tuendelee.

Kifungu 04	Idara ya Mipango na Sera	748,118,000
Kifungu 06	Idara ya Anga	763,418,000
Kifungu 07	Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara	

Mhe. Omar Ali Jadi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, maana nilikuwa nataka kutoka tena, maana nimepiga buti mara nne hujanipa, lakini nashukuru kwa kuniona.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia katika barabara za ujenzi za Kaskazini Pemba vijijini, niliweza kumuuliza waziri na sikupata ufafanuzi, maana kanijibu kwa kunichanganya mimi na Mhe. Said Khelef, lakini alimjibu Mhe. Said Khelef mimi kaniacha, alinitaja tu kisha akaniacha hivi hivi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka kujua tu, katika kiambatanisho nambari moja barabara ya Kojani inaendelea kujengwa au inataka kujengwa, sikupata jibu. Mwaka jana aliniambia mwezi wa tisa itajengwa na pesa zimeshaingizwa mwezi wa nne, kwa bahati nzuru ukapita. Nina imani ule ni mwaka wa kusherehekea ile fedha kuingia tu pale. Je, mwaka huu kwa sababu ananiambia tayari imeanza kujengwa na haijajengwa, waziri ataniambiaje ili wananchi wangu wa Kojani wasikie kwamba itajengwa mwaka gani, maana sina imani kuwa itajengwa kwa kipindi hiki. Kweli kwenye bajeti ameingiza na kwenye kiambatanisho anasema hivi. Kwa hivyo, nataka nijuwe barabara ya Kojani inajengwa au itajengwa na itajengwa lini?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, kiambatanosho nambari moja, nafikiri na Mhe. Hamad Masoud alizungumzia kiambatanisho hiki pia. Kuna barabara za upande wa kulia zilizojengwa tayari zimeshakamilika na kuna barabara nyengine ambazo zinaendelea kujengwa. Sasa labda lugha tu tumetofautiana, kwamba hizi barabara tano zote za

Kaskazini Pemba ikiwemo ya Kojani, ukizungumzia kujenga kwa ma-*bulldozer* bado hazijaanza kujengwa, kwa sababu kuna mambo ya msingi yameshafanyika. Sasa sisi tunapofanya *design* na mambo mengine hivyo ndio tunasema ujenzi umeanza.

Mhe. Mwenyekiti, unajua barabara ujenzi wake unahatua nyingi sana kuliko mambo mengine, kuangalia ujenzi, usafishe na ufanye mambo mbali mbali. Hata hicho kifusi chenyewe unakiweka katika karibu *layer* tatu za barabara. Kama mimi au mtu mwengine aliyekuwa hajui mambo ya barabara, akiona kifusi cha mwanzo basi anaweza kusema barabara hii tayari imeshajengwa, lakini kuna hatua kubwa. Kama unataka kusema kuwa kwa kupeleka *bulldozer* na mambo mengine basi nikiri kwamba bado haijaanzwa kujengwa. Kwetu sisi ambao tuna faraja kubwa kwa hatua tuliyofikia, kwa sababu hata ukishapata kwamba sasa zabuni ya mjenzi uanze basi hapo sisi tunasema ujenzi ndio tunasema umeanza na tunatarajia kwamba mwezi wa September barabara hizi za Kaskazini Pemba zitajengwa. Nafikiri Mhe. Omar Ali Jadi, umenielewa sasa.

Mhe. Omar Ali Jadi: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri sina wasi wasi sana. Mimi nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa hatua moja aliyonifurahisha, maana anasema ni awamu ya pili au mwaka wa pili mfululizo nguvu zote za ujenzi wa barabara anazielekeza Pemba. Kwa hivyo, nafikiri barabara ya Mgagadu na Kiwani Mhe. Mwenyekiti, haijawa tayari ishajengwa na mimi yangu itakuja kujengwa japo mwaka wa 2050. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 07

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru sana, nilipochangia nilimwambia Mhe. Waziri kuhusu barabara ya Chuo cha Kiislamu na nikamwambia kwamba barabara unazozitaja katika maeneo huru na kule Micheweni ni moja katika sehemu ya maeneo huru. Nilimwambia kwamba kwa bahati mbaya barabara hizi za maeneo huru kule Micheweni, pamoja na hii ya Kiuyu hata kuitaja hukuitaja. Kwa bahati nzuri alipotoa majumuisho, kwa bahati mbaya naona alisahau hata kusema, lakini mimi simlaumu sana kwa sababu naona waziri ana mambo mengi.

Kwa hivyo, nilitaka anitolee ufafanuzi kuwa vipi na nilimlalamikia sana na nikapiga kelele sana, kuhusu vifaa vinatoka kule kwetu lakini hata kile kifusi hatutiliwi. Kwa hivyo, naomba anijibu Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, Mhe Subeit Khamis samahani sana sikukutaja katika barabara yako. Kuna barabara ya Mjini Wingwi na kumalizia barabara ya Micheweni Kiuyu.

Kwanza ile uliyosema suruali mguu mmoja tunataka tuje kukuwekea na mguu wa pili. Kwa hivyo, tutakuja kutengeneza ili shughuli iende, usiwe na wasi wasi tutashirikiana Mwenyezi Mungu akipenda Micheweni. Kwa hivyo, ukirudi huko waambie wananchi wako kuwa waheshimiwa watakuja, hii ni ahadi sio ya waziri tu lakini na wataalamu wangu wote, kwamba Micheweni tutakuja kukufanyia kazi yako.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mimi Mhe. Mwenyekiti, unajua sio mkaidi sana. Unajua mimi napenda sana kushumigwa, nikishashumigwa tu basi huwa ninafurahi. Waziri naona keshanishumiga. Kwa hivyo, tuendelee.

Kifungu 07 Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, katika kuchangia kitabu kimeeleza katika ukurasa wa 68 wa barabara ya Bagamoyo Kele yenye urefu wa kilomita 3, kazi ya uwekaji kifusi inaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilisema kuwa hii barabara pamoja na kuwa wizara inaazimia kuitengeneza kutokana na umuhimu wake, lakini bado hatakupigwa ile kiparapara au *grader* kazi hii haijakamilika. Lakini Mhe. Waziri aliponijibu aliniambia kazi hii inaendelea nakifusi kipo, sasa sijui kifusi hiki kimewekwa wapi, kwa sababu sijakiona wala kazi haijaendelea ilisita kwa sababu ya mvua.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe hajenda kuona, kiparapara kipo na barabara hii inajengwa. Mhe. Salim Abdalla sijui kama umekwenda hivi karibuni, lakini hatua tuliyofikia sio mbaya kama ilivyokuwa. Tena una bahati mheshimiwa maana na daraja tunakujengea, lakini bado kidogo. Mhe. Salim analijua hilo daraja au kama nadanganya basi niambie, je, halikujengwa au limejengwa.

Mhe. Mwenyekiti: Naona umerudishiwa swali, haya jibu Mhe. Salim Abdalla Hamad.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, mimi sijenda karibu mwezi mzima niko hapa, lakini taarifa za kila leo nazipata. Lilipokwenda hilo *grader* nilipigiwa simu, nikaambiwa limeshaondoka kazi haifanyiki. Mpaka jana nauliza naambiwa kuwa hii kazi bado. Sasa pengine Mhe. Waziri ameelezwa hivyo. Lakini kwa taarifa tu hii barabara kama nilivyosema, ile barabara kuu haipitiki. Kwa sababu ya shida tumefanya mpaka tunapita barabara hiyo hivyo hivyo ilivyo. Kwa hivyo umuhimu wa kutengeneza ni mkubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, ombi langu kwake ni kwamba labda tukubaliane kuwa kifusi bado hakijapelekwa ni taarifa ya kimakosa na kazi itaendelea kwa haraka ili tuweze kuitumia.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, nadhani ukienda kwa Mhe. Hija Hassan Hija, basi upite na kwa Mhe. Salim Abdalla Hamad. Tuendelee.

Kifungu 07	Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara	1,070,683,000
Kifungu 08	Idara ya Usafiri na Leseni	

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, katika kuchangia kwangu jana nilitoa tamko rasmi kwamba naiomba serikali suala la wafanyabiashara wa daladala ambao wanawasaidia wananchi wetu wa Zanzibar wanyonge liendelee na Mhe. Waziri nikamuomba sana kama rafiki yangu au mwanachama wa Chama cha Mapinduzi mwenzangu au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi mwenzangu au simba mwenzangu, lakini kakubali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati kwenye jibu lake amekiri kwa asilimia 100 amekubali, nampongeza sana na naipongeza serikali kwa hili. Naomba tuendelee.

Kifungu 08	Idara ya Usafiri na Leseni	384,363,000
	Jumla ya Fungu	**4,067,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 26 – WIZARA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI

Kifungu 03	Afisi Kuu Pemba	22,606,030,000
Kifungu 04	Idara ya Mipango na Sera	

Mhe. Omar Ali Jadi: Mhe. Mwenyekiti, nina imani kwamba sasa matumaini yangu yanakwenda vizuri na Mwenyezi Mungu *Inshaallah* akupe uwezo zaidi. Kwa bahati nzuri wakati wa kuchangia nilitaka kujua kuhusu utaratibu wa gati ya Mkoani, na nikafanya vichekezo watu wote wakacheka hapa. Maana nilisema aidha itobolewe au ifanywe kama bwawa la kuogelea.
Mhe. Mwenyekiti, lakini madhumuni yangu ni ili kuondoa kero la wananchi kwa gati ile ya Mkoani. Je, ni siku gani au mwaka gani, ili wananchi wapate matumaini japo mwaka wa 2020, lakini wananchi wajuwe au wawe na uhakika kwamba siku fulani ikifika basi tatizo hili la maji litaondoka kwenye gati ya

Mkoani. Sasa Mhe. Waziri katika kujibu sikuyapata majibu yale, kwa kweli nataka ufafanuzi zaidi ili wananchi waelewe kutokana na usumbufu ule.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, suala la Bandari ya Mkoani au gati ya Mkoani tumeshalizungumza sana. Kwanza miaka ya nyuma tulikuwa tunaangalia litakwendaje na tulileta wataalamu mbali mbali, wakiwemo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kampuni kutoka Dernmark wakaangalia.

Pia Mhe. Mwenyekiti, tulisema tusifanye haraka, kwa sababu ile bandari ilijengwa na *COGEFER* kwanza tuiangalie itakwendaje. Lakini mpaka sasa hivi wataalamu wanaturidhisha kwa hatua iliyofikia kuwa sasa hivi tunaweza kufanya matengenezo.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tulikusudia mwaka huu wa fedha wa 2011 basi Bandari ile ya Mkoani tuishughulikie na wataalamu wa Shirika letu la Bandari wana uwezo huo wa kushughulikia. Kwa hivyo, tutafanya kutokana na fedha zetu na wataalamu wetu.

Mhe. Omar Ali Jadi: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu nina imani kwamba serikali ina azma nzuri yakuondoa kero za wananchi. Mimi furaha yangu ni kuliona tatizo lile linaondoka. Ushauri wangu kama itakuwa hizo hatua za kutengeneza gari ile zitachelewa, basi bado ushauri wangu nasema angalau ufanywe japo ukarabati mdogo wa kupunguza yale maji ili wananchi wasipate usumbufu kwa sababu kuna wengine ni waja wazito.

Juzi nilipokuwa napita alianguka mtu, kwa kweli kusema ni aibu kutokana na maji yalivyo na jinsi kunavyoteleza. Kwa hivyo, sina tatizo na waziri namuamini kama ataifanya hiyo kazi. Lakini kwa hatua hiyo kama ikishindikana basi pachukuliwe hatua ya dharura ili yale maji yaondoke. Mhe Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 04	Mipango na Uendeshaji	100,000,000
Kifungu 06	Idara ya Anga	8,791,200,000
Kifungu 07	Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara	21,224,000,000
Jumla ya Fungu		**52,721,230,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makisio hayo.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na hoja hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi, wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano yenu. Itakumbukwa kwamba siku ya Ijumaa tulikubaliana kubadilisha ratiba ya maendeleo ya vikao vyetu. Sasa nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi atowe hoja ya kuahirisha kikao hiki hadi tarehe 13/07/2010, siku ya Jumanne saa 3:00 barabara za asubuhi.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri Kiongozi, naomba kama ulivyosema kutokana na ratiba zetu zilivyo tuahirishe Baraza letu hili mpaka siku ya tarehe 13/07/2010 saa 3:00 asubuhi. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyuwe mkono. Wasiokubaliana nayo. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Nakushukuruni sana kwa mara nyengine Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano mazuri na hatimaye tumeweza kupitisha hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi. Sasa naahirisha kikao hiki hadi siku ya Jumanne ya tarehe 13/07/2010 saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 1:04 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe13/07/2010
saa 3:00 asubuhi)